

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

- 1.Mhe. Kamal Basha Pandu Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
- 2.Mhe. Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
- 4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
- 5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
- 6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary Kiongozi wa Upinzani/“Waziri Kivuli”–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
- 7.Mhe. Haji Omar Kheri Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
- 8.Mhe. Haji Faki Shaali “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
- 9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
- 19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
- 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang’ombe.
- 12.Mhe. Hamza Hassan Juma MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
- 15.Mhe. Samia Suluhu Hassan MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
- 16.Mhe. Burhan Saadat Haji MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
- 17.Mhe. Asha Abdalla Juma MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.

18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	“Waziri Kivuli”-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.

38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyiddin Moh’d Muhyiddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbwe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anacllet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53.Mhe. Asha Bakari Makame	Uteuzi wa Rais.
54. Mhe. Asha Moh’d Hilal	Jimbo la Magogoni.
55.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
58.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
59.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
60.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
61Mhe. Hasnuu Moh’d Haji	Uteuzi wa Rais.
62.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
63.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.

64. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
65.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
66.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
68.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
69.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
70. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
71.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
72.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
73.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
74.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
75.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
76.Mhe. Saleh Ramadhan Feruz	Uteuzi wa Rais.
77.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
78..Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
79.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
80.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim

Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

BARAZA LA SABA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA ISHIRINI NA MOJA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 09 Agosti, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameer Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaali leo hii tarehe 09/08/2010 kukutana kwa kikao chetu cha mwisho kwa ajili ya marekebisho ya Katiba katika ukumbi mpya huu tulionao.

Niwashukuru nyie Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwaoneni kuwa mpo katika ukumbi wetu huu na mko tayati kuendelea na shughuli zetu. Lakini zaidi ya hivyo nataka niwaombe radhi, kuhamia kuna matatizo yake. Unaweza ukatokea usumbufu wa hapa na pale kuanzia kwenye utaratibu wa ukaaji wetu ndani ya ukumbi huu hasa tukielewa kwamba viti viliopo ni vya muda tu kwa ajili ya mkutano huu wa siku tatu unaoanza leo. Lakini tunategemea baadaye tutaweka viti rasmi vinavyotegemewa viwepo katika ukumbi huu.

Lakini zaidi ya hivyo usumbufu wa aina mbali mbali unaweza ukatokea na nimearifiwa hata mitambo yetu bado haijaka vizuri, lakini kwa madhumuni ya kuendeshea kikao basi tunatumia utaratibu karibu kama ule wa kawaida tuliokuwa tunatumia isipokuwa hapa yule Mjumbe atakayeruhusiwa kusema atakuwa anabonyeza alama ya manjano na moja kwa moja pale *control room* atapewa nafasi aseme yule ambaye atakuwa anatamkwa jina lake.

Baadaye nitambo itakapokamilika tutaelekezwa zaidi utaratibu halisi ambao utakuwa unaendelea katika ukumbi wetu huu. Pamoja na hayo kunaweza kutokea usumbufu wa aina mbali mbali natuelewe tu kwamba hiyo ni kawaida unapohamia katika nyumba mpya au hapa isiwe mpya lakini kwa mara kwanza ukihamia basi unaweza ukakuta kuna mapungufu ya hapa na pale.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba radhi sana juu ya usumbufu huu ambao utajitokeza mara kwa mara hapa na pale.

Lakini la pili tulikubaliana kwamba eneo la huku juu liwe kwa ajili ya mamlaka ya Spika peke yake. Spika, huyo sio mchoyo nilitaka eneo hili tulitumie pamoja na Waheshimiwa wengine. Kwa kweli ni kinyume kidogo na mazoea ya kawaida kanuni haisemi kitu iko kimya, lakini mazoea ni kwamba huku anaetumia anakuwa ni Spika peke yake.

Kwa mara hii maeneo ya kuzungumzia ambayo yapo ndani ya program ni upande wa kulia kwa ajili ya mawaziri na upande wa kushoto kwa ajili ya Mawaziri Vivuli. Naomba radhi pia na hilo tukubali tupate usumbufu kidogo kupanda ngazi kwa upande wa mawaziri kwenda kuliani na Wenyeviti wa Kamati wakati wa kuwasilisha taarifa za Kamati na pia vile vile kuwasilisha maelezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu wizara inayohusika. Kwa hivyo, usumbufu huo nao utakuwepo na tunategemea kwenye Baraza lijalo Mwenyezi Mungu akipenda basi tutapata nafasi ya kuweza kujulishwa na kueleweshwa wakati huo maeneo ya kuzungumzia itakuwa yameteremshwa hapa chini kama vile tulivyopendekeza kupunguza muda wa kupanda juu na pengine usumbufu wa hizi ngazi ambazo ziliopo na ile panda shuka inaweza ikajitokeza.

Jengine kwa kuwa ukumbi wetu bado haujawa na kamera ambazo zinaweza zikamchukua Mheshimiwa Mjumbe yule anayezungumza au hata Wajumbe wengine bado nilitoa kibali na naomba hili mlikubali kwa sababu ulibidi matayarisho yaanze mapema kabla hamjaruhusu wageni na wenzetu hawa wanaochukuwa picha za video wawemo humu ndani, kwa sababu ya usumbufu wa uwekaji wa kamera zao.

Nilichukua madaraka kwa niaba yenu ya kuwaruhusu waweke vizuri kamera zao tayari kwa kuendeleza mkutano huu. Nafikiri mtakubaliana na mimi kwamba chombo hiki na wenzetu hawa tumekuwa tukishirikiana nao kwa muda mkubwa kuchukua mambo yote yanayotokea ndani ya ukumbi wetu. Kwa hivyo, niwaombe mkubaliane na mimi juu ya kile ambacho nimekiamua kuwaruhusu kuingia katika maeneo haya ambayo haya ni mamlaka ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi peke yao pamoja na wahudumu wetu. (*Makofi*).

Makofi hayo yananijulisha kwamba mnakubaliana na hilo ambalo lilifanywa mapema kwa ajili ya kuendesha vikao vyetu vizuri.

Naomba niwakaribishe wageni wetu waliopo pale juu nao ipo haja ya kuja kushuhudia shughuli hii muhimu ambayo tunaianza leo ya masuala mazima ya marekebisho ya Katiba pamoja na masuala mengine ambayo yametayrisihwa kwa ajili ya mkutano huu wa ishirini na moja. Hizo ni taarifa za awali na sasa naomba nitoe taarifa kwa mujibu wa taratibu zetu za Kanuni.

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa 19 wa Baraza la saba la Wawakilishi uliofanyika tarehe 24 Machi 2010. Baraza lilipitisha miswada mitano ya sheria kama ifuatayo.

Mswada wa kwanza ni wa Sheria ya kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika kesi za madai na utaratibu wa mwenendo wa madai dhidi ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada mwengine ulikuwa na Mswada wa kufutwa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na kuanzishwa sheria mpya ya mamlaka ya Hifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa tatu ni mswada wa Sheria wa kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na kuanzisha sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada mwengine ni Mswada wa Sheria ya kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na mambo yanayohusiana na hayo.

Mswada wa tano ni Mswada wa kufuta Sheria ya Uvuvi na kuweka masharti bora yanayohusiana na usimamizi na maendeleo ya Uvuvi ndani ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Ishirini wa Baraza la saba la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 06 Juni 2010 Baraza lilipitisha Mswada mmoja wa sheria kama ufuatao. Mswada huo ni mswada wa kuidhinishwa matumizi ya serikali kwa mwaka 2010/2011 kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 91 kifungu kidogo cha 3 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2009 naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*).

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa makofi hayo ya kumpongeza Mhe. Rais kwa kukamilisha kazi ambayo tuliifanya sisi ndani ya ukumbi wetu kwenye Baraza hili la 19 na 20.

Waheshimiwa Wajumbe taarifa nyengine ya Spika, ni kama ifuatavyo:-

Kuanzishwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni Sheria namba 6 ya mwaka 2010 na kufanyika kwa kura ya maoni hapo tarehe 31 July 2010. Baraza la Wawakilishi tumepokea salamu za pongezi kutoka

ndani na nje ya nchi zinawapongeza wananchi wa Zanzibar kwa maamuzi yaliyofanywa kupitia kura hiyo ya maoni. Salamu hizo ni kama ifuatavyo:-

Salamu ya kwanza ni tamko ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambayo ametuma kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inasema kama ifuatavyo:-

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anawapongeza wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa hasa wananchi wa Zanzibar kwa hivi karibuni kufanya kura ya Maoni Zanzibar kwa amani kabisa. (*Makofi*).

Aidha Katibu Mkuu huyo amefurahia maridhiano baina ya Vyama Vikuu Viwili vya siasa Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF. Maridhiano ambayo yamepelekea kufanyika kwa kura ya maoni kwa madhumuni ya kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya suluhu ya muda mrefu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ameendelea ametiwa moyo sana na umadhubuti wa wananchi wa Zanzibar katika kujenga mustakabali wao wa Amani na Umoja na nawahakikishia kwamba Umoja wa Mataifa uko tayari kuwasaidia wananchi wa Zanzibar katika maendeleo ya nchi hii. Taarifa hii imetoka *New York* tarehe 04 Aug 2010 naomba mpokee salamu hizi za pongezi. (*Makofi*).

Salamu nyengine za pongezi ni tamko la John Kasoz msaidizi wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekeni anayeshughulikia masuala la Afrika. Maelezo ya salamu hizo inasomeka kama ifuatavyo:-

“Kura ya Maoni ya kugawana madaraka Zanzibar 2 Agosti, 2010 ndio ilivyotumwa salamu hii.”

Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje Hilary Clinton na kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya nje ya Marekeni nawasilisha pongezi kwa wananchi wa Zanzibar ambayo mnao tarehe 31 Julai 2010 kwa amani na kwa mafanikio makubwa walifanya kura ya maoni kuhusu kugawana madaraka. Wazanzibari kwa busara sana wamechagua kuondokana na migawanyiko ya kiuhasama kwa ajili ya kujenga Zanzibar mpya yenye mfumo wa siasa wenye misingi ya amani haki na ujumuishi.

Kura ya maoni ni kielelezo cha hatma ya mchakato mgumu wa maridhiano Marekeni inaungana na marafiki wengine wa Tanzania kuunga mkono mchakato huo. Lakini viongozi na watunga sheria wa Zanzibar kutoka kwenye vyama vikuu viwili vya siasa visiwani humu Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar jumua za kiraia Vyama vya Siasa viongozi wa dini na wananchi wa Zanzibar ndio waliofanikisha mchakato huo. (*Makofi*).

Mafanikio ya wananchi wa Zanzibar ya kuridhia shuluhisho linalotekelezeka zidi ya matatizo ya muda mrefu ni mfano bora kwa wengine duniani ambao wanakabiliwa na changamoto sugu zenye kutatiza na za migawanyiko. Wananchi wa Zanzibar sasa wanafursa nzuri ya kujenga nchi yao kwa mafanikio haya ya kihistoria wakati wanakaribia kwenye uchaguzi mkuu mnamo Oktoba mwaka huu.

Endapo Wazanzibar wataendelea kuchagua utawala wa sheria na ushiriki wa kisiasa kwa amani zidi ya migawanyiko na fujo basi wananchi wa Zanzibar watarajie mswada wa nchi ya Marekeni. Hizo ni salamu kutoka kwa ndugu yetu John Kasoz msaidizi wa Waziri wa Mambo ya Nje ya Marekeni. Naomba mzipokee salamu hizi. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe salamu zilikuwa ni nyingi lakini kwa kifupi vile vile Baraza la Wawakilishi limepokea salamu kutoka kwa wafuatao:-

Children Fund, Mstakabali wa Zanzibar Muwaza, *Istiqama for Development*, Umoja wa Wazanzibar Den Mark, Salamu kutoka Norway, Salamu kutoka Benkok, salamu kutoka Mwalimu Nyerere Foundeshen na salamu za watu na Jumuiya mbali mbali hapa nchini.

Waheshimiwa Wajumbe naomba pia mpokee salamu hizo za Jumua mbali mbali pamoja na wananchi mbali mbali kutoka ndani ya nchi yetu. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana. (*Makofi*).

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi):- Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kuwasilisha Barazani nakala zote za Serikali pamoja na vielelezo vyake kuanzia tarehe 17 Julai 2010 naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana nakuomba ubaki na makatibu kwa sababu ya mambo ambayo yanaweza kujitokeza kwamba Waziri mmoja ana mambo mbali mbali ya kutoa kwa wakati mmoja basi pawe na kiti pale ambacho anaweza kuketi kidogo, tutatayarisha baada ya jambo hili na haya ndio masumbufu ambayo nimeyataja mapema naomba radhi ya Waheshimiwa Wajumbe na nakuomba radhi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Barazani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa muda huu kazi yako imemalizika.

Naomba sasa nimakaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala.

Mhe. Haji Omar Kheri (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilishi mezani hotuba ya maoni ya kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada ya Sheria ya Marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti ni zamu yake sasa Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora. Mhe. Haji Faki Shaali upande wako wa mkono kulia kwa huko.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambayo lengo lake ni kuwezesha kuundwa Serikali ya Umoja ya Kitaifa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri Kivuli. Waheshimiwa Wajumbe tuliona kwamba kwa kuwa shughuli hizi ni mtiririko na muda wetu ni mfupi basi moja kwa moja tuwasilishe na hati nyengine ili mara baada ya shughuli hii ya Marekebisho ya Katiba kumalizika tuweze kuendelea moja kwa moja na mswada mwengine unaofatia. Kwa maana hiyo basi naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha hati mezani ya hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Umilikaji Ardhi namba 12 ya mwaka 1992 na Mswada wa Sheria ya Kondomionio ya Zanzibar.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi .

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti Kamati wa Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya umilikaji Ardhi na namba 12 ya mwaka 1992 na Mswada wa Sheria ya Kondominio ya Zanzibar naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Sasa ni zamu yake Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Maji Ujenzi, Nishati na Ardhi. Waheshimiwa Wajumbe naona mnampa upendeleo maalum.

Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny: Mhe. Waziri wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya upande wa upinzani kuhusu Marekebisha ya Sheria ya Umilikaji wa Ardhi Nam. 12 ya 1992 na Mswada wa Sheria ya Kondominio ya Zanzibar.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisha ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Marekebisha ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyobadilishwa kwa mujibu wa orodha ya mabadiliko iliyoambatanishwa pamoja na mswada wenyewe sasa usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, kikao cha leo cha Baraza letu hili ni kikao cha historia, kikao kinachokusudia kutandika barabara iliyo safi ambayo tunategemea itatufikisha katika mshikamano, amani na utulivu wa nchi yetu. Mhe. Spika, kitendo ambacho tunakusudia kukifanya leo ni mwendelezo wa kitendo kilichofanywa na viongozi wetu wakubwa Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad tarehe 5 Novemba, 2009 hapo Ikulu ya Zanzibar. Maridhiano hayo yaliyofikiwa siku hiyo kusema kweli ndio hasa makusudio ya Mapinduzi yetu matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964.

Mhe. Spika, kila aliyehai leo ambaye alizona harakati za kutafuta uhuru wa nchi hii zilizokuwa zikifanywa na Chama cha Afro Shirazi atakubali kwamba azma ya chama hicho ilikuwa ni kutafuta umoja wa Wazanzibari, amani katika nchi yetu na mshikamano ili kuwapatia watu wetu maendeleo.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Zanzibar kwa uamuzi wao wa kukubali yafanywe mabadiliko ya muundo wa serikali baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2010 kwa asilimia 66.4. Nina hakika wananchi wamekubali kwamba amani, umoja na mshikamano ni kitu muhimu katika nchi ili maendeleo yapatikane. Pia nachukua nafasi hii Mhe. Spika, kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya watu 6 ya Baraza lako tukufu kwa kazi nzuri waliyofanya kwa NGO's, Mashekhe, Wakuu wa dini mbali mbali na Masheha wa Unguja na Pemba kuwaelevesha vizuri umuhimu wa umoja na mshikamano.

Mhe. Spika, pia shukurani zangu za dharti zinakwenda kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu na afisi yake kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kuona marekebisha yanayokusudiwa kufanywa katika katiba yanapatikana kwa wakati. Pia namshukuru na nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Haji Omar Kheir pamoja na wajumbe wake wote wa kamati hiyo kwa maelekezo na mchango wao ambao umesaidia sana mswada huu kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza marekebisha katika vifungu mbali mbali vya Katiba ya Zanzibar ya 1984. Marekebisha yanayopendekezwa yanahusu mambo yafuatayo:

1. Kutekeleza azimio la Baraza la Wawakilishi la mwezi wa Januari, 2010 kuhusiana na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, azimio hilo lilipelekea kupitishwa kwa sheria ya kura ya maoni ili kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kuamua kama wanakubali au kukataa juu ya uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara baada ya uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba, 2010. Kura ya maoni ilifanywa siku ya tarehe 31 Julai, 2010 na matokeo yake kutangazwa siku ya tarehe 01 Agosti, 2010 ambapo wananchi wengi walikubali kuundwa kwa Serikali ya Umoja Kitaifa.

2. Mapendekezo mengine ya marekebisho haya yanatoka serikalini kwa ajili ya kukidhi hali ya mageuzi makubwa ya kisiasa hapa Zanzibar tangu tulipopitisha marekebisho ya 9 ya Katiba ya Zanzibar kwa sheria Nam. 8 ya 2002.

Mhe. Spika, mswada umegawika katika sehemu 2. Sehemu ya kwanza ni utangazaji ambayo inahusu jina fupi na kuanza kutumika na kusomwa kwa sheria hii pamoja na katiba. Sehemu ya pili inahusu marekebisho mbali mbali ambayo yanaanzia kifungu cha 3 hadi 67, marekebisho muhimu yanaanzia katika vifungu vya 3, 4 na 5 vya mswada ambavyo vinapendekeza kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 1 na cha 2 vya Katiba kwa kuitambua Zanzibar kuwa ni nchi ambayo ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, marekebisho mengine muhimu yapo katika vifungu vya 9, 10 na 11 vya mswada. Kifungu cha 9 kinafuta kifungu cha 6(1) na kukiandika upya ili kufafanua hadhi ya Rais wa Zanzibar. Kifungu cha 10 kinarekebisha kifungu cha 27 cha Katiba kwa kufuta kifungu cha 3 kinachohusu siku ya uchaguzi wa Rais. Marekebisho mengine muhimu yapo katika kifungu cha 11 (2) cha mswada kinarekebisha kifungu cha 28 cha Katiba kwa kurekebisha kifungu cha 3 ili kuondoa utata wa ukomo wa mtu kuweza kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar.

Aidha, marekebisho mengine muhimu ni katika vifungu vya 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25, 26, 27, 29 vya mswada ambavyo vinahusu vifungu vya 39, 40, 41, 42, 43, 44, 45, 46 na 47 vya Katiba ambavyo kwa ujumla wake vinafanyiwa marekebisho ili kuwezesha uundaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, aidha marekebisho mengine muhimu ni katika vifungu vya 37, 38, 39, 40 na 41 vya mswada ambavyo vinahusu vifungu vya 63, 64, 66 na 67 vya Katiba ambavyo kwa ujumla wake vinafanyiwa marekebisho kuhusu nyongeza za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Rekebisho jengine ni kwamba iwapo Mhe. Spika, hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi atatambuliwa pia kuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile idadi ya wajumbe kupitia viti maalum vya wanawake inaongezwa kutoka asilimia 30 kufikia asilimia 40.

Mhe. Spika, marekebisho mengine muhimu yapo katika vifungu vya 45 na 46 vya mswada ambavyo vinahusu vifungu vya 78 na 79 inapendekezwa kuwa baada ya mswada kupitishwa na Baraza la Wawakilishi basi Spika auwasilishe kwa Rais ndani ya siku 30. Aidha, Mhe. Rais anatakiwa kuukubali au kuukataa ndani ya siku 90 na endapo Rais atashindwa kufanya hivyo ndani ya kipindi hicho basi mswada huo utakuwa ni sheria.

Mhe. Spika, marekebisho mengine muhimu yanapatikana katika kifungu cha 47 cha mswada ambacho kinapendekeza kuongeza kifungu chengine kipya cha 80 (a) mara baada ya kifungu cha 80 cha Katiba. Inapendekezwa kuanzishwa utaratibu wa kura ya maoni kwa mambo maalum yanayohusu masharti maalum ya Katiba ambayo yatakusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, marekebisho mengine muhimu yapo katika kifungu cha 55 cha mswada ambacho kinahusu kifungu cha 103 cha Katiba. Inapendekezwa kuwa watumishi wote wa Mahakama wawe chini ya uongozi na usimamizi wa Tume ya Utumishi ya Mahakama. Mhe. Spika, marekebisho ya mwisho muhimu yapo katika vifungu vya 57, 59 vya Katiba ambavyo vinahusu vifungu vya 116 na 117 vya Katiba. Inapendekezwa kuanzishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ndicho chombo kitakachosimamia tume zote katika utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ambayo nategemea wajumbe wameupata mswada na wameusoma vizuri na watauchangia vizuri. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya mjadala wa hoja hii ni kwamba kuna mambo tulikubaliana yasaidie katika utaratibu wa mjadala wetu kwenye mkutano huu ambao ni wa siku tatu,

muda inawezekana ikawa ni mfupi kidogo kwa hiyo tukajipanga kwamba tutenge kanuni kando, na kulikuwa na suala zima la kwamba muda wetu hautoshi. Waheshimiwa Wajumbe tulisema kwamba tuongeze muda hadi kwenye saa 8:00 mchana kwa kipindi cha asubuhi na kipindi cha jioni tuongeze muda hadi saa 2:00 usiku.

Tukasema kwamba hata mijadala yetu tujaribu kujikita kwenye waraka huu ambao nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi atoe hoja ya kutenga kanuni kando haipo kwenye waraka huu, lakini pia kuhusu suala la muda ambao unamtegemea Mhe. Mjumbe autumie katika mjadala wetu tulisema tujifunge kwa kutumia muda wa dakika 15. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi sasa atoe hoja kwa ajili ya kutenga kanuni kando juu ya jambo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, muda uliopo kwa ajili ya shughuli za mkutano huu wa 21 ni mdogo sana lakini kuna mambo muhimu ambayo tunapaswa tuyajadili ndani ya muda huu uliopo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba naomba tutumie kanuni ya 150 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 209 na tutenge kando kanuni ya 24 inayohusu nyakati za vikao vya Baraza ili mkutano huu ufanye shughuli zake kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana. Vile vile vikao vya jioni vianze saa 11:00 jioni hadi saa 2:00 usiku. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri vile vile nakuomba uchange na muda wa kutoa hotuba kwa mjumbe ambao tulikubaliana pale juu ziwe dakika 15 changanya na hili tuiamuwe kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Vile vile Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba na muda wa mjumbe kuzungumza katika Baraza hili uwe dakika 15 kwa kila mjumbe kuchangia katika miswada yetu mbali mbali. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni lakini kuna jambo litajitokeza katika kutumia mitambo yetu humu ikitokezea kwamba kuna Waheshimiwa Wajumbe kama wawili watatu wanaomba kwa pamoja basi nafikiri tumia utaratibu wa kawaida ama kuleta karatasi huku au asimame nimwite ili hiyo itawasaidia watu wetu wa *control room* kuweza kumpa nafasi yule mmoja ambaye ameruhusiwa na Spika. Tukibonyeza moja kwa moja kwa kuanza kusema kule *control room* inakataa kwa sababu *programming* wenyewe ni kwa yule ambaye atakuwa ameruhusiwa na Spika.

Kwa hivyo, naomba tutumie utaratibu wa kawaida ama kuleta maombi mapema au kunyanyuka na akaonekana na Spika kuitwa na halafu akipewa ruhusa moja kwa moja wenzetu wa *control room* wataweza kumpa nafasi akasema. Kwa hivyo, twende kwa utaratibu huu.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, napenda kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana asubuhi hii ya leo kwa mara ya kwanza katika ukumbi huu wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kitaifa.

Mhe. Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada huu muhimu wa Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Spika, aidha naomba kutoa shukurani maalum kwa wananchi wa Zanzibar kwa uamuzi wao wa busara wa kukubali mfumo mpya wa muundo wa Serikali ya Umoja wa kitaifa kwa asilimia 66.4. Kwa hakika uamuzi huo waliochukua ni wa busara na unadhihirisha wazi kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawawakilisha wananchi wao vyema. Hii ni kutokana na kuwa mapendekezo yote yaliyotolewa kwenye azimio la Baraza la Wawakilishi juu ya uazishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar yameungwa mkono na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, inaonesha jinsi gani wananchi walio wengi wana hamu na ari ya kutaka kuleta mabadiliko katika nchi yao na kufungua ukurasa mpya wa maisha kwa kusahau tofauti zao za muda mrefu ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sitokuwa mwenye kuitendea haki hata kidogo iwapo sitoipongeza Kamati ya Watu Sita ya maridhiano iliyochini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali, kwa jitihada zao walizozifanya, za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, pia napenda kuwapongeza wadau mbali mbali katika kutoa michango yao juu ya suala hili.

Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila nisipoipongeza Tume ya Uchaguzi - Zanzibar kwa kusimamia vyema zoezi la kura ya maoni. Zoezi ambalo limefanyika kwa mafanikio makubwa, kwa kuendeshwa kwa amani, utulivu na uwazi mkubwa. Kwani hata waagalizi wa ndani na wa nje wamelikubali pamoja na kulisifia zoezi hilo jinsi lilivyoendeshwa. Ni matarajio yetu kuwa mafanikio hayo yataendelezwa katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwezi wa Oktoba, 2010.

Mhe. Spika, kwa moyo wa dhiti napenda kuipongeza Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa kuandaa na hatimae kuwasilisha mswada huu kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili kuipa fursa Kamati yetu kutoa mapendekezo yake kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza letu tukufu kama kanuni ya 83 ya Baraza la Wawakilishi inavyoelekeza.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa kuipitia kwa makini Mswada huu na kupata fursa ya kutoa mapendekezo yao ili kuimarisha zaidi. Mhe. Spika, ili kuzipa nguvu shukurani zangu hizo napenda kuwatambua wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

- | | |
|---------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Haji Omar Kheri | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Haji Mkema Haji | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Mjumbe |
| 4. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin | Mjumbe |
| 5. Mhe. Najma Khalfan Juma | Mjumbe |
| 6. Mhe. Zahra Ali Hamad | Mjumbe |
| 7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |
| 8. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 9. Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Mjumbe |
| 10. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Mjumbe |
| 11. Ndg. Nasra Awadh Salmin | Katibu |
| 12. Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |

Mhe. Spika, naomba unaruhusu pia kuwashukuru, Mhe. Abubakar Khamis Bakary Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni pamoja na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwa michango yao madhubuti waliyoitoa wakati kamati yetu ilipopitia na kuuchambua mswada huu.

Mhe. Spika, Mswada wa Marekebisha ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 umekuja kufuatia, pamoja na mambo mengine kurekebisha baadhi ya vifungu vya Katiba hiyo ili kukidhi haja ya kuwepo kwa muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaohusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2010.

Mhe. Spika, kamati yetu imefanya kazi ya kuupitia mswada huu kwa kina kifungu kwa kifungu na kutoa maoni na mapendekezo yake kwa baadhi ya vifungu kwa kadri ambavyo kamati imeona inafaa.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 3 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 1 cha Katiba, kwenye ukurasa wa 74. Kamati yetu imependekeza maneno ya pembeni ya kifungu cha 1 cha Katiba yasomeke kwenye kifungu cha 2 cha Katiba ambacho kinapatikana kwenye kifungu cha 4 cha mswada na yale maneno ya pembeni ya kifungu cha 2 cha Katiba yasomeke katika kifungu cha 1 cha Katiba. Hii ni kutokana na kwamba maudhui ya maneno ya pembeni ya kifungu cha 1 cha Katiba yanaowana zaidi na maneno ya pembeni ya kifungu cha 2 cha Katiba na yale ya kifungu cha 2 yanaowana na ya kifungu cha 1 cha Katiba.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 20 cha mswada kinachofuta kifungu cha 39 cha Katiba Kamati imependekeza kijifungu cha (3) cha kifungu hicho kwenye proviso kisomeke kama ifuatavyo;-

“Isipokuwa kwamba:-

- (i) iwapo chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya uchaguzi wa Rais kimepata sio chini ya asilimia kumi (10%) ya kura zote za uchaguzi wa Rais; au
- (ii) endapo Rais atakuwa hana mpinzani katika uchaguzi basi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itapewa chama chochote cha upinzani kilichotokea cha pili kwa wingi wa kura za majimbo katika Baraza la Wawakilishi”.

Hii ni kutokana na kuwa asilimia tano ni kidogo, kwani idadi kubwa ya vyama vinaweza vikaifikia. Aidha, kamati imependekeza kuandikwa upya kijifungu hiki ili kieleweke kwa wepesi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 23 cha Mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 41 cha Katiba, Kamati ilipendekeza kuongezwe kwa maneno **“au Makamo wa Kwanza wa Rais”**. Hii ni kutokana na kwamba marekebisho ya awali hayakumjumuisha Makamo wa Kwanza wa Rais katika jukumu hili ambalo na yeye ni mhusika.

Aidha, katika kifungu cha 49(2) Kamati ilipendekeza kuongezwe maneno **“na hatoanza kazi zake mpaka atakapoapishwa”** baada ya neno **“Zanzibar”**. Kamati ilipendekeza marekebisho haya baada ya kubaini kuwa maneno hayo ambayo ni muhimu yamekosekana. Aidha, uzoefu unaonesha kuwa Katibu Mkuu huapishwa kwanza na ndio aanze kutekeleza majukumu yake.

Katika kifungu cha 33 cha Mswada ambacho kinarekebisha Kifungu cha 50 cha Katiba. Kamati ilipendekeza marekebisho katika kijifungu cha 50(1) kama ifuatavyo;-

“Pale Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais au Waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yoyote ya Serikali, atakuwa ndiye Kiongozi na Msimamizi Mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi. Katibu Mkuu ambaye afisi yake itakuwa ni ya Utumishi wa Serikali atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara”. Marekebisho haya yamelenga kukifanya kifungu hiki kuwa katika hali ya uwazi zaidi.

Aidha, kamati ilipendekeza katika kijifungu cha (2) cha kifungu cha 50 cha Katiba kisomeke **“Kutakuwa na Katibu Mkuu katika Afisi ya Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Makatibu Wakuu wengine wa wizara mbali mbali kama rais atakavyoona inafaa”**. Kamati ilipendekeza marekebisho haya ili kukifanya kijifungu hichi kijitosheleze.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 41 cha Mswada ambacho kinaandikwa upya, kifungu cha 66 cha Katiba, Kamati ilipendekeza katika mstari wa tatu kutoka juu viongezwe vijifungu vya **“(a) na (c)”**

baada ya neno “68” na “cha”. Mhe. Spika, tulipendekeza hili ili kutoa nafasi zaidi za uteuzi wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 48 cha Mswada ambacho kinarekebisha kwa kuandika upya kifungu cha 80A cha Katiba, Kamati yetu ilipendekeza kiongezwe kijifungu cha “(h)” baada ya kijifungu cha “(g)” na kisomeke “Vifungu vya 121(1) na 123 vya Sura ya Kumi”. Tulipendekeza haya baada ya kugundua kuwa kuna umuhimu mkubwa wa vifungu hivi kupata ridhaa ya wananchi kabla ya kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, baadhi ya marekebisho yaliyofanywa na Kamati yetu hayakuwemo kwenye Mswada tunaoujadili, lakini Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imeona ni vyema vifungu hivyo vifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia Azimio lililopitishwa na Baraza la Wawakilishi kuhusu uazishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Miongoni mwa vifungu hivyo ni;-

Kifungu cha 9(3) cha Katiba ambapo Kamati yetu ilipendekeza katika kifungu hicho lifutwe neno “pamoja” liliopo baina ya neno “Zanzibar” na neno “na” na badala yake, kuwekwe maneno “kutakuwa na Umoja wa Kitaifa”. Hivyo, kutokana na kuongezwa marekebisho ya kifungu hicho, kifungu cha 6 kisomeke kuwa ni cha 7.

Aidha, katika kifungu cha 16(ii) cha Mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 3(1)(ii) cha Katiba kuongezwe maneno “ambaye anatoka katika Chama anachotoka Rais” baina ya neno “Wawakilishi” na “na”. Mhe. Spika, Kamati yetu imependekeza hivyo kutokana na ukweli kwamba upo uwezekano wa mtu kushika nafasi ya Uspika wakati hawatoki katika chama kimoja na Rais hali ambayo inaweza kuleta mtafaruku wa kisiasa. Sambamba na kwenda kinyume na Azimio la Baraza la Wawakilishi, kwani mtu anayetakiwa kushika nafasi ya kiti cha Urais ni yule ambaye anatoka chama kimoja na Rais.

Hii Waheshimiwa Wajumbe ni pale inapotokea Spika wa Baraza la Wawakilishi ametoka Chama cha Upinzani na masharti ya Katiba yanasema mrithi wa rais anakuwa ni kutoka katika chama chake. Kwa hivyo, hata kama Spika atakuwa anatoka katika Chama cha Upinzani kwa mujibu wa Katiba imeorodheshwa ni nani pale wanatakiwa wakamate zile nafasi, Makamo wa Pili wa Rais, Spika na Jaji Mkuu. Lakini kama Spika anatoka kwenye chama cha upinzani maana yake jambo hilo halitafanyika na badala yake atakamata Jaji Mkuu.

Mhe. Spika, Kamati yetu pia inapendekeza kifanyiwe marekebisho Kifungu cha 33(2)(b)(ii) cha Katiba ya Zanzibar kwa kufutwa na kuandikwa upya, ili lengo la kutoa nafasi kubwa zaidi kwa Mjumbe yeyote wa Baraza la Mapinduzi hata kama sio Waziri kuweza kushika nafasi hii. Hivyo, kamati ilipendekeza kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo;-

“Mjumbe yeyote wa Baraza la Mapinduzi ambaye Rais ataona anafaa”.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imehisi baadhi ya vifungu vilivyopendekezwa na wizara husika kufanyiwa marekebisho, ilipendekeza vibakie kama vilivyo kwenye Katiba. Miongoni mwa vifungu hivyo ni Kifungu cha 35 cha Mswada kinachorekebisha Kifungu 55 cha Katiba. Hii ni kutokana na kifungu hiki kinasomeka kwa ufasaha zaidi kama kinavyoonekana kwenye Katiba ukilinganisha na marekebisho yaliyofanywa.

Aidha, Kifungu cha 16(ii) cha Mswada kinachofuta Kifungu cha 33(1)(iii) cha Katiba kibakie kama kilivyo kutokana na kuwa Spika anaweza kutoka katika chama tofauti na chama cha Rais aliyepo madarakani.

Mhe. Spika, mbali na marekebisho hayo ambayo nimeyaeleza, pia Kamati yetu ilirekebisha baadhi ya vifungu kutokana na makosa ya kiuchapaji. Ili kuokoa muda na kwa kuwa marekebisho hayo yanapatikana katika waraka wetu wa marekebisho ya Mswada husika, nawaomba Waheshimiwa

Wajumbe waupitie waraka huo kwa kina ili wayaone marekebisho mengine ambayo Kamati yetu ilipendekeza ambayo hatukuyaelezwa katika hotuba yetu hii.

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha, haya ndio maelezo ya uchambuzi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muhtasari. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuuchangia Mswada wa Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 na hatimaye kuupitisha ili tujenge Zanzibar yetu mpya na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha kufika pale tulipokusudia. Mimi binafsi kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Tumbatu tunauunga mkono Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya 1984 kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Kivuli, Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora): Mhe. Spika, Kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nasema ingetosha kusimama hapa nikasema naunga mkono hoja. Kwa sababu mambo yote yanakubalika lakini lazima nitoe maelezo machache kwa niaba ya kambi yangu ili tuonekane na sisi tumesema, lakini moyoni kwa dhati yetu sisi tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha maoni ya kambi ya upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, kufuatia kura ya maoni iliofanyika tarehe 31 Julai mwaka huu.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka kwamba tarehe 28 Januari mwaka huu tuliamua kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya kupata ridhaa ya wananchi kwa njia ya kura za maoni. Tuliamua ikiwa uamuzi wa wananchi walio wengi watakubaliana na wazo hilo, Baraza lifanye marekebisho ya Katiba ili kuwezesha mfumo huo wa Serikali uweze kufanya kazi baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2010. Kwa bahati njema, wananchi walio wengi walikubaliana na wazo hilo kwa asilimia 66.4 (66.4%) hivyo kulipa uwezo Baraza letu kufanya marekebisho ya Katiba ili kutimiza shabaha hiyo.

Mhe. Spika, kabla sijaingia katika mjadala wa hoja hii, napenda kutumia fursa hii kulishukuru Baraza Kuu la Uongozi la Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kunitua kuwa mgombea wa uwakilishi katika Jimbo langu la Mkanyageni. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wataniunga mkono kwa wingi katika uchaguzi mkuu wa tarehe 31 Oktoba, 2010 na kufaidi matunda ya jengo letu jipya ambalo kama linavyotarajiwa na wananchi walio wengi litakuza demokrasia.

Mhe. Spika, mswada huu tunaoujadili licha ya kuwemo marekebisho ya Katiba yaliopendekezwa katika Azimio la tarehe 28 Januari, 2010 pia umeingiza mambo mengine ambayo hayakuagizwa katika Azimio la Baraza la Wawakilishi la tarehe 28 Januari, lakini ni mambo ya msingi sana na hivyo serikali inastahili kupongezwa sana na kambi yetu ya upinzani.

Mhe. Spika, vifungu vya 3 na 4 vya mswada huu vinaondoa utata kuhusu Zanzibar kwamba ni nchi au laa. Vimeeleza wazi juu ya hadhi ya Zanzibar kama nchi na pia vimeweka wazi juu ya mipaka yake. Jambo hili litaondoa utata kama uliotokea mwaka jana ambao ulichafua hali ya hewa ya kisisa nchini Tanzania.

Mhe. Spika, vifungu vya 7, 8, na 9 vinarekebisha mambo ya Mahakama ili kuondoa utata mdogo uliokuwepo na kambi yetu haina pingamizi hata kidogo na yote yaliomo katika marekebisho hayo.

Mhe. Spika, kipengele cha 3 cha Azimio la Baraza la mwezi wa Januari 2010, ilipendekezwa muundo wa kuwa na Rais Mtendaji ambaye atasaidiwa na Makamo wawili wa Rais. Makamo wa Kwanza ambaye atatoka katika chama kilichoshika nafasi ya pili katika kura za Rais na Makamo wa pili atatoka katika chama alichotoka Rais. Katika kifungu cha 20 cha marekebisho ya Mswada huu wa Katiba, Kifungu cha 39 cha Katiba kinafutwa na kuweka mapendekezo haya ya Baraza.

Katika kifungu cha 39(3) kipya kinachopendekezwa, pia kinaweka wazi utaratibu wa kumpata Makamo wa Rais iwapo chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya uchaguzi wa

Rais kimepata chini ya asilimia 10% ya kura zote za uchaguzi wa Rais, au endapo Rais atakuwa hana mpinzani katika uchaguzi. Chini ya kifungu hiki, nafasi ya Makamo wa Rais kitapewa chama chochote cha upinzani kilichopata nafasi ya ya pili kwa wingi wa kura za majimbo. Kifungu hiki kitasaidia kuondosha migogoro, kwa vile vyovyote itakavyokuwa Makamo wa Rais hatatoka chama kilichopata nafasi ya Rais.

Mhe. Spika, kipengele cha 9 cha Azimio la Baraza kiliagiza serikali kuwaondoa Wakuu wa Mikoa katika Baraza ili wabaki kuwa watawala tu kama inavyotaka kanuni ya utawala wa sheria. Katika marekebisho haya, kifungu cha 64(d) kimerekebishwa ili kukidhi mapendekezo haya.

Katika kipengele cha 4 cha Azimio la Baraza kuhusu marekebisho ya mfumo wa Serikali, iliamuliwa Rais ateuwe mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo kwenye Baraza. Kifungu cha 24 cha Mswada huu, kinafanya marekebisho ya kifungu cha 42 cha Katiba ili Rais aweze kutekeleza agizo hilo la Baraza kwa uaminifu.

Mhe. Spika, katika marekebisho ya mswada huu kimeongezwa kifungu kipya cha 80A(1) ambacho kinahusu kura ya maoni kwa mabadiliko ya vifungu vya Katiba. Chini ya kifungu kidogo cha 2, kuna vifungu vilivyoainiswa kwamba haviwezi kurekebishwa isipokuwa kwa njia ya kura ya maoni. Marekebisho haya ni ya msingi kwani yatasaidia kujenga imani kwa wadau wote wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mswada huu wa Sheria umesikia kilio cha wanawake kwa kuongezewa nafasi katika Baraza. Kifungu cha 67(1) kimerekebishwa kwa kuongeza asilimia 40 badala ya asilimia 30 iliopo sasa. Hivyo, idadi ya viti vya upendeleo wanawake itaongezeka kutoka wanawake 15 hadi 20.

Mhe. Spika, mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni muhimu sana kwa Zanzibar, kwani utasaidia kuondoa migogoro inayojitokeza baada ya chaguzi. Mfumo huu hutumika sana katika nchi mbali mbali pale panapojitokeza matatizo ya kiuchumi au panapokuwa na matatizo ya vita au panapojitokeza migogoro baada ya uchaguzi.

Mhe. Spika, Canada waliuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika mwaka 1917 wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na waliuunda tena katika mwaka 1940 wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Walifanya hivyo ili kujenga umoja na mshikamano ili waweze kupambana na maadui zao wa nje.

Mhe. Spika, vile vile Uingereza waliuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika Vita Vikuu vya Kwanza na vya Pili vya Dunia. Aidha, waliuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa wakati wa mgororo mkuu wa kiuchumi (*great depression*). Walifanya hivyo ili kujenga umoja na mshikamano wa wananchi ili waweze kukabiliana na matatizo yao.

Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar wamechoshwa na migogoro inayotokea mara tu baada ya chaguzi. Wananchi wana matumaini makubwa na mfumo huu mpya wa serikali, hivyo ni wajibu wetu kuyapitisha marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ili mfumo huo uweze kufanya kazi mara baada ya uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010.

Mhe. Spika, nawashukuru wajumbe wote kwa kuniskiliza na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kuingia katika historia mpya ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika jengo hili baada ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Waziri Kivuli Wizara na Nchi (AR) Kartba na Utawala Bora kama kawaida yangu.

Pili Mhe. Spika, nishukuru tu kwamba katika miongoni mwa wajumbe waliolifungua jengo hili mimi ndio wa mwanzo nimo katika historia ya nchi hii.

Tatu Mhe. Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji wa mwanzo juu ya hatma muhimu ya nchi yetu ambapo sisi tuliopo leo tutaondoka, watakuja wengine wataondoka na vizazi vyetu vyote vinavyotutegemea katika nchi hii vinategemea amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, marekebisho ya Katiba ni jambo muhimu sana katika nchi panapohitajika, maamuzi ya wengi yanapotoka basi huwa huna njia ya kuyaepuka na lazima uyatii na kuyaheshimu matakwa hayo ya wengi. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nasema kwamba nimepokea vizuri na naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani Abeid Karume, nampongeza Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharrif Hamad, naipongeza kamati ya watu sita chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali, nawapongeza wananchi wote wa Zanzibar waliosema “ndio” na wale waliokuwa hawakusema ndio kwa sababu ni demokrasia. Lakini pia nazipongeza taasisi mbali mbali kwa ushauri na maelekezo juu ya usalama na hatma ya nchi yetu.

Mhe. Spika, histotia ya nchi yetu baada ya mapinduzi tulikuwa na chama kimoja, Chama cha *Afro Shirazi Party* na mimi nilikuwa miongoni mwa wanachama wakati huo. Lakini kufika mwaka 1977 tulianzisha mfumo wa chama kimoja cha CCM, miongoni mwetu humu sote Mhe. Spika, tulikuwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi au asilimia 98/99 kama sikosei. Lakini baada ya mambo kugeuka kwa sababu upepo huwa unageuka Mheshimiwa, watu wengine wakasema mambo labda yabadilike na yakabadilika, waliokwenda mkono wa kushoto wakenda tuliobakia mkono wa kulia tupo hapa mpaka leo. Kwa hivyo, hii ni fursa ya demokrasia katika ulimwengu wa leo hupingani na upepo unavyovuma.

Lakini kwa mtazamo wangu Mhe. Spika, baada ya miaka 15 tuliyolumbana tumekwenda na kurudi, kasoro moja tu halikutimia kusema turudie katika chama kimoja, lakini tumetafuta njia ya kuwa angalau tuwe karibu. Kwa hivyo, kwa nia njema kabisa Maalim Seif Sharrif Hamad kapigania vipindi vitatu kama sikosei kaona mambo mazito kwa upande mwengine, lakini baada ya kutafakari na kuangali kwani tunagombana na nani? Akigombana na Shihata baba mmoja mama mmoja, akigombana na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja baba mmoja mama mmoja, turudi tukae meza moja tuzungumze. Kama nilivyosema si rahisi kuamua kama nataka chama kimoja, lakini hivi vyama vyetu tuwe na serikali ya umoja.

Mimi Mhe. Spika, hili naona si baya kwa sababu tunajuana, tunaelewana na tutakuwa pamoja. Kwa hivyo, mimi ushauri wangu katika Katiba hii, mambo yote yaliyozungumzwa naunga mkono kwa dhati kabisa. Naunga mkono kwa hatma ya leo na kesho juu ya wananchi na vizazi vyetu.

Mhe. Spika, kubwa Mhe. Rais kwa nia njema kwa sababu Mhe. Rais ni kiongozi wa nchi hii siku zote nasema, leo akisema hakuna kutoka nje basi hakuna kutoka nje bwana, ndio Amir jeshi wa nchi hii hapa kwetu Zanzibar. Kwa hivyo, Maalim Seif alipoamua mimi nataka hivi na hivi akasema basi, hilo mimi nilikuwa nalitafuta kwa hamu kwa sababu katika Dini zetu zote ya Kiislamu na nyenginezo zinatangaza amani na utulivu na watu wafahamiane.

Mhe. Spika, sisi Wazanzibari asilimia 98/99 ni Waisilamu, lakini tunaishi katika mazingira na wenzetu ambao si Waislamu na tuko kitu kimoja na serikali yetu inasisitiza umoja na upendo na kila mtu awe huru katika maamuzi ya dini yake. Lakini kwa bahati nzuri yanapotokea matatizo mbali mbali hata katika nchi za Kiislamu, wale wenzetu wa upande mwengine wa Kikristo wao ndio wa mwanzo kutaka watu watulie na wafahamiane. Sasa sisi kwa upande mwengine tumepata kura ambazo zimetuthibitishia kwamba kumbe tunaweza kuliko kuingiliwa na watu wengine.

Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Rais, nampongeza Maalim Seif, naipongeza tena Kamati ya Watu Sita. Mimi Mhe. Spika, nilikaa na kuangalia *Zanzibar Cable*, Mhe. Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Kamati hii sijui alipata taaluma wapi, lakini ni mtu ambaye anafaa na ana kila uwezo wa hekma na ana uwezo wa kumuelimisha mtu akafahamu.

Mhe. Ali Mzee kwa bahati nzuri *Zanzibar Cable* watu hawana, lakini kama ingekuwa taarifa ile imetoka katika televisheni yetu ya Zanzibar, basi wananchi wengi walikuwa hawana shida ya kufahamu wangepahamu moja kwa moja bila ya kungoja mambo mengine. Kila kitengo au taasisi aliyoshiriki kuelimisha walikuwa hawazungumzi, watu wako kimya wanamuangalia, wanamsikiliza na anatoa kitu ambacho hata mtoto mdogo anakifahamu.

Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya familia yangu, kwa sababu niliwakusanya watu wazima wakae na kumuangalia na walimuangalia wengine wakasema kumbe huyu mtu mzuri, hawamjui lakini walimjua siku hiyo. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa hilo.

Mhe. Spika, tukiingia katika Katiba kuna jambo moja nataka kupata ufafanuzi. Sisi tuna vikosi vya SMZ (Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar), vinaongozwa na makamanda lakini leo katika marekebisho yetu ya Katiba tunaambiwa kwamba sasa kikosi hiki kitakuwa Idara Maalum. Ninasikia vikosi viko chini ya idara maalum, lakini katika mtazamo wake vitakuwa katika idara maalum, ukurasa wa 81.

Lakini vikosi vilivyotajwa hapa Mhe. Spika, mimi nataka nije nifahamishwe, pameelezwa kwamba Vyuo vya Mafunzo, KMKM, JKU, lakini kuna vikosi vyengine sikuvisikia na katika Katiba naamini vimo. Vikosi hivyo ni vikosi vya Valantia na Zimamoto, hivi vinabakia kama vilivyo au kuna matatizo ambayo yamejitokeza sikuyaona. Naomba nije nipewe ufafanuzi. Kwa sababu kama ni Idara ya Vikosi vya SMZ na hivi vyote vimo humo.

Jengine Mhe. Spika, niseme tu kwamba napongeza kwa dhati kabisa marekebisho haya ya Katiba ukurasa wa 74. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba nisome kidogo sehemu inayosema.

“Marekebisho mbali mbali sehemu ya pili Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyozungukwa na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iliitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar”.

Niliwahi kusema katika Baraza hili hii serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepatikana na nchi mbili, imepatikana na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika ndio ikaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndio maana nikasema pia kama Zanzibar ni nchi ndivyo ilivyo ni nchi kwa sababu tunakuwa na sherehe zetu za Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano anakuja kama mualikwa, lakini Rais wa Zanzibar anaingia mwisho pale kama ni Rais wa nchi.

Lakini jengine lililonifurahisha zaidi ni kwamba kama Rais anaongoza nchi ukiacha Rais wa ZFA au Rais wa Yanga lakini Rais wa Zanzibar anaongoza nchi haongozi Mkoa, kwani kuna sehemu gani katika dunia hii kuna rais wa Mkoa, labda wenzetu walioweka utaratibu wao wa waziri mkuu au nani lakini sisi tuna Rais na lazima ataongoza nchi.

Kwa hivyo napongeza kwa dhati marekebisho haya na naiomba serikali isimamie iangalie kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo la mwisho serikali ina raslimali zake na katika katiba imesema kwamba serikali lazima ilipe na imiliki raslimali zake kwa maendeleo ya nchi yetu, mimi bado naipongeza serikali kwa kuliangalia hili na kuona kwamba wananchi wake wanataka kufaidika katika mambo mbali mbali ya maendeleo na kinachopatikana katika nchi hii ni kuwasaidia juu ya maisha yao.

Mhe. Spika, tukitaka tusitake katika miaka kumi hii tunayomalizia leo yaani hapa tulipo mpaka kufunga Baraza letu mwisho wa Oktoba tuna mambo mengi sana yaliyopatikana, lakini yote kutokana na ile rasilimali kuwekwa pamoja na kinachopatikana kuhifadhiwa na kutumika ili wananchi wakione. Leo tuangalie barabara zetu, tuangalie umeme, maji, bandari, jengo la Baraza hili hapa, Uwanja wa ndege na mambo mengine mengi ambayo hayana kiwango. Kwa hivyo nasema Mhe. Rais aliidhibiti Wizara ya Fedha na Uchumi nampongeza sana na matunda yake yanaonekana haya hapa, mwanzo huu ulitokana na baba yake aliweka historia hiyo hiyo. Baada ya Mapinduzi ya 1964 akasema Wizara ya Fedha iko mikononi mwangu siitoi tumeona matunda yake.

Mhe. Spika, naomba radhi kusema hili na namuomba mwenyezi Mungu aniepushe na hili nitakalosema lisiwe baya na wala kueleweka vibaya, mimi mtoto madhali nimemzaa ata akifanya zuri zaidi kuliko mimi hawezi kujisifu lakini tunaweza kumsema tu naweza kusema hayo nisieleweke vibaya. Mhe. Rais wa kwanza Mhe. Abeid Amani Karume Mungu amrehemu na waliotangulia wote waliopindua nchi hii yeye alituweka njia kwa kufanya mapinduzi ndio leo tukafikia hapa kubwa kuliko yote hilo kaweka.

Lakini pili miundo mbinu aliyoianzisha katika miaka yake minane tumepata viongozi mbali mbali wamejitahidi lakini Mhe. Amani kwa kipindi chake hiki cha miaka kumi hakuweza kumshinda baba yake, kwa sababu baba yake kafanya mapinduzi lakini kafanya mengi kamkaribia baba yake nafikiri nimeeleweka. Kafanya mengi kamkaribia baba yake lakini hakumshinda baba yake maana baba yake kapindua nchi hii ndio tukafikia kuwa hapa.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nawapa hongera wale wote waliopita katika mchakato wa kushinda katika majimbo yao kwa upande wa CCM na CUF, lakini pia na mimi nashukuru kwa kipindi changu cha miaka kumi na tano niliyokaa katika Baraza hili najinasibu nimefanya mengi, jimbo langu wakati huo Jimbo la Mikunguni nilipata soko la Mikunguni la Mapinduzi zuri tu, nimepata skuli yangu ya muungano nzuri, nimepata mradi wa maji *SEMUSO* mzuri, nimepata matawi ya Chama cha Mapinduzi mazuri nimewaweka watu umoja sikuwa na ubaguzi wa mtu, nimesaidia wanafunzi na hata kwenye ajira naweza kusema watu mia nne na nathubutu kusema nimewapeleka katika sehemu mbali mbali.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika, sisi binaadam tunatakiwa lazima tuheshimu maamuzi ya watu na maamuzi ya watu yaliyoheshimiwa haya tuyaheshimu na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakaorudi humu ikiwa tutamwendea kinyume Rais wetu mstaafu baada ya uchaguzi huu Mungu atawahukumu, watakaomgeuka maana yake nasema hili kwa uchungu na nasema kwa nia yangu njema katika nafsi yangu. Mhe. Rais wa Zanzibar hatuna cha kumlipa sote na tuliokuwemo humu kwa mengi aliyoyafanya na mazuri aliyoyafanya lakini kati yetu kila mtu ana nafsi yake katika moyo wake.

Kuna wengine humu humu ndio na kuna wengine humu humu sio, kwa hivyo mimi naomba na naliomba Baraza lijalo nalisema hili na machozi yatanitoka kwa uchungu wa Rais anayeondoka katika madaraka kwa kutupatia mwangaza mkubwa mataa yanang'ara hapa, barabara zinang'ara, umeme unang'ara na maji yanang'ara mpaka Pemba pia. Lakini kwa kuwa muda umekwisha nataka niseme tu kwamba Rais wetu tumuenzi na tumuenzi na kuhakikisha kwamba yeye ni kioo kwa atakayekuja yoyote hana shida akachukue tu kwake Mheshimiwa nisaidie fakira hizi kwa sababu ni mbunifu na mtafutaji ndio mafanikio haya tuliyoyapata. Vyuo vikuu hivyo hapo na mambo mengine chungu nzima mahospitali na kila kitu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa heshima kabisa na taadhima nasema tena kwamba naunga mkono mswada huu wa marekebisho ya katiba na naomba wenzangu wachangie tutizame hatima ya nchi yetu huko mbele tunakokwenda tuishi salama na tuendelee na maendeleo. Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Fatma Abdulhabib Fefeji: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kidogo katika mswada huu wa marekebisho ya kumi ya katiba ya Zanzibar

ya mwaka 1984 ambayo chanzo chake kimetokana na mazungumzo ya Baraza kuhusu uanzishwaji wa serikali ya umoja wa kitaifa, mimi ningekuwa sina haja hii leo ya kusimama na kuchangia hapa kwa sababu ilikuwa ni sehemu ya wajumbe wa Kamani na mimi naungana na kamati katika kujadili mswada huu.

Lakini kwa sababu tu ni suala la kihistoria nimeona na mimi leo nisimame kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali na mimi niwe mtu wa kwanza katika kambi yangu ya upinzani kuweza kuchangia kwa jengo hili jipya.

Mhe. Spika, nianzae basi kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano na Sheikh Ali Yussuf pamoja na jumuiya yake kwa uwezekano wa kupatikana jengo hili jipya na la kisasa ambalo ni jema katika kudumisha demokrasia katika nchi yetu, lakini shukurani nyingi zaidi ziende kwako wewe Mhe. Spika, pia kwa makatibu wetu yule aliyestaafu na huyu aliyekuwepo pamoja na jopo zima la wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wamefanikisha leo hii sisi kuwepo hapa kuweza kutekeleza shughuli zetu, moja ni hii ya leo ambayo ni muhimu sana kuhusu marekebisha ya kumi ya katiba.

Mhe. Spika, naomba na mimi nianza kwa kushukuru Tume ya watu sita ambayo imeongozwa na naomba nimpandishe cheo kaka yangu Mhe. Ali Mzee kwamba anahitaji kupewa cheo cha Professor, wengi wetu ambao tulikuwa tukiiangalie hiyo kamati na mimi nitapenda kuwashukuru wajumbe wote na singependa kumtaja mjumbe mmoja mmoja kwa kuwa tunaielewa ni kamati ambayo imetokana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia niwashukuru maseketeri wake na wasaidizi wake ambao walikuwa wakifuatana na kamati hiyo wakati wote kwa kuweza kuona kwamba inatekeleza kazi zake.

Kwa kweli kamati imefanya kazi nzuri na kutoa uelewa kwa jamii, Mhe. Spika, wote hatuna uelewa wa aina moja unaweza ukatupeleka shule watu watatu na sote tukafundishwa tusome tu moja mbili tatu, lakini baada ya sasa moja ukasema turejee yale yaliyofundishwa mwanafunzi mmoja anaweza kueleza moja mbili tatu na mwengine anaweza kusema moja tatu mbili na mwengine hataweza kuileta hata moja. Hivyo ndivyo ambavyo Mwenyezi Mungu ametuumba katika uelewa wetu kwa wanadamu wako ambao rahisi sana kuelewa, wako ambao ukiwaelevesha watachukua muda wa kuelewa na wako ambao watachukua muda sana pengine mpaka baada ya kufanyiwa mtihani wa mara ya pili ndio watasema alaa kumbe ni moja, mbili na tatu.

Kwa hivyo kamati hii iliweza wale wa sehemu ya pili kuwaeleweza na wakaelewa kwa maana hiyo kuweza kuleta ufanisi katika kura ya maoni ambayo ilifanyika katika nchi yetu na lilikuwa jambo la historia kwa mara ya kwanza na tukafikia 66.4% naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wote ambao walishiriki katika kupiga kura za maoni mimi nilikuwa muangalizi wa uchaguzi katika eneo la kati, nilikuwa nashuhudia kwamba zoezi hilo lilikuwa la huru na la haki na halikuwa na matatizo yoyote napenda kwa namna pekee niwashukuru tume ya uchaguzi na tuwaambie kwamba vile ndivyo chaguzi zinavyotakiwa. Walijipanga vizuri, vifaa vyote vilifika kwa wakati na *process* nzima ya uchaguzi ilikuwa nzuri ni mategemeo yetu basi kwamba sasa tume ya uchaguzi itakuwa na zile chaguzi ambazo tumeziona ili wananchi waridhike na sio fujo na tafrani ambazo zinakuwa zikitawala hapo nyuma.

Mhe. Spika, nitoe shukurani za pekee kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ambao kwa sasa mimi ndio ninawawakilisha hapa kwamba wao walikuwa waelewa na wengi waliokuwa walielewa mara moja tuliwapata katika jimbo la Mji Mkongwe, kama kawaida Mhe. Spika wale wa mjini ndio mjini na wengine wanasema ndio chuo kikuu. Katika suala hili la kura za maoni wananchi wa mji mkongwe kwa asilimia 88.5 walisema ndio kwa maana ya kukubali mfumo huu na 11.5 nao walisema hapana lakini 1.5 ndio kura ambazo zimeharibika.

Kwa hivyo napenda niwapongeze sana na ni imani yangu kwamba wale wachache ambao nao tunaheshimu mawazo yao waliosema hapana ni kwamba watachukua muda kufahamu kidogo kadri tunavyokwenda na kunazisha huo mchakato wenyewe wa serikali ya umoja wa kitaifa kwa kweli

wataunga mkono mia juu ya mia kuungana na wenzao ambao wamekubaliana na mfumo huu, baada ya kuona faida ya mfumo huu hiyo ndio imani yangu.

Mhe. Spika, katika mswada huu kama nilivyosema sina mengi isipokuwa kuna maeneo mawili ambayo ningependa niyazungumzie, katika kifungu cha 41 ambacho kinafanya marekebisha katika kifungu cha 66 ambacho pia kwa pamoja baadae nitazungumzia kifungu cha 42. Au nianze na cha 42 ili iweze kupatikana ile mada yenyewe.

Kifungu cha 42 hapa niipongeze sana serikali kwa kuweza kuthamini yale matamko na matoleo na mambo ambayo yanasemwa sana sasa hivi duniani kuhusu kuwasogeza wanawake mbele katika vyombo vya maamuzi na vyombo vya kutunga sheria, kutoka asilimia thalathini na kwenda arubaini ni hatua nzuri na imani yangu kwamba serikali itaendelea kutafakati na hatimae kuona inafikia asilimia hamsini. Niwapongeze pia wanawake ambao wamejitokeza kwenye majimbo na imani yangu kwamba wengi watarudi kwa hivyo asilimia ya wanawake ndani ya Baraza lijalo bila ya shaka itakuwa kubwa zaidi ya asilimia arubaini.

Lakini nasema serikali ingeliona hiki kufungu cha 66 ambacho kuna nafasi za uteuzi naomba mhe. Spika, hapa kunukuu.

“Kifungu 66 kinasema kwamba kutakuwa na wajumbe kumi wa kuteuliwa na Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoelezwa katika kifungu cha 68 cha katiba ambao wakiteuliwa watafaa kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, isipokuwa kwa wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au kwa kushauriana na vyama vya siasa vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi iwapo hakuna kiongozi wa upinzani”.

Mhe. Spika, mimi ningeiomba sana hapa serikali kwa nia ile ile ya kuweza kuwaona wanawake basi napo rais akawekewa hapa katika nafasi hizi kumi angalau mbili basi wawe ni wawakilishi wanawake ili idadi ya kufikia asilimia hamsini iweze kukaribia, mimi ningeliomba sana hili serikali ilitafakari kwa nia ile ile ya kuheshimu mikataba ya kimataifa na kuona kwamba wanawake nao wanazingatiwa. Tunajua kwamba ni fursa ya Rais lakini iwekewe kipengele kwamba basi angalau wawili au anaweza kuteua zaidi ya wawili wawe ni wanawake.

Mhe. Spika, katika mswada huu mimi nitakuwa sina la ziada zaidi ya hilo isipokuwa sasa nilizungumze moja tu la jumla kwamba niwaombe Wazanzibari wakae tayari, wajipange na uchaguzi ujao *inshaalla* Mwenyezi Mungu ajaalie wende kwa amani kabisa kama tunavyotegemea na wawe tayari kuona mchakato mzima wa uanzishwaji wa serikali ya umoja wa kitaifa na wawe tayari kutoa mchango wao na kuipa serikali hiyo ushirikiano wa kutosha ili yale malengo yaliyofikia ya kupata maendeleo ndani ya Zanzibar yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naomba nikushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote na mimi nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezeshwa siku ya leo ambayo ni siku ya kihistoria katika nchi yetu hii ya Zanzibar, lakini pia nichukue nafasi hii nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa mambo yote ambayo umeyaendesha kwa kipindi chote umeendesha kwa umakini zaidi na hasa wewe mwenyewe ukiwa ni mwanasheria.

Mhe. Spika, lakini nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza wajumbe wa Baraza hili tukufu wote waliomo humu leo jinsi walivyoendelea na mchakato huu na leo tukafikia katika maridhiano haya, sasa niseme tu mwiba utokeako ndiko uchomako na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nilisema hili jengo nitalikosa hivi hivi lakini kwa rehema zake mwenyewe Subhanah wataala ameteremsha rehema kwamba mwimba utokeako ndiko uchomako leo na mimi

nimo katika jengo hili jipya kwa maslahi kubwa sana ya nchi hii kwa kupitisha maamuzi yetu ambayo ni maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar pamoja na Tanzania nzima.

Mhe. Spika, Ndugu yangu msemaji wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali baadhi ya mambo amenifilisi mengi sana lakini na mimi nitazungumza japo mawili matatu, kwa kweli Mwenyezi Mungu alitaka kutuonyesha baadhi ya mambo kwamba yeye ndie mwenyewe na sisi tukawa tulijisahau kama tumepewa dhamana na wananchi wa nchi hii kulinda, kutetea maslahi ya wananchi. Lakini Mungu akasema narudisha kwa sababu nyinyi ni baba mmoja mama mmoja si vyema mkaa pamoja mtoto wa shangazi na mjomba mkasukumiana mambo ambayo hayaleti maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nilipoingia tu juzi kuapishwa mkwe wangu Mhe. Haji Faki Shaali ananambia mama mkwe umekuja wakati mbaya hakuna tena malumbano, nikamwambia huu ni wakati mzuri kwa sababu ni wakati wa kukaa pamoja kujenga maslahi ya wananchi ya wananchi na kuijenga nchi. Kwa sababu unaelewa tulivyokuwa huko nyuma mimi na mkwe wangu na ndugu yangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary hapo nipe nikupe, lakini kutokana na mambo ambayo yalikuwa hayajafika wakati wake kwa mwenyezi Mungu leo ameyafikisha.

Mhe. Spika, na mimi niipongeze sana ile kamati ya watu sita kwa kweli kamati ile imefanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba serikali ya umoja wa kitaifa inapatikana Zanzibar hii, lakini nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kamati hii ingelilumbana kidogo ikasuguana basi haya mambo yasingekuwa, lakini ilikubaliana kwa pamoja kwa dhamira ya kuhakikisha katika nchi hii tunaingia katika usalama wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hakuna kitu kizuri kama uzalendo haya yote walikaa wenzetu na sisi tukakaa tukatafakari kwamba nchi hii ina wenyewe na sisi ndio wazalendo wa nchi hii hatokei mwengine, mimi nisema tujipongeze sote kwa jumla. Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi CUF na nimpongeze sana tena kwa mara ya pili Rais wangu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nimpongeze na mwanangu Seif Sharif mimi ni mwanangu kiuzawa kaburi lake hili kaburi langu hili haya ni mambo ya kupita ya kamari. Lakini nipongeze sana viongozi wawili hawa na niwapongeze sana wafuasi wao ambao waliwapa maelekezo jamani fanyeni hivi wakati umekwisha wa malumbano.

Mhe. Spika, niseme kwamba tunakubali sote Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mambo mengi sana, ombi kwa wajumbe wako tukufu wa Baraza hili la Wawakilishi ni kazi yetu kuyaenzi maendeleo ambayo yamefikwa hapa tulipo na itakuwa ni kazi yetu tukiingia katika kikao hiki kuhakikisha maendeleo yale tunayaenzi na Rais ambae atakuja wa chama tawala hapa kuhakikisha tunamsaidia kwa nguvu zetu zote kuyaendeleza na kuchangia kwa pamoja kuhakikisha tunaengeza maendeleo zaidi ya nchi hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza na kijana wetu Mhe. Mansour Yussuf Himid ni kijana ambae naweza kusema katika vijana wetu ni mmoja ambae anajitahidi sana katika shughuli zake, anaelewa katika utendaji wake kama mimi ni waziri ambae nimekabidhiwa dhamana tena dhamana aliyokabidhiwa ni muhimu katika nchi. Kama hakuna maji katika nchi hii binaadamu hawezi kuishi kama hatukupata umeme nchi hii maendeleo hayawezekani, lakini pia amejitahidi sana katika kufanikisha mambo mbali mbali, kwa hivyo nimtakie kila la kheri Baraza hili ambalo ni la kihistoria leo na niwape pole wale wenzetu ambao hawakurudi kwenye mchakato lakini ndio tunasema anaetoa ni mungu, vile vile niwape pongezi za dhati wale wote ambao wamerudi ili tushirikiane pamoja na wale waliokuwa hawakurudi kushirikiana pamoja katika kujenga nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi nichukue nafasi hii niunge mkono hoja hii ya serikali ya umoja wa kitaifa, na niwapongeze sana wananchi walijua namna walivyoamua kwamba sasa nchi hii tunatakiwa iwe katika hali ya amani na utulivu. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, Mungu atupe kila la kheri na atupe imani ya kuiongoza nchi hii kwa umoja wetu na uzalendo wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, na mimi kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na kuendeleza shughuli zetu hizi. Lakini pili naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Spika, mbele yetu ni Mswada wa Kurekebisha Katiba. Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na Katiba siku zote tunasema kwamba ni mwanga na ni tochi ya nchi ambayo inahusiana nayo. Sasa tochi hiyo ikiwa na mwanga mzuri naamini nchi hiyo itakuwa na maendeleo mazuri.

Sasa katika marekebisho haya kuna mambo mawili makubwa. Kwanza kuna suala la Azimio la Baraza ambalo tulilipitisha katika kikao kilichopita kuhusiana na suala la Kura ya Maoni. Lakini la pili kuna suala la kuboresha Katiba katika vipengele vyengine.

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba kwa mujibu wa Azimio la Baraza ambalo tulilipitisha katika kikao kilichopita, nafurahi kusema kwamba maazimio yote yale tuliyoyapitisha katika azimio lile au vifungu vyote vile vimezingatiwa vizuri na ipasavyo katika Katiba hii. Kwa hivyo, kwa upande huo mimi na wenzangu katika kambi yetu hatuna tatizo nalo na tunasema kwamba tunaunga mkono hoja hii.

Lakini la pili kuna sehemu ambayo inaboresha Katiba katika vifungu vyengine. Kwa kweli vifungu hivi vinavyoboresha Katiba navyo ni vizuri na vimezidi kuiweka Katiba yetu katika hali nzuri na yenye maslahi kwa watu wetu.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika, Katiba yetu nathubutu kusema sasa yakipita marekebisho haya itakuwa ni miongoni mwa Katiba nzuri sana katika ulimwengu. Kwa hiyo, itakuwa wawakilishi wetu wamefanya kazi nzuri sana kwa kuiondoa Katiba yetu hapo ilipokuwa na kuipeleka katika kiwango cha juu cha miongoni mwa Katiba nzuri za ulimwengu.

Mhe. Spika, Katiba hii sasa inaondoa mfarakano ambao ulikuwepo mara moja moja na inajenga Umoja wa Kitaifa. Umoja wa Kitaifa katika nchi yetu unaleta utulivu ambao naamini utazalisha maendeleo zaidi katika nchi yetu. Kwa maana hiyo, Katiba hii itakuwa ni Katiba nzuri ambayo ina lengo la kuendeleza nchi yetu kiuchumi na kidemokrasia.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika, naamini hata ile amri ya Mwenyezi Mungu Katiba hii imeizingatia vizuri kwamba tushikamanane sote kwa pamoja ili nae Mwenyezi Mungu aweze kuleta baraka zake zaidi katika maslahi yetu na maslahi ya nchi.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika, mimi nimesimama hapa kusema kwamba tunaunga mkono marekebisho ya Katiba hii na tunaunga mkono hiyo kwa maslahi ya nchi yetu, kwa maslahi ya umoja wetu na kwa maslahi ya vizazi vyetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia mimi binafsi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Mgogoni.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia machache sana katika mswada huu. Kabla ya kwenda ndani zaidi nami naomba niwashukuru na niwapongeze wote ambao kwa njia moja au nyengine wametufikisha hapa tulipo leo. Lakini pongezi zaidi zinastahiki kwa wananchi wa Zanzibar ambao la si kwa maamuzi yao ya kukubali kura ya maoni kitendo ambacho tunakifanya leo kisingewezekana. Sasa kwa sababu wananchi wa Zanzibar kwa umoja wao waliamua kutupa kazi hii mimi binafsi nawapongeza sana.

Lakini pia Mhe. Spika, naomba niwapongeze viongozi wetu wakuu Mhe. Rais Dk. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Shariff Hamad kwamba ile ndoto yao waliyokuwa nayo kwa kweli leo Baraza letu tukufu linaikamilisha. Namuomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na umri zaidi ili waweze kuwatumikia wananchi wa Zanzibar popote walipo na katika hali yoyote ile.

Mhe. Spika, bahati nzuri tumepewa karatasi moja muhimu leo hivi asubuhi, ni ile ambayo sheria namba 6 ya 1964. Nilipoisoma nimejua kumbe Mzee Abeid Amani Karume hii kazi alianza. Sheria

namba 6 ya 1964 ya tarehe 25 Februari, iliweka Sheria ya Katiba inayotambua kuwepo kwa usawa, maridhiano na umoja kwa watu wa Zanzibar.

Sasa hii kazi mzee wetu Mhe. Abeid Amani Karume alianza na bahati nzuri mwanawe Dk. Amani Abeid Karume leo tunamsaidia kuimaliza. Yeye Dk. Karume atakuwa amenawa, kazi iko kwetu sasa kuhakikisha kwamba yale ambayo yalitarajiwa tunayaendeleza.

Katika hili Mhe. Spika, naomba nikubaliane na wenzangu kwamba Rais Dk. Karume anahitaji kuenziwa kwa sababu amefanya kazi kubwa sana. Isingekuwa vizuri baada ya kazi yote hii ambayo mwaka mmoja uliopita hakuna ambaye angedhani tungeweza kufika hapa. Kwa kweli anastahiki heshima na kuenziwa sana.

Mhe. Spika, mimi katika hili naomba tuanze sisi wenyewe kwanza kutafuta utaratibu wa kumuenzi Dk. Amani Abeid Karume baada ya kustaafu. Lakini pia hilo halitoshi viongozi wa nchi ambao wamefanyia nchi zao kazi nzuri Jumuiya ya Kimataifa nao huwaenzi. Nakumbuka baada ya kumalizika ubaguzi wa rangi waliwatunuku kwa pamoja ile tuzo ya *noble prize* Mzee Nelson Mandela na Peter De Klerk heshima ile. Sasa na sisi si vibaya kuwaomba wale wanaotunuku *noble prize* watoe heshima hiyo kwa Dk. Karume na kwa Maalim Seif kwa kuifikisha Zanzibar hapa tulipo. (*Makofi*)

Lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Spika, mwaka jana kuna tunzo ya *More Ibrahim* inayotolewa kwa viongozi wa Afrika wanaofanyia kazi nchi zao, lakini bahati mbaya mwaka jana hakuna kiongozi ambaye ali-*qualify*. Kwa hivyo, haikutolewa kwa kiongozi yeyote mwaka jana.

Sasa mimi ningewaomba wale wote wanaotoa tunzo hii ya *More Ibrahim* kwa viongozi wa Afrika, nakumbuka Dk. Salim Ahmed Salim ni miongoni mwao, basi waone umuhimu wa viongozi wetu wa Zanzibar kupewa heshima hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilisema mapema kwamba kunaweza kukatokea usumbufu hapa na pale hasa katika viti. Nawaomba radhi sana nimeona kama viti viwili vitatu tayari vimeleta usumbufu huo na kiasi cha kumfanya Mhe. Nassor Ahmed Mazrui afanye kazi ya ufundi ndani ya chombo hichi hivi sasa. Nimeshaagiza tu kwamba mara tutakapoondoka pale saa nane basi mafundi waje ili wavirekebishe vile viti ambavyo vinaleta hitilafu ya hapa na pale, tutakaporudi jioni viwe katika hali nzuri zaidi. Naomba radhi sana kwa usumbufu huo unaojitokeza.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, kwa kweli mimi katika yale ambayo yalitokana na Azimio la Baraza letu na kwa namna ambavyo yameingizwa katika marekebisho haya na marekebisho yake yaliyotolewa na kamati, mimi sina zaidi isipokuwa ni kuwapongeza sana Serikali na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuona kwamba inatuletea kitu kizuri ambacho kitakuwa ni historia kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, ila kuna mambo mawili matatu naomba nizungumze katika yale mambo ambayo hayatokani na Azimio letu la Baraza. La kwanza ni suala la kifungu namba 3 ambacho kinazungumzia Zanzibar ni Nchi ambayo eneo na mipaka yake mpaka mwisho. Hilo ni jambo zuri na kwa kweli kama walivyosema wenzangu litaondoa utata.

Ila kuna sentensi mstari wa mwisho inayosema kwamba “Kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar”. Sasa hapa mimi naomba ufafanuzi kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mimi ninavyojua maana ya neno jamhuri ni nchi inayoongozwa na Rais. Sasa na Zanzibar ni nchi inayoongozwa na Rais. Kwa hiyo, sifahamu ni vipi kwamba Zanzibar zamani ikiitwa Jamhuri ya Watu za Zanzibar na leo isiitwe Jamhuri ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi nafikiri tunahitaji kitu kama hicho. Lazima tuwe hapa Zanzibar bado ni jamhuri kwa sababu inaongozwa na Rais na kwa sababu ni nchi ya Mapinduzi basi ni Jamhuri ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi nafikiri

Katiba ingeweka *specifically*, yaani tusijivunge vunge tukajitia katika matata yasiyo na msingi tukawapa watu nafasi ya kutudogosha.

Mhe. Spika, kuna nchi zinajifafanua nyengine zinajiita *Kingdom* ya nchi fulani au *Sultanate* ya nchi fulani, nyengine zinaweka mfano *Republic of Kenya*. Sasa sidhani kwamba tukiita *Zanzibar Revolution Republic* tutakuwa tunamvunjia mtu Katiba au vipi. Nafikiri tuwe wazi sana.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri hilo, Mhe. Waziri alifikirie na nadhani si vibaya kuliingiza katika Katiba yetu. Kwa sababu tumepata fursa ya kubadilisha Katiba na yeye mwenyewe ameweka hilo, kwa hivyo mimi bado namkumbusha kwamba Zanzibar ni Jamhuri na hata wimbo wetu wa Taifa leo asubuhi tulipoimba tuliimba kwamba sote tunasherehekea jamhuri kutuletea. Kwa hivyo, *Republic of Zanzibar* bado ni *sustainable*, ipo na lazima wenyewe tuiweke katika hali ile.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 89 (3) kinachozungumza Kinga za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vile kilivyokaa kinaonekana kama tunajaribu ku-*prune* zile kinga za Wajumbe wa Baraza. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri aniweke sawa kwa sababu jambo tunalolipitisha ni jambo kubwa na naomba tulipitisha ikiwezekana sote kama alivyosema sahibu yangu Mhe. Ame Mati Wadi mia kwa mia iwe mia kwa mia kweli.

Mhe. Spika, kifungu cha 118 kinachozungumza Kamisheni ya Utumishi ya Umma, sasa hapa kuna kitu chengine naomba ufafanuzi pia. Katika kifungu hichi Mhe. Waziri anazungumza “Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Tume ya Utumishi ndani ya Katiba zitakuwa na mamlaka yafuatayo: Kuajiri watu kushika nafasi za utumishi serikalini au kuthibitisha ajira zao za utumishi serikali. Kupendekeza mishahara na marupurupu ya watumishi wao serikalini”.

Mhe. Spika, kuna tume nyingi, kuna Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na tuna Tume ya Utumishi ya Mahakama. Sasa kuna mihimili mitatu ya dola ambayo ni Serikali (*Executive*), Baraza (*Legislature*) na Mahakama (*Judiciary*). Sasa nilikuwa napata tabu kwamba kuajiri watu wa kushika nafasi za utumishi serikalini ambao wako katika Baraza. Sasa hawa watu wanaofanya kazi Mahakamani au Barazani ni vipi utumishi wao uko serikalini. Hapa ndio kidogo napata tabu. Au ajira na utumishi wao serikalini napata tabu kuona kwamba watu wanafanya kazi Barazani au Mahakamani halafu wakawa utumishi wao unakuwa *link* na Serikali.

Kwa hivyo, hapa naomba ufafanuzi wa Mhe. Waziri anapozungumza Serikali na vipi utumishi wa nafasi nyengine za Mahakama ambao sio Serikali, au Baraza ambao sio Serikali, tume zao zitakuwa na mamlaka ya kuthibitisha au kupendekeza mishahara na marupurupu ya watumishi wao. Hilo ningemba ufafanuzi.

Lakini pia nilikuwa nataka kujua kutoka kwa Mhe. Waziri marekebisha haya ambayo yanahusiana na kuunda kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma yanarekebisha vipi matatizo makubwa yaliyonayo utumishi wa umma hivi sasa mfano *seniority* na mambo mengine. Hilo ni jambo ambalo ningemuomba Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia. Nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nami nichukue nafasi hii kukupongeza na kukushukuru kwa hatua nzuri tuliyofikia. Nikupongeze kwa ubunifu wako na jitihada zako na leo hii sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wa Zanzibar kwa jumla wanafaidi jengo letu jipya hili la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, hongera sana.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kufika hapa tukiwa wazima wa afya na siha. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ataendelea kutujaalia nchi yetu kheri, amani, masikilizano na mshikamano. Mhe. Spika, sina maneno mengi, maneno yangu ni machache tu nitawaachia wenzangu nafasi naamini wanaweza kuzungumza vizuri zaidi kushinda mimi.

Lakini kwanza nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa maana ya wana wa CCM kwa kuniamini na kunichagua upya kutetea kiti cha uwakilishi kupitia kwa Chama cha Mapinduzi kwenye Jimbo hili la Kiembesamaki. Niwakumbushe tu Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe kwamba hapa mlipo mko kwenye Jimbo la Kiembesamaki. Niwashukuru kwa namna walivyotukaribisha sote kwa ukarimu wao. Nataka niwahakikishie kwamba tutaendelea kuwa na msaada mkubwa sana kwa Baraza hili na Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi wa Zanzibar.

Lakini pia niwaombe wana wa CCM kwenye Jimbo hili la Kiembesamaki sasa kujipanda na kujiandaa vizuri ili Chama cha Mapinduzi kishinde kwenye Jimbo la Kiembesamaki. Lishinde kwa nafasi ya Urais, nafasi ya Ubunge, nafasi ya Uwakilishi na nafasi ya Udiwani. Nataka niwaombe Wazanzibari wote kwamba baada ya maamuzi haya muhimu waliyoyafanya yaliyotukuka ya muelekeo mpya wa nchi yetu katika siasa zake, niwaombe wakichague Chama cha Mapinduzi kwamba na mimi naamini haya tunayoyazungumza humu leo yanalenga kwenye mustakbali mpya na mwema zaidi wa nchi yetu yatakuwa salama zaidi mikononi mwa Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, wamchague Dk. Ali Moh'd Shein kuwa Rais wa nchi hii. Mhe. Spika, najua wenzangu wa chama cha CUF hawana matatizo na hilo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa ukienda zaidi kidogo ya hapo itakuwa kampeni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nimeshamaliza. Mhe. Spika, pili niishukuru sana Kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali. Mhe. Spika, kamati zote zilizofanya kazi nzuri katika historia ya nchi yetu huwa zinapewa jina la yule Mwenyekiti. Naamini kwa kazi nzuri aliyotufanyia Mhe. Ali Mzee sio kwa kamati hii tu, lakini kwa msaada wake mkubwa kwa Baraza hili kwa miaka kumi iliyopita. Basi mimi napendekeza kamati hii iitwe Kamati ya Mhe. Ali Mzee. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tuna Kamati ya Nyalali ambayo wewe ulikuwa Mjumbe pamoja na Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Tuna Kamati ya Shelukindo na tuna Kamati ya Kasanga na nyenginezo. Basi nafikiri kwa hili itakuwa muafaka turidhie kama maridhiano yetu yalivyo, kamati hii ipewe jina rasmi la Kamati ya Ali Mzee.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumza Sheria ya Rais namba 6 ya 1964. Sheria ya Katiba inayotambua kuwepo kwa usawa, maridhiano na umoja kwa watu wa Zanzibar. Sheria hii imeundwa baada ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Ninakuomba uniruhusu niinukuu kwa haraka haraka nieleze yangu machache nimalizie.

“Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Usawa, Maridhiano na Umoja ya Watu wa Zanzibar ya mwaka 1964. Madhumuni makuu ya Mapinduzi ya watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii au upendeleo wa kisheria na mapungufu yote yaliyopita yalikuwa yanawagawa wananchi na makundi mbali mbali ya raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini, uasilia wa mtu. Madhumuni hasa ya Mapinduzi ni kukuza usawa, maridhiano na umoja kwa watu wa Zanzibar.

Kwa msingi huo, kila raia wa Zanzibar anatangazwa kuwa ana haki sawa, fursa na hifadhi ya uraia wake kama vile ambavyo anatekeleza majukumu na wajibu wake wa uraia. Hakuna haki, fursa au hifadhi inayoweza kufutwa kisheria kwa raia yeyote kwa kutumia vyombo vya dola au kwa kutumia hatua za mtu binafsi kwa sababu ya misingi au kisingizio cha ukabila, dini, jinsia, uasilia wa raia huyo.

Hakuna kifungu chochote ndani ya sheria hii kitakachozuia serikali kutunga sheria itakayotoa nafuu maalum au upendeleo wa kiuchumi, kitamaduni au kijamii kwa raia waliokosa haki za msingi kwa madhumuni ya kuwaletea usawa kama raia wengine.”

Mhe. Spika, haya tumekuwa tukiyazungumza kwa siku nyingi sana. Madhumuni makuu ya Mapinduzi ni kuwaunganisha watu wa Zanzibar, kuhakikisha usawa, haki, utu na heshima ya watu

wote wa Zanzibar inalindwa, si vyengine vyovyote vile. Wale ambao walikuwa wanadhania Mapinduzi maana yake vurugu, mabavu sio kweli, haikupata kuwa hivyo na si misingi ya Mapinduzi hiyo.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri sana miongoni mwa walioweka saina sheria ile Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi mmoja marehemu baba yangu mimi Yussuf Himid ambaye ndie alikuwa Mkuu wa Jeshi la mwanzo, Jeshi la Ukombozi.

Kwa bahati nzuri zaidi mjumbe mwengine yule pale yupo Mzee Hassan Nassor Moyo naomba tumtambue. Hawa ndio waasisi na ninajua amekuwa makusudi kwa sababu misingi ile ile iliyowatuma kupindua nchi hii bado inamkereketa, inamuuma na amekuwa kushuhudia misingi ile sasa ikiwasilishwa. Kwa sababu yale ndio yaliyokuwa malengo yao, sio mtafaruku, sio utengano, wala sio mazingira ya Wazanzibari kutafautiana kwa mambo yasiyokuwa na maana. Ndio maana Mzee Moyo yupo kwa niaba ya wenzake. Wengi wametangulia mbele ya haki wamebaki wachache sana. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na maisha marefu washuhudie Zanzibar iliyo mpya kama walivyolenga.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Maalim Seif Shariff Hamad na yeye kwa ujasiri wake wa kukubali kufanya maamuzi magumu ambayo yameifikisha nchi yetu hii sasa kwenye hatua ya kuelekea kwenye kheri kubwa zaidi.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Rais wetu Mhe. Amani Abeid Karume, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ujasiri wake juu ya mazingira magumu lakini alikubali kufanya lile lililofaa kufanywa. Juu ya kwamba kipindi fulani palikuwa na switafahamu, mengine ya kupandikizwa, lakini walikuwa tayari viongozi wetu hawa kufanya maamuzi yaliyokuwa sawa kwa niaba yetu sote. Hatimaye wananchi wa Zanzibar kufanya maamuzi yaliyotukuka tena kwa kura zilizokuwa nyingi kutuelekeza kwenye umoja, amani na mshikamano. Bila ya amani, umoja na mshikamano hakuna nchi yoyote inayoweza kustawi wala kuwepo.

Mhe. Spika, sina maelezo ya kupitia kwenye vifungu kwa maana mimi ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi huko ndio yalikoasisiwa hayo. Kwa hivyo, labda nimalizie tu kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa maamuzi ya kura za ndio. Jimbo la Kiembesamaki limechagua ndio. Nina washukuru, ninawapongeza na ninarudia kuwaambia, kama nilivyokuwa nikiwaambia kwamba hawatojutia maamuzi hayo na maamuzi hayo ndio sahihi kwa mustakabali mwema wa nchi yetu sisi.

Mhe. Spika, ninakushukuru na ninakupongeza sana kwa mara ya pili kwa kazi hii nzuri na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, naomba radhi kidogo sauti yangu imeganda, lakini nadhani watu watanielewa. Kwa mara ya kwanza tangu kuingia Baraza hili, naomba kuunga mkono hoja kabla sijachangia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Mama yangu Mhe. Bi Ashura alikuwa akisema sijui mara mia tatu, sijui kama yumo.

Baada ya kusema hivyo Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimekuwa sehemu ya kuleta mabadiliko haya ambayo tunataka kufanya maamuzi na yale yaliyokwisha kufanywa na wananchi, ni masuala ya msingi katika kuendeleza umoja wetu kama Wazanzibari. Katika kujua kuwa kwenye kuendesha maisha kuna matatizo na matatizo yanastahiki kuamuliwa.

Mhe. Spika, nilitaka Mhe. Mansour Himid kanyinyang'anya. Nilitaka na mimi kunukuu hii sheria, nilikuwa nayo kopi kabla na ninakumbuka katika kuwahamasisha wananchi kuna mahala fulani niliisoma hii. Lakini Mhe. Mansour ameisoma na wananchi wameisikia. Mimi nilitaka tu kuisitiza na kumuunga mkono Mhe. Mansour Yussuf Himid kwamba hii aliyosoma ambayo mimi ninayo na wengine wanayo, kuna watu hawajawahi kuisikia, wala hawajui na wala hawafahamu kwamba kumbe misingi wa Mapinduzi ni huu. Waliukuta mchezo unachezwa na wao wakademka, wakaona ile ngoma inayochezwa ndio ndio, kumbe zile chapuo zilikuwa sizo, walikuwa watafute goma kubwa

linapiga vipi. Mwenyezi Mungu ametusaidia, Mhe. Mansour Yussuf tunakushukuru kwa kufanya nukuu hiyo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi naunga mkono tu. Waheshimiwa Wajumbe hapa wanapongeza, na mimi nawajibu kupongeza. Mimi namshukuru sana Mhe. Amani Karume, nadhani mambo mengine ukiyazungumza sio vibaya. Mhe. Amani Karume karibuni alikuwa na harusi ya mtoto wake, akasema hakikisheni kadi hii munamfikishia nyumbani kwake Mhe. Juma Duni, *technology* hiyo.

Mhe. Spika: Mhe. Abubakar Khamis Bakary namuomba radhi kwa yaliyotokea. Mhe. Juma Duni endelea.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, wakati tunapeana mikono ya kumpongeza, akanitambulisha kwa mkwewe, muonzi mwenziwe, akamwambia huyu ndiye Sheikh Juma Duni Haji, huyu ni rafiki yangu sana bwana, lakini yupo upinzani na tunafanyakazi pamoja vizuri sana, Sheikh Juma nakushukuru kwa kuja harusini.

Ni kwamba Mhe. Amani Karume anafahamu kuwa mimi na yeye tunatofautiana kwa mawazo, lakini la msingi anafahamu kuwa sisi ni wamoja na ni marafiki kwa sababu sote ni Wazanzibari. Kwa hivyo, muda wote tulipokuwa tukifanya majadiliano tulikuwa tukipingana, lakini dhamira kubwa ilikuwa ni kujenga umoja. Ilikuwa tufahamu kwamba jamani tunahitaji umoja wetu kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mapinduzi yavyotokea mimi sikushiriki kwa bunduki lakini niliyaona, nilikuwa mjini na nikahama usiku huo huo mwitu kwa mwitu mpaka kijijini kwangu. Wakati huo nilikuwa nimemaliza darasa la saba na baba yangu akaniambia sasa ujitayarishe twenzetu tukavuwe, maana ndio kazi yake. nikamuuliza kwa nini, akaniambia mimi sina pesa ya kukulipia wewe usome zaidi ya hapo ulipofika. Kutokana na Mapinduzi yale, matokeo ya mthani wa darasa la saba au siku zile darasa la nane, mimi nilipata kuingai kutoka darasa la saba na mimi nikatangazwa kwamba nimekwenda sekondari.

Ninaamini kabisa kama sio mabadiliko ya Mapinduzi yale, basi siajabu sasa nimeshatoka kibiongo, aidha kwa kubeba magunia au kwa kulima na kumbe nilikuwa na akili nzuri ya kuweza kushiriki katika maisha ya kujenga nchi yangu. Ninachoamini mimi kwamba na hivyo vizazi vilivyo nyuma basi vinahitaji fursa kama niliyoipata mimi.

Mhe. Moyo yupo alifanya hayo waliyofanya ndio maana sisi tuko hapa. Tutakayofanya sisi ndio yatakayowafaa hao wanaokuja. Kwa hivyo, kwanza naipongeza kamati ya Mhe. Ali Mzee rafiki yangu sana. Lakini katika kupongeza hapa watu wamesahau jambo moja, naomba nisaidie. Hapa Barazani pamepita viongozi wengi, pamoja na wawakilishi wengi. Lakini nataka kukumbushia tu kwamba Mhe. Ramadhan Haji bado yuhai alikuwa Waziri Kiongozi wa kwanza, akafuatia na Mhe. Maalim Seif Sharif, akafuatia Mhe. Dk. Omar Ali Juma Mwenyezi Mungu amrehemu, akafuatia Dk. Moh'd Gharib Bilal na hivi sasa naona swahib yangu katoka Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.

Sasa mimi nilitaka kutoa pongezi kwa Mhe. Shamsi na wewe Mhe. Spika. Mswada wa Mhe. Abubakar Khamis ulipokuja, kama wawili nyinyi mlisema hapana, basi siajabu mngekwama. Sasa nyinyi kama viongozi wa Baraza hili na yeye kama Waziri Kiongozi, anaingia katika kumbukumbu kwamba wakati wake akiwa Waziri Kiongozi, basi mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa nchi hii kikatiba yametokea. Kwa hivyo, naomba tumpongeze kwa moyo wa dhati kabisa Mhe. Shamsi na tukupongeze wewe wakati ukiwa ndio Spika, wa Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba pia niwapongeze viongozi wetu waliosababisha hili kutokea. Mwanzo ilionekana hoja hii ni ya Maalim Seif Sharif na Mhe. Aman Abeid Karume, lakini leo tunafahari kwamba sote ni sehemu ya mabadiliko. Katika dunia Mhe. Spika, ni lazima tuseme kwamba mawazo yoyote hayawazwi na watu mia. Mawazo yanaanza na mtu mmoja au wawili na kwa nadharia ya uongozi *management*, ukipata asilimia 20 basi wale wengine hufuata. Nashukuru kwamba hili limetokea.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nashukuru tena kwa kunipa ruhusa. Vile vile naomba nivishukuru Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF kwa mashirikiano ya pamoja na kuwawezesha Wazanzibari wasiopungua asilimia 66.4 kusema katiba ibadilike. Naomba kukushukuru Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia machache katika mswada huu. Mhe. Spika, mswada huu hautaki kuchangiwa sana kwa sababu maana na madhumuni yake sote tunaelewa na sote tunayakubali.

Mhe. Spika, kwanza nianze katika haya machache kwa kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo langu la Chambani. Nawapongeza sana kwa imani na kuniunga mkono kwa miaka 15 tokea kuanza kwa mfumo huu wa vyama vingi nikiwa kama mwakilishi wao.

Mhe. Spika, mwaka huu walinipunguzia kura na hawakunikataa kabisa. Waliniambia tu kwamba kura zako mara hii hazitoshi kwa kazi hii ya kuliwakilisha jimbo. Mhe. Spika, haya ni maamuzi ya kidemokrasia, ni lazima niyaheshimu. Natoa wito kwao, kwa sababu ya kuona kuwa kazi hii ni ngumu kwangu mimi, ni nzito basi yeyote ambaye wataona naweza kuwafaa kushirikiana nao Mhe. Spika, niko tayari kwa mashirikiano.

Mhe. Spika, katika pongezi nawapongeza sana viongozi wetu wawili ambao wamekwisha pongezwa sana, Mhe. Dk. Aman Karume na Mhe. Maalim Seif Sharif kwa kutufikisha hapa leo, tunatoka mbali na hatuna haja ya kumbukumbu.

Mhe. Spika, lakini tunapaswa tujipongeze wenyewe haidhuru mtu huwa hajiiti mwenyewe bwana. Kama Mhe. Spika, sisi wawakilishi tusinge geuka tukasahau ya nyuma basi pamoja na dhamira nzuri zilizokuwepo kwa viongozi wetu kwa kweli tusingefikia pahala hapa leo. Naamini wako ambao wataingia humu na kuliendeleza hili, lakini wananchi watawakumbuka hata wale ambao hawakubahatika kuendelea tena kwa kazi nzuri ambayo wamechangia katika kuliweka sawa suala hili ambalo leo tunalijadili hapa.

Sasa Mhe. Spika, ni nini matarajio ya watu katika yote haya ambayo tunayafanya. Kwa upande wa siasa wananchi wanatarajia sana kuimarika kwa demokrasia kupitia chaguzi zetu, lakini wanatarajia vile vile kuimarika kwa utawala wa sheria na kuimarika kwa utawala bora. Kwa upande wa kijamii Mhe. Spika, wananchi wanatarajia kwamba mabadiliko haya yataweza kuigeuza jamii yetu ambayo hapo awali ilikuwa inashirikiana kama ndugu, lakini siasa chafu kidogo ilileta dosari na mashirikiano ya kijamii nayo yakatetereka. Lakini Mhe. Spika, kiuchumi wananchi wanatarajia kuimarika kwa uchumi wao. Serikali inayokuja ambayo leo tunajadili hapa na kuipanga ni lazima ihakikishe kwamba matazamia haya ya wananchi yanakamilishwa kwa hali yoyote, iwapo haya Mhe. Spika, hayatofikiwa basi mabadiliko haya yatapoteza maana na mwelekeo wake kwa muda mfupi sana baada ya kuanzishwa.

Sasa Mhe. Spika, ni nini hasa lifanyike katika kufikia matazamia haya. Ni mambo mengi Mhe. Spika, lakini kwa mnasaba wa sheria hii ambayo tunaitunga leo hapa ya kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa. Ni matazamia yetu ya kwamba serikali itakayoundwa haitokuwa ya umoja wa kitaifa tu, lakini itakuwa ni serikali makini na yenye uwezo wa kutekeleza majukumu ili kufikia majukumu haya ambayo wananchi wanayategemea. Katika hayo Mhe. Spika, najua Rais ana uwezo kikatiba wa kuiunda serikali hiyo na kuunda wizara hizo na ana uwezo na anao washauri wa kufikia hapo. Lakini mambo machache ambayo kama mchango wangu katika suala hili ni muundo wa serikali ambayo itazingatia mambo matatu. Kwanza tumekubali na leo tumethibitisha katika katiba kwamba Zanzibar ni nchi. Mhe. Spika, kwa sababu Zanzibar ni nchi na leo tumethibitisha, mashirikiano ya nchi hii na nchi za nje katika mambo ambayo hayaathiri Muungano wetu ni lazima yaimarishwe ili kuipa nguvu serikali inayokuja uwezo wa kutumia rasilimali zake katika kuinua uchumi wetu. Hilo ni jambo la kwanza.

Kwa hivyo, narudia jambo ambalo nimekuwa nikilizungumza kwamba iwapo ndani ya wizara hizo ambazo kwa zile Rais ataziunda haiathiri masharti ya katiba ya Jamhuri ya Muungano. Suala la mashirikiano yetu na nchi za nje zionyeshwe wazi wazi ndani ya Muungano.

Jambo jengine ambalo vile vile sambamba na hili tumekuwa tukilizungumza na mimi napongeza sana kauli ya Mhe. Ali Suleiman ya namna ambayo Rais ameitumia nafasi hii ya Wizara ya Fedha, ingawa sio jambo la lazima kwamba Rais aitumie nafasi ya Wizara ya Fedha. Kwa misingi hiyo hiyo basi Makamo wa Rais wa kwanza na Makamo wa Pili wa Rais ambao kwa kawaida wanazo wizara, maana yake zimo wizara chini ya afisi hizo kubwa, lazima zitafutwe wizara ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha sio tu ushirikiano wa viongozi hawa wakubwa, lakini kwa umuhimu wa kuangaliwa wizara hizo ili ziweze kuwa na ufanisi wa kutosha.

Mhe. Spika, sambamba na hili nimeona marekebisho ya kifungu ambacho kimetaja vikosi vya serikali, kwa nia njema sana Mhe. Spika, wakati tunaunda au tunajaribu kusaidia muundo wa serikali inayokuja, serikali za mitaa ziwe huru na zisichanganywe kabisa katika vikosi hivi vya idara ya serikali. Mhe. Spika, hili litaweza kuziimarisha serikali hizi na zitachangia katika uchumi. Kwa sasa hivi mfumo uliopo wa kuzichanganya serikali za mitaa na vikosi vya SMZ au wizara nyengine yoyote, sio jambo la busara.

Mhe. Spika, linapata umuhimu zaidi suala hili sasa hivi, hasa kwa vile Wakuu wa Mikoa wamepunguziwa majukumu ya kungia katika Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo Wakuu wa Mikoa wanahitaji kuwa huru zaidi na kushughulikia suala la serikali za mitaa. Isije ikawa Mkuu wa Mkoa yupo leo ametolewa katika shughuli hizi, lakini Mkuu wa Mkoa aende akapige saluti kwa waziri ambaye anashughulikia vikosi vya serikali. Nadhani hili Mhe. Spika, likifanyika tutakuwa na serikali za mitaa ambazo ni muhimu sana kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi lakini kwa kuongeza pato la uchumi wetu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema vifungu vingi ambavyo vimetajwa katika sheria hizi, vimefanyiwa kazi nzuri sana na hatuendi kifungu kwa kifungu kwa makusudi leo kwa sababu mengi ya mambo haya tunaamini kwamba yameandikwa vizuri na ni imani yetu kwamba watakao husika na utekelezaji watatumia busara na uwezo wao ili kuhakikisha kwamba haya ambayo leo tunayazungumza hapa na kuyatungia sheria yatafanyakazi ili lile lililokusudiwa katika muundo mpya liweze kuleta maana katika maendeleo yetu.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, ni suala la *check and balance* ya Baraza letu, *check and balance* ya mihimili yetu ya dola. Tunayoizungumzia hapa ni serikali zaidi, lakini kadiri inavyozungumziwa serikali, vimo vifungu moja kwa moja vinavyogusa mahakama na vinavyogusa Baraza la Wawakilishi. Ndio maana hapa katika ile itifaki Spika, anafika pahala mpaka ikiwa kuna mambo yatatokezea basi anaweza akashika nafasi japo kwa muda ya Urais. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Uspika una umuhimu wake na ninachokusudia kukisema hapa Uspika lazima utiliwe nguvu kwa sababu ya umuhimu wake.

Kwa hivyo, limekuwa likizungumzwa jambo ambalo hapa naona ni *official* zaidi serikali itusikie ya kwamba sasa tuna haja ya kuuimarisha Unaibu Spika, sambamba na kuanzishwa kwa Unaibu Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, haya ni muhimu sana kwa sababu, Naibu Spika, atakayeimarishwa atamsaidia Spika, lakini kwa sababu Spika, ni binadamu patakapotokezea aina yoyote ya matatizo, basi watu hawatafuti waende wapi tayari wamekwisha jiwekea njia ya kupita.

Vile vile Naibu Mwanasheria Mkuu hata kama hatuingia wala sio lazima kwamba aingie katika Baraza la Wawakilishi, lakini ni matayarisho makubwa ya iwapo Mwanasheria Mkuu na kwa sababu anaingia moja kwa moja katika Baraza, basi mambo yoyote yatakayomtokezea kwa kuingia kwenye Baraza basi isiwe tena Baraza letu linatafuta nani aje hapa kuja kutoa ufafanuzi wa mambo ya kisheria.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho kinachokuja kitakuwa ni kipindi ambacho Baraza letu litahitaji zaidi huduma ya mambo ya kisheria kuliko wakati wote ambao umepita. Kwa hivyo, kama huna Mwanasheria ambaye wakati wowote yuko *sober* na mwenye uwezo na msaidizi wa kumsaidia shughuli zake, kwa kweli tutaipa kazi sana shughuli za huduma za sheria za Baraza letu.

Mhe. Spika, nilisema nisizungumze mengi, ile mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya Jimbo langu la Chambani naunga mkono mswada huu mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuwemo katika wachangiaji wa mapema. Naomba nitangulize shukrani zangu tena Mhe. Spika, kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais Aman Abeid Karume, wakati ulipompelekea wazo la kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi jipya na akakubali, ndio imani aliyokuwa nayo Rais wetu. Huwa kwa yale ya heri yote huwa Mwenyezi Mungu anamjaalia anatukubalia. *Inshaallah* tunaomba Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu na afya njema.

Mhe. Spika, nasimama hapa nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi na sijafanya tathmini ya waliotangulia kusema, lakini inaelekea mimi ni mwakilishi wa jimbo ambalo lilitoa maamuzi ambayo nitayasema baadae.

Mhe. Spika, naipongeza sana kamati ya watu sita au kamati ya Mhe. Ali Mzee, maana yake mimi lile wazo limelikubali. Wakati tulipokuwa kwenye Baraza kongwe tulimpa cheo cha u- *professor*. Sasa katika Baraza hili jipya mimi namtunukia cheo cha u-*chancellor* kwa sababu ya mambo makubwa aliyoyafanya. Sasa wale wasaidizi wake watano basi wale sasa wanapandishwa vyeo watakuwa ni ma-*professor* kwa sababu walichangia kwa kiasi kikubwa na kufanikisha zoezi hili.

Mhe. Spika, Rais Aman Karume tarehe 05 Novemba, alikutana na Katibu Mkuu wa chama cha CUF Maali Seif Sharif Hamad, wakazungumza na yakapatikana maridhiano. Tarehe 05 Novemba, Mhe. Spika, ni muhimu sana hii katika historia ya kumbukumbu zetu za matumio makubwa yanayotendeka katika nchi. Nadhani nchi nyingi duniani huwa wanaweka kumbukumbu za mambo mbali mbali yanayotokea na tarehe zao. Kwa hivyo, na mimi ningependekeza kuwa tarehe 05 Novemba, ikawekwa kwenye kumbukumbu zetu na bahati nzuri mimi ndio dhamana wa mambo ya kumbukumbu, lakini hizi taratibu zinakwenda za kiserikali. Sasa mimi naomba hii tarehe 05 Novemba, tuiwekee utaratibu maalum ambao utafikiriwa huko baadae.

Mhe. Spika, pia Mhe. Said Ali Mbarouk na wajumbe wengine wawili au watatu walizungumza juu ya kumtunza na kumpongeza Mhe. Rais Karume. Mimi nilikuwa nataka nitowe wazo kwa sababu Jumatano atakuja kutufungia Baraza letu hili au kulivunja Baraza i, sasa kama Mhe. Spika, hili litakubalika na waheshimiwa kuna haja ya kutayarisha *Certificate of Appreciation* ambayo itasainiwa na wajumbe wote wa Baraza hili, kwa ajili ya kumtunuku kwa kuheshimu kazi kubwa aliyofanya katika kipindi chake cha uongozi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, makofi yamepigwa nadhani ujumbe umefika kwa sababu hili jambo linafaa. Kwa hivyo, tutie saina ili ajue kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa vyama vyote viwili vikuu hapa wameridhika na uongozi wake. Kutokana na hali hiyo, tunampa *certificate* ile ambayo itakuwa ndio kumbukumbu yake ya kudumu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tumegaiwa hii Sheria ya Nam. 6 ambayo Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na Mhe. Juma Duni Haji wameizungumzia. Kwa hivyo, mimi naomba kuisoma kidogo kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kipengele kinachosema hivi:-

“Madhumuni Makuu ya Mapinduzi ya Watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii au upendeleo wa kisheria na mapungufu yote yaliyokuwa yakiwagawa wananchi na makundi mbali mbali ya raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini au uasili wa

mtu, madhumuni hasa ya Mapinduzi ni kukuza usawa, maridhiano pamoja na umoja wa watu wa Zanzibar.”

Mhe. Spika, unyonge hauna kabila, dini wala jinsia kama ulivyo utajiri hauna rangi, kabila wala jinsia. Kwa kweli napenda kujitolea mfano mimi mwenyewe kwenye familia yangu na kwa wale wanaotuelewa basi wanatuelewa na wale wasiotuelewa nataka watuelewe leo ninazungumza hapa.

Sisi tulikuwa wanyonge huko Makunduchi na leo *Alhamdulillah* nimesimama hapa namshukuru Mwenyezi Mungu ni neema za Mapinduzi. Kwa kweli kama si mapinduzi hapa mimi nisingefika. Tena ninao ushahidi Mhe. Spika. Kwa mfano, mpaka mwaka 1962 katika familia yetu kaka yetu mkubwa alimaliza kidatu cha nne katika Skuli ya King George wakati ule na hivi sasa ni Lumumba.

Kwa hivyo, aliomba kazi na baba yangu alifika pa kufika, lakini kutokana na unyonge wakati ule basi aliambiwa mwanao hatuwezi kumpa kazi. Kutokana na hali hiyo, basi alirudi nyumbani na baadaye alisaliki raka mbili kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kaka zangu wote unawajua alipasi Skuli ya St. Joseph na hivi sasa inaitwa Tumekuja mwaka 1963. Kwa kweli ile *fees* kama sikosei ilikuwa shilingi 5 lakini baba yangu ilimshinda na mwaka mmoja baadaye ndipo yalipotokea mapinduzi na Skuli hiyo ya St. Joseph ikachukuliwa na serikali na tulikosa nafasi na mpaka leo anauza duka hapo Mchanganani.

Kwa hivyo, mapinduzi haya yametukomboza Mhe. Spika, kwa sababu hayana ubaguzi wa aina yoyote kama malengo makuu ya mapinduzi yanavyosema. (*Makofi*).

Mhe. Spika, leo hii tunashuhudia mabadiliko mengine ambayo ni makubwa sana. Mabadiliko haya yametufungulia ukurasa mpya. Hivi karibuni nilikuwa nikizungumza na Walimu Wakuu pamoja na maafisa wengine Bububu, kwamba leo tunaendelea na shughuli zetu za kawaida kama hizi na hata wakaguzi katika hoteli ambayo bahati mbaya imeungua moto kule Jambiani ambako walikuwa wamefanya semina yao na wala msijekusema nimesababisha mimi aah!

Kwa hivyo, tulikutana pale kiasi wiki moja iliyopita na niliwaambia mnaweza kwenda kuzikagua skuli hivi sasa mpaka kesho uchaguzi mtakwenda. Lakini wakati ule tulipokuwa na uhasama, wakaguzi miezi mitatu kabla ya uchaguzi wanaacha kwenda kukagua, kalenda na kufunga skuli ilibidi tuzifunge mapema kwa sababu ya kutoa nafasi kwa masuala ya uchaguzi.

Mhe. Spika, mpaka hivi sasa ninavyozungumza shughuli za skuli zinaendelea kama kawaida, isipokuwa tutazifunga kwa sababu ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani na tutakapomaliza mwezi huo basi shughuli zetu zitaendelea kama kawaida na mitihani yetu itafanyika. Kwa kweli yote haya ni kutokana na hali ya utulivu tulionao katika nchi yetu hivi sasa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tarehe 31 Julai, 2010 wananchi wa Zanzibar walipiga Kura ya Maoni kwa ajili ya kukubali au kukataa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010. Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kupongeza kwa dhati kabisa wananchi wote wa Zanzibar kwa maamuzi yao ya kuamua kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tulikuwa na mtihani mkubwa na mimi nilikuwa na mtihani mkubwa kweli, kwa sababu nilihubiri Serikali ya Umoja wa Kitaifa kabla ya kupigwa kura na nilitembea jimbo langu lote kusini, kaskazini, magharibi na mashariki, yaani maeneo yote manne ya jimbo lile. Lakini Kura ya Maoni ilipopigwa matokeo kama mlivyoyasikia na wala sina haja ya kuyasema.

Kwa hivyo, mimi nikaanza kupoteza usingizi yaani sikulala, kwa sababu siku ya pili unafanyika Uchaguzi wa Kura ya Maoni kwa ajili ya kuchagua wagombea wa Chama cha Mapinduzi. Sasa kama Kura ya Maoni kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa wamesema hapana, hali itakuwaje kwangu mimi, kwa sababu mimi nilikuwa mstari wa mbele na nathubutu kusema nitakuwa mstari wa mbele mpaka dakika ya mwisho naunga mkono hoja hiyo na wala hakuna kurudi nyuma. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nilisema kwenye Baraza wakati tulipokuwa tukichangia hoja hii kwamba, *we are not ready to go back to that error* na wala hatuko tayari. Kwa kweli kwa mshangao mkubwa na mimi nilihuzunika sana kwa matokeo yaliyotokea kwenye Jimbo la Makunduchi, yaani nilikuwa mnyonge sana.

Hivi nimetembea katika maeneo yote kwa ajili ya kuwaeleza wananchi na kunisikiliza pamoja na kunipigia makofi na sisi viongozi wakati tunapopigiwa makofi huona kwamba ni mambo mazuri tu, basi makofi yale yalinipa mtihani mkubwa baada ya matokeo yale.

Mhe. Spika, napenda nikwambie kweli nimeshinda tena kwa kishindo sana kule kwa zaidi ya asilimia 90 na ninawashukuru kwa hilo. Lakini badala ya kupita kuwashukuru kwa kunipa kura nyingi basi nilipita na kuwauliza hivi jamani kumetokea nini kuhusiana na haya mambo. Kwa hivyo, waliniambia mheshimiwa tunakuomba yamalize na sisi tuko pamoja na wewe pamoja na wote walioamua Serikali ya Umoja wa Kitaifa na tutashirikiana kuunga mkono hoja hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa dhati kabisa na nimetembelea kwenye maeneo kama vile Kamati za Siasa pamoja na Masheha nikuzungumza nao katika kipindi hiki, kwa sababu mimi niliona unyonge mkubwa sana kuhusiana na jambo hili kwani nina imani au ninaliamini ndani ya moyo wangu yakatokea yaliyotokezea. Kutokana na hali hiyo, basi wameniahidi kwamba hayatatokezea makosa kama hayo, tena ninasema hapa kifua mbele kwamba wanaunga mkono na wala tusiwe na mashaka na Inshaallah mambo yatakuwa mazuri. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hili ni jambo kubwa sana kukaa, kupendana pamoja na kushirikiana. Vile vile tunafanyakazi na kutekeleza majukumu yetu katika hali ya utulivu. Kwa maana hiyo, naomba sana Mhe. Spika kuanzia leo tukiondoka hapa kwa Jimbo langu la Makunduchi nawaomba watu wasiende kwa ajili ya kuwaharibu mawazo wananchi wangu.

Kwa kweli jambo hili limekwisha na tayari tumeshaliunga mkono, kwa hivyo wasitokezee watu na kutia maneno ya hapa na pale, kwa sababu sote ni wamoja, tushirikiane kwa pamoja na kila mmoja na Itikadi yake ya Chama, lakini kwenye suala hili ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa tumeliamua sote kwa asilimia 66.4. Lakini tuchukulie sote baada ya maamuzi haya ni asilimia 100 kwamba tumeunga mkono hoja hiyo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu pamoja na marekebisho yaliyofanywa. Kwa hivyo, naomba sote Mhe. Spika, tuwe kitu kimoja kwa ajili ya kuendeleza mbele mustakbali wa maslahi ya nchi yetu.

Pamoja na hayo, naunga mkono hoja na ninakutakia kila la heri pamoja na mafanikio makubwa katika kuendeleza mbele juhudi zetu za kimaendeleo kwenye nchi yetu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuchangia mswada huu ambao umewasilishwa asubuhi ya leo kuhusu Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kwa kweli wenzangu wameshazungumza mengi katika mswada huu Mhe. Spika na wala sikuwa na nia ya kuchangia, isipokuwa nimeona kuna haja na mimi kuingia kwenye ukurasa wa historia katika kuchangia Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar.

Vile vile Mhe. Spika, nikushukuru hivi karibuni miezi iliyopita ulinichagua katika Kamati ya Watu Sita na Mwenyekiti wetu alikuwa Mhe. Ali Mzee Ali, kwa kweli ulinipa mtihani mkubwa lakini nilimuomba Mwenyezi Mungu akusaidie na alitusaidia kazi tumejitahidi kufanya na wananchi wote wameiona.

Mhe. Spika, tukiangalia kwenye mswada ukurasa wa 87 unazungumzia sababu na madhumuni ya kuletwa mswada huu na ninaomba ninukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 87 kifungu (i) kuhusu sababu na madhumuni kinaeleza hivi:-

- (i) “Kutekeleza Azimio la Baraza la Wawakilishi la mwezi wa Januari, 2010 kuhusiana na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Azimio hilo lilipelekea kupitishwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni, ili kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kuamua kama wanakubali au wanakataa juu ya uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010 ...”

Kwa kweli kazi hiyo imefanywa lakini kwa hatua. Sasa baada ya kazi hiyo niwapongeze wananchi baada ya kuelimika na kuweza kutoa maoni yao bila ya woga siku ya tarehe 31 Julai, 2010 na matokeo yameonekana na leo ndio tunarekebisha hiyo sheria. Kutokana na hali hiyo, nawapongeza sana wananchi wa Zanzibar baada ya kuona kwamba hapa tulipo hivi sasa tunachelewa, basi wamekubali muundo huo waliouamua kwa ajili ya kwenda kwa kasi zaidi katika maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile niwaombe wananchi kwamba hii ni awamu ya kwanza ya kazi tuliyoifanya ya Kura ya Maoni, lakini mwezi wa Oktoba, 2010 ipo kazi ya pili ya Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya kuweza kuunda hiyo serikali yenyewe. Kwa hivyo, nawaomba wajitokeze kwa wingi kama walivyojitokeza hivi juzi kupiga kura basi na kipindi hicho waje kwa wingi sana ili tuweze kufikia lile lengo tulilokusudia.

Mhe. Spika, kwa kila ambaye atakayefika na kuwa mzima na afya njema, basi ikifika mwezi huo wa Oktoba, 2010 waweze kupiga kura na serikali hiyo ambayo tumeipendekeza na leo ndio tunarekebisha Katiba iweze kuundwa. (*Makofi*).

Sambamba na hilo niipongeze serikali kupitia Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume pamoja na mawaziri wake, kwa jitihada kubwa ya kufanya marekebisho, pamoja na haya mambo tuliyoyaona katika kipindi hiki lakini bado kuna mambo madogo madogo ambayo nimeyaona na wameweza kuyarekebisha. Mhe. Spika, naunga mkono marekebisho hayo hasa kwenye kifungu cha 67 kuhusu suala zima la kuongeza uwiano wa Viti ya akinamama kutoka asilimia 30 kwenda 40. (*Makofi*).

Kwa kweli tunaipongeza hatua hii kwa sababu nchi nyengine zilizoendelea tayari zimeshafika asilimia 50 kwa 50, lakini na sisi kwa asilimia 40 nadhani si jambo baya sana tena ninaamini huko tunakokwenda tutafika asilimia 50 kwa 50.

Mhe. Spika, ninashukuru kwamba wameona tatizo kubwa katika Serikali za Mitaa nayo pia wamebadilisha sheria, ili Serikali za Mitaa ziweze kwenda vizuri. Kwa hivyo, hivi sasa kuna mchakato wa Sheria kuhusu Serikali za Mitaa, kwa lengo la serikali hiyo kusaidia maendeleo ya nchi yetu.

Pia imeonekana kuna kipengele cha Vikosi vyetu kugeuzwa hivi sasa kuwa Taasisi Maalum, hili ni suala zuri. Vile vile tunashauri Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ni kubwa sana, sasa nadhani watakaolingia madarakani wanaweza kuikasim, yaani Tawala za Mikoa ikawa inajitegemea na Idara Maalum vile vile, kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nimshukuru pamoja na kumpongeza Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume pamoja na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa jitihada kubwa walizozichukua. Hivi sasa nchi yetu iko katika hali ya utulivu na amani na tunategemea kwamba haya mawazo waliyofanya yatawekwa katika historia kwa ajili ya kufika kule tulikokusudia. (*Makofi*).

Mhe. Spika, sikuwa na nia ya kuzungumza mengi kwa sababu mswada ni mfupi na watu tayari wameshazungumza mengi, isipokuwa nia yangu ni kusimama na kusema machache na baadaye niunge mkono kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini.

Kwa hivyo, kwa kumalizia mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Vile vile tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie yale tuliyoyakusudia yaweze kufanikiwa kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika, kwamba leo tarehe 09 Agosti, 2010 kuwa katika kiti hicho cha enzi kwenye jengo hili jipya ambapo kama Mhe. Rais wa Zanzibar alipofungua alisema kwamba hili ni jengo jipya, siasa mpya na mambo mapya. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea naomba kuchukua fursa hii kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kuchagua ile Kamati ya Watu Sita, ambayo ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali na mimi nilikuwa ni mjumbe na kweli ile Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilianza pale, kwa sababu kulikuwa na wajumbe wa tatu kutoka kila chama, yaani CUF na CCM. Kwa hivyo, tulifanyakazi kwa ufanisi pamoja na ushirikiano mkubwa sana na ninashukuru sana. (*Makofi*).

Pamoja na hayo, nampongeza Mhe. Zakiya Omar Juma kwa sababu kwenye kamati ile alikuwemo yeye peke yake ndio mwanamke, lakini alifanyakazi kwa mashirikiano makubwa katika hali nzuri kabisa. Vile vile naomba kumshukuru sana Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa namna alivyokuwa akifanyakazi na sisi sambamba katika kutoa elimu kwa wananchi wa Zanzibar. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nakupongeza tena kwa mara ya tatu kwa namna ulivyokuwa pamoja na sisi kwenye kamati hii katika matokeo mbali mbali kwa ajili ya kutuunga mkono. Mhe. Spika, katika kamati hii nimejifunga mengi sana hasa kufanyakazi na Mhe. Ali Mzee Ali. Kwa kweli umahiri, uzoefu pamoja na ujuzi ambao anao Mhe. Ali Mzee Ali ni wa kupigiwa mfano na anastahiki sifa hizi kupewa, kwa sababu kazi aliyofanya ni kubwa. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wenzangu tunamshukuru sana. (*Makofi*).

Kwa kweli naunga mkono Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ulioletwa hapa na kusomwa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, vile vile naunga mkono masawazisho yale yaliyotolewa na Mhe. Haji Omar Kheir ambaye ni Mwenyekiti wa Katiba Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi.

Mambo haya yote ni mazuri kabisa na ninawaomba Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kuunga mkono mswada huu kwa moyo mkunjufu kabisa kwa ajili ya maslahi pamoja na mustakbali wa nchi yetu. (*Makofi*).

Vile vile nawapongeza sana wananchi wa Zanzibar kwa kutimiza ile azma ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hili ni jambo la kihistoria kabisa mara ya kwanza kufanyika Zanzibar tena limetupa heshima kubwa kwa Zanzibar, Tanzania, Afika na Ulimwengu mzima. (*Makofi*).

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimuendee Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na usimamizi wake mzuri wa kuongoza nchi hii hadi kufikia leo tunamaliza awamu hii kwa salama, amani pamoja na utulivu wa hali ya juu. (*Makofi*).

Kwa kweli mshikamano na uwelewano uliopo hivi sasa ni utabiri wa hakika kabisa kwamba serikali inayokuja itakuwa kweli ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambayo itakuwa serikali ya kushikamana na kuweka maslahi ya Wazanzibari pamoja na utaiifa mbele kuliko maslahi ya chama.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Jimbo langu la Ikulu naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ninaomba wenzangu waiunge mkono kwa ajili ya kuupitisha mswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ambayo ni muhimu. Pili natoa pongezi za dhiti kwako kwamba jengo hili zuri leo linaanza kikao chake ikiwa wewe Mheshimiwa ndiye Spika wa Baraza hili, kwa hivyo hongera sana. (*Makofi*)

Vile vile nichukue fursa hii kukupongeza tena kwamba Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 tunayajadili leo hapa ikiwa wewe ndio Spika wa Baraza hili, kwa kweli hongera sana. (*Makofi*)

Pia tunajadili mambo ya uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ukiwa wewe ni Spika wa Baraza hili, nasema hongera sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Baraza hili leo tuko katika hali nzuri ya amani, utulivu, mshikamano pahala pazuri, tumekaa uzuri na wengine leo tumevaa suti. Kwa kweli yote haya yanatokana na uongozi wako ambao ni mzuri wenye busara, hekma na unatuongoza vizuri kiasi ambacho sote tunafurahia uongozi wako Mhe. Spika.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia bila ya matatizo yoyote. (*Makofi*).

Pamoja na hayo natoa pongezi za dhiti kwa Kamati ya Watu Sita ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Mzee Ali. Kwa kweli Mhe. Ali Mzee Ali alizungumza siku moja kwenye televisheni kama sijakosea nadhani ni *Channel* 10 kipindi cha Bwana Hamza Kasongo yeye na Mhe. Zakiya Omar Juma.

Mhe. Ali Mzee Ali alitoa darasa la aina yake kwa ajili ya kueleza kwamba upinzani si uhasama, isipokuwa kinachotakiwa katika nchi ni kuwa nchi itulie pawe na amani, utulivu, watu waende kwenye maziko, harusi pamoja na kujadili mambo yao, yaani anamfundisha Bwana Hamza Kasongo. Kutokana na hali ile basi sisi watazamaji ndio tuliokuwa tukielimika.

Mhe. Spika, Kamati ile ya Watu Sita imefanyakazi vizuri sana kwa Unguja na Pemba kwa kuwahutubia Mashekhe, Masheha na sisi wananchi tunafarajika na tumeona raha kabisa. Kwa hivyo, hongereni sana Waheshimiwa. (*Makofi*).

Nikiendelea na mchango wangu nimpongeze Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ibrahim Mzee Ibrahim, kwa kweli vipindi vyake kwenye *Cable* vilikuwa vikitoa taaluma ya aina yake. Kwa mfano, siku moja nilikuwa nikiangalia *cable* nilimuona mwanasheria mmoja bwana Awadh nilivutika naye, lakini alipokuja kuzungumza bwana Ibrahim Mzee Ibrahim basi niliona raha Mhe. Spika. (*Kicheko/Makofi*).

Kwa kweli alieleza kwamba hawa Wapemba, Waarabu, Waafrika, Wahindi, Wakristo, Waislamu wote utawakuta kwenye chama ikiwa Chama cha CCM au CUF. Sasa unapowajumlisha wote, yaani kuwashirikisha wote katika serikali ya Umoja wa Kitaifa, basi wote utakuwa nao pamoja kwenye jahazi moja, lakini ukisema hawa Wapemba na wale hivi na vile.

Mhe. Spika, kwa kweli Katibu wa Baraza la Wawakilishi darasa lake lilikuwa la aina yake katika *cable* na wala hatuwezi kukusahau Katibu wetu, kwa sababu amefanyakazi nzuri na katika mchango huu ametoa taaluma ya aina yake kwa Wazanzibari. (*Makofi*)

Sasa nakwenda kwa Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad. Mhe. Spika, Maalim Seif unajua kama ametusomesha Lumumba ni maalim wetu, kwa sababu maalim wangu amenisomesha somo la *Geography*.

Hivi sasa Maalim Seif shughuli zote zinazofanyika basi yumo, kama vile Malaria, Ufunguzi wa *Generators*, Ufunguzi wa Uwanja wa Ndege, Harusi Ikulu kutunza pamoja na kucheza yote anayafanya. Mhe. Spika, huu ni ukweli juzi kwenye harusi alikuwa akikata rumba pale Ikulu, hamjamuona. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa hii ndio Zanzibar inayotakiwa na mambo haya tayari yameshaanza hata Katiba bado haijabadilishwa na wala sio Wazanzibari ukimtolea *Assallam Allaykum*, anajibu *Waallaykum Sallam* huku amekasirika aah! Yaani huyu amevimba na yule amekasirika na hivyo sivyo, kwa sababu sisi sote ni wamoja ambao ni ndugu. (*Kicheko/Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Spika leo tunajadili jambo muhimu sana katika nchi yetu, yaani mustakbali mzuri kabisa na Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie twende vizuri kama hivi. Mhe. Spika, sasa nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli Mhe. Rais dunia nzima inampongeza, kwanza kwa maendeleo ya nchi yetu, amani na utulivu na wala hajaogopa chochote waliosema wamesema, walioandika wameandika. Na alisema katika (*Makofi*). ufunguzi wa *generators* alisema nimemuuzia nani nchi hii na wala hajamuuzia, hoo! Mhe. Amani Abeid Karume ameuzia nchi, hivi amemuuzia nani, isipokuwa amewaleta Wazanzibari pamoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kikao chengine kijacho utakuta hapa mstari wa mbele humjui CUF wala CCM, yaani mawaziri watakuwa wa aina hii. Vile vile na wale wa nyuma hajulikani wa CCM wala CUF, isipokuwa wanapigwa vita mawaziri tu. Kwa hivyo, tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri aliyoifanya ya nchi yetu kwa miaka kumi, nchi imetulia pamoja na maendeleo ya hali ya juu na kila mtu ameridhika na tunamshukuru sana na anaiacha nchi yetu katika amani na utulivu sote wazanzibari tuko katika kitu kimoja na hili ndio jambo muhimu Mhe. Spika. Tukitoka hapo niwapngeze wazanzibari wote kwa kazi nzuri ya kutia kura ndio 96.4. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijawapongeza kwanza Mwanasheria Mkuu wetu, Mhe. Iddi Pandu, sisi wajumbe wa Baraza la Mapinduzi tunajua nini Mhe. Iddi Pandu kazi nzuri aliyoifanya na alivyotuongoza vizuri katika marekebisho haya ya katiba waheshimiwa wote wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kazi nzuri wamefanya, tulikuwa hatuna masaa kujadili mambo haya kwa sababu tulikuwa tunajadili mstakbali wa nchi yetu mambo mazuri, chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Amani alikuwa anatuongoza vizuri. Kwa hivyo wote Waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Mapinduzi tunawapa hongera pamoja na mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Pia nimpongeze mnadhimu wetu Mhe. Haji Omar Kheri, leo amezungumza mambo mazuri nikamwambia Mhe. Machano sisi Baraza la Mapinduzi hatukuliona hili, kamati imeona ya Katiba ya Baraza la Wawakilishi hiyo ni kazi nzuri sana, na kitu kwamba Rais akitoka chama kile basi Spika anaweza kutoka chama chengine, sisi hatujakiona Baraza la Mapinduzi lakini kamati ya Katiba imeona hilo kwa hivyo tunawapongeza sana Kamati ya Katiba. (*Makofi*).

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Tafana Kassim Mzee: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ambao mchango wangu utakuwa ni mdogo sana. Kwanza naunga mkono hoja hii iliyokuja mbele yetu ya marekebisho ya katiba naunga mkono zaidi ya mia juu ya mia.

Mhe. Spika, lakini nataka niseme kwa lugha ambayo siipendi kwa sababu sijui lakini nitasema neno moja tu, kama sikosei Mahatma Gandhi wakati wa kudai uhuru alisema hivi kuwaambia wananchi wake “ *An eye for an eye will make the whole world blind*” Haya yalisemwa na Mahatma Gandhi moja ya waniasia maarufu hapa duniani kule India.

Mhe. Spika, wote tunaelewa kuna kipindi cha miaka mitano ambapo serikali inakuwepo madarakani ni kipindi cha miaka mitatu tu ndio kunakuwepo na utulivu katika visiwa hivi, mwaka mmoja baada ya uchaguzi ni vurugu na mwaka mmoja kabla ya uchaguzi inakuwa ni vurugu. Kwa mfano kipindi

hiki ni kawaida katika visiwa hivi kuanza kuona yale magari ya maji ya Polisi yanatembea tembea lakini mpaka tumefikia hivi leo tumepiga kura za maoni ya serikali hii ambayo tumeikubali hakuna gari la aina yoyote wala polisi wanaoranda na gari zao nyengine kumekuwa na hali ya utulivu.

Lakini hili Mhe. Spika, limekuja baada ya ujasiri ambao wa Rais Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif ambao watu wengi wameshazungumza, nasema haikuwa rahisi hata kidogo hata kwa Amani mwenyewe ingekuwa kwa mtu mwengine ambae hajiamini kukubali kukutana na Maalim Seif Sharif na kutoa yale maamuzi ambayo kwa sehemu kubwa watu walikuwa hawayataki na walikuwa hawayataki kwa sababu hawaelewi. Hivyo mimi nisema Rais gani katika nchi yoyote ile katika dunia angependa kuongoza watu ambao asubuhi akiamka kwa hapa kwetu kuna sheha unamkuta katiwa *acid*, keshokutwa ukiamka nyumba ya huyu imetiwa moto, Rais gani angependa kuongoza nchi ya namna hiyo Rais anapenda kuongoza nchi ambayo ina watu wametulia watulivu wanafanya mambo yao.

Sasa hali hii ambayo tumeifikia hata kuwepo kwetu hapa ni sababu ya kukutana watu hawa wawili, nikiwa mwanasiasa kwa kipindi cha miaka kumi na tano karibu kila chaguzi niliwahi kupata tatizo ndani ya jimbo langu, lakini pia nikiwa njiani katika safari zangu za kawaida tuliweza kutekeleza hizi shughuli za kikazi, kule kwetu Kiboje basi CCM ikishinda hao hao CCM wanakwenda kuharibu mazao ya CUF wanakata migomba, wanachukua kuku wa watu ndio hali hii lakini mpaka sasa hivi sijalisikia hilo.

Siku moja natoka kwenye kampeni nimeazima gari ya Mhe. Ali Suleiman Ali gari yangu ilikuwa mbovu ile kubwa ile, nafika Dole pale gereji kizimbani kuna kijana akanisimamisha nikamwambia dereva simama hebu msikilize mimi nikajua anaomba lifti tu unajua ukiwa mwanasiasa wakati mwengine unalialia japo maiti sio wako kwa hivyo hata mtu akikusimamisha usipomchukua ataninyima kura huyu. Kwa hivyo nikasimama alikuwa hanijui mimi nani lakini alipokuja akanambia Mhe. Tafana nakuomba hapo Langoni Skuli usipite, nikamwambia kuna nini akanambia hakupitiki, nikamwambia dereva twende lakini pole pole ni kweli nimefika pale nimekuta kumewekwa *road block* ya gogo imewekwa njiani nimefika tu gari imeshavamiwa.

Lakini wavamizi hao ni CCM wakati huo CUF wako kaskazini wanafanya mkutano nilipofika pale waliponiona mimi wakasema ondoa gogo haya pita, lakini kabla ya kupita akanambia simama shuka ndani ya gari tukutoe nje kwa mchaka mchaka na mimi kwa sababu mazoezi nayaweza wakanitoa nje pale mpaka mwisho wakaweka *road block*. Lakini pale pale nikakuta kuna watoto wameshapigwa kwa hivyo pale alikuwa anasubiriwa CUF akitoka kwenye kampeni akifika pale anapigwa, kule Bububu nako ni hivyo hivyo ndio hakupitiki.

Sasa leo hii ameshasema Mhe. Mugheri hapa wale wanaosema kwamba Amani ameua nchi hawa watu ni wapuuzi hawajui wanalolisema tusiwalaumu tuwaelimishe, kama Amani ameua nchi alotuuzia ni sisi CUF na CCM na vyama vyengine basi wacha tununue tufanye kazi tulete uvulivu na tulete amani.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo napenda sana niwanasihii wananchi wote ambao walipiga kura ya hapana na zaidi niseme katika Mkoa ambao umepiga kura za hapana ni Mkoa wa Kusini takriban, sina hakika jimbo la Koani lakini majimbo yote yaliyobakia yamepiga kura hapana mimi ningewaomba wananchi wa majimbo haya siku ya kupiga kura waende wakapige kura waipe CCM ushindi, wakinuna kama walivyonuna Abubakari yupo pale na chama chake na Rais atatoka kule na sisi tunataka Rais atoke huku kwetu. Kwa hivyo wasinune waende wakapige kura ili CCM iweze kuongoza serikali inayokuja ni yetu sote na nina imani kabisa tutaweza kushirikiana.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa hakika mchango wangu sio mkubwa lakini naunga mkono mswada huu ambao umeletwa mbele yetu wa marekebishi ya katiba. Lakini jengine kwa wale wawakilishi ambao ni wapya watakaokuja hapa sikufanyii kampeni Mhe. Spika, lakini nadhani wangempa nafasi Mhe. Spika, wamchague awe tena Spika, wa Baraza hili. Katika kipindi changu chote ambacho nimekuwepo hapa miaka kumi na tano wote tuna imani kabisa na uwezo wako wa

kuliongoza Baraza hili, umeliongoza kwa hekima kwa busara na sijawahi kukuona umekasirika hata siku moja.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia jambo muhimu sana kwa taifa letu la Zanzibar, laiti kama si umuhimu huo basi ningekaa kitako nisiseme kitu, lakini nahisi nitakuwa sijaifanyia vyema nchi yangu ya Zanzibar kama sijazungumza angalau kidogo kuhusiana na suala hili muhimu ambalo tumekuwa tukienda nalo kwa kipindi sasa na atunaelekea katika kufikia ukingoni mambo yaweze kutengenea na kufikia pale tulipokusudia kupafikia.

Mhe. Spika, naanza mazungumzo haya ya saa hizi kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu Allah na namuomba aniongoze niweze kwenda vizuri kama vile nilivyokusudia, baada ya hayo naomba nianze na shukurani nyingi sana Mhe. Spika, kuwashukuru wananchi wa jimbo la Mkoani Pemba jimbo ambalo liko katika Bandari kuu ya Pemba ambako watu wengi huwa wanafikia ukiacha wale wanaopanda ndege.

Mhe. Spika, watu wa jimbo la Mkoani ni watu wa aina yake waliniona nawafaa kuwawakilisha kuwatetea na kutoa mawazo yao kila pale panapostahiki kuwatolea mawazo katika Baraza hili na kwengineko wakanichagua kwa umoja wao nikawa mwakilishi wao, nimefanya kazi hiyo katika vipindi viwili ambavyo sio vya mfululizo kwa sababu ambazo hazikuepukika katika kipindi kimoja cha kati kati.

Mhe. Spika, kutokana na takirima yao hiyo kutokana na kunipendelea wakanipa nafasi hii adhimu na kwa sababu nimeshawaomba radhi kuwa mara hii sikugombea kuwawakilisha tena katika baraza hili basi nawashukuru sana kwa kipindi chote ambacho tumekuwa tukifanya mambo mbali mbali ya maendeleo ya jimbo letu kwa pamoja na maendeleo ya nchi na kuwawakilisha na wakawa wananiunga mkono kila wakati, nashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, naomba kuwahikikishia tu watu wa Jimbo la Mkoani kuwa kutokugombea kwangu haina maana kwamba nimewaacha mkono lakini maana yake ni kuwa mimi ni mwalimu na mwalimu hupenda kufundisha, kwa hivyo natoa nafasi kwa wale ambao bado hawajapata nafasi hii ili wawe na mwalimu wakati watakapokuja katika Baraza hili na Mhe. Spika, nakuhakikishia utaona kazi nitakayoifanya ya kukufundishia mjumbe wako atakayetoka Mkoani atakavyokuja kufanya kazi katika Baraza hili.

Mhe. Spika, nikiacha hapo naomba niwashukuru sana sana wazanzibari kwa umoja wao, nawashukuru kwa sababu wameweza kusikiliza, wameweza kupima wakaweza kuamua, wamesikiliza mawazo mbali mbali yaliyokuwa yakitolewa na watu mbali mbali kuanzia viongozi mpaka wale waliokuwa sio viongozi. Wakayapima mawazo yale vizuri sana na hatimae wakatoa uamuzi sahihi waliouona wao na ambao na mimi kwa upande wangu nauona ni sahihi kama vile walivyoona wao.

Kwa hivyo nawashukuru sana kwa hilo, lakini kwa nini niwashukuru kwa sababu Mwenyezi Mungu katuletea neema kutokana na maneno yake aliyotwambia Mwenyezi Mungu kutokana na ahadi zake alizotuahidi Mwenyezi Mungu tumezitekeleza na kwa kuzitekelza huko mambo yameanza kubadilika kuanzia humu ndani ya Baraza mpaka nje ya Baraza, kuanzia tuliyokuwa na uwezo nayo mpaka tuliyokuwa hatuna uwezo nayo. Sisi hatuna uwezo wa kuleta mvua analeta yeye mwenyewe Mwenyezi Mungu hapana asiyeona mvua ilivyonyesha mara hii, imenyeshwa mvua nzuri sana ya aina yake inayohuwisha mazao ya kutosha hii ni neema kaileta Mwenyezi Mungu kwa sababu aliahidi, kaahidi kuwa habadilishi kitu miongoni mwa watu mpaka wao wenyewe kwanza waanze kubadilisha sisi tumeanza kubadilika Mwenyezi Mungu na yeye kaja katubadilishia na katuletea mema baada ya ukame tuliokuwa tukiupata kila wakati.

Mhe. Spika, jambo hili ni kubwa sana na ndio maana nikasema nisimame angalau niseme na mimi kidogo, sasa nataka niwashukuru vingozi walioliasisi jambo hili nikianza na Mzee watu aliyekuwapo juu pale Mhe. Hassan Nassor Moyo, napenda nitoe shukurani za dharti kabisa zilizotoka ndani ya moyo wangu kwa sababu Mwenyezi Mungu alimtumia yeye kulianzisha jambo hili na akalianzisha kwa watu wawili Mwenyezi Mungu nae akawapa ilihamu watu wawili wale wamkubali waende kidogo kidogo kwa hatua mpaka pale lilipofikia pahali pa jipu kutumbuka Mwenyezi Mungu akalitumbua vyema akalitoa moyo kidonda kikawa safi kikatiwa dawa sasa kimepona.

Mhe. Spika, hili sio jambo dogo ni jambo kubwa kwa hivyo napenda nitoe shukurani kwa viongozi wetu hawa watatu, Mhe. Hassan Nassor Moyo, Mhe. Rais Amani Abei Karume na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, natoa shukurani za dharti kwa nafsi yangu lakini pia kwa niaba ya jimbo langu la Mkoani.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo niseme kuwa sasa hivi tunaelekea katika njia iliyonyooka na kuna viongozi waliotangulia katika nchi mbali mbali ambao wameweza kufanya mambo mazuri wakawaacha wananchi wao katika hali ya umoja na utulivu, mmoja katika hao naomba nimitaje Mhe. Spika, ni mzee Nelson Mandela. Huyu kafanya kazi ngumu sana na mwenyewe katika kitabu chake kaandika jinsi alivyofanya kazi mpaka akaiacha nchi katika hali ya utulivu anasema kapambambana na wakoloni mpaka akawaweza, akisha akarudi akapambambana na wenzake mpaka nao akawaweka ndipo alipofika pahala akaiweka nchi katika hali ya utulivu uliopo hivi sasa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, katika jambo hili zima tujue kuwa kuna kazi ya kufanya bado kuna kazi ya kuwaelimisha ambao watakuwa bado hawajafahamu vizuri, kwa wale waliokwisha kufahamu kuna kazi ya kuzidi kuwaunganisha ili tusukume mbele maendeleo yetu tuliyoyakusudia. Mhe. Spika, hii sio kazi ndogo ni kazi kubwa tunalolifanya hapa leo ni kutandika miundo mbinu ambayo itatusaidia baadae kwenda katika safari tunayoitaka kwa kutumia chombo tunachokitaka, tunataka kubadilisha katiba ili katiba hii imuwezeshe kila Mzanzibari kujiona kashinda katika uchaguzi, na kila mzanzibari akijiona kashinda katika uchaguzi maana yake nini. Maana yake Wazanzibari wote watakuwa katika kitu kimoja na wakiwa kitu kimoja maana yake nguvu ya kwenda katika maendeleo itakuwa ni kubwa zaidi.

Kwa hivyo tendo hili tunalolifanya ukiachilia mbali kubadilisha historia na kuweka historia mpya lakini pia itakuwa ni chachu ya kuleta maendeleo endelevu ambayo ndio tunayoyataka ili wananchi wetu nao waweze kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, juzi tuliambiwa hapa katika ufunguzi kuwa jengo hili jipya litakuwa na mambo mapya hiyo mimi nakubali na wala sikubali kuwa imesadifu hii haikusadifu lakini ilipangwa, lakini hatumjui aliyepanga ni nani hii aliipanga Mwenyezi Mungu kuwa ifike siku tulifungue jengo hili kwa mambo mapya. Ndio maana mswada huu wa marekebisho ya katiba umekuja ndani ya jengo jipya haidhuru tunatubwika tubwika wakati mwengine lakini ni afadhali hilo kuliko kutokufika kabisa, nakuomba Mhe. Spika, usiwe na huzuni tukitubwika kwa sababu hakuna jambo jema lisilokuwa na misuko suko hii ni midogo tu hakuna hata mmoja aliyetubwika akavunjika mguu, sana anatubwika kidogo halafu anarudi juu tunakiunga basi tunakaa kitako.

Kwa hivyo hili lisikushughulishe Mhe. Spika, ni mambo ya kawaida sana katika utekelezaji wa mambo mazuri, mabadiliko haya ya katiba ni mabadiliko muhimu sana niishukuru serikali kwa sababu wengine tulitarajia labda yatakuja mabadiliko ya katiba yanayohusu lile tu jambo la serikali ya umoja wa kitaifa. Lakini kumbe katika utekelezaji wa katiba iliyokuwepo kuna mambo ambayo yalikuwa yakileta matatizo wakati mbali mbali nashukuru kuwa serikali iliyaratibu mambo yale ikayaweka kungojea nafasi itakapotokea ya kubadilisha katiba ya yale yabadilishwe nashukuru kwa hilo.

Ndio maana tukaona katika mswada huu kuna mambo yanayohusu hili tulilolikusudia hasa lakini pia kuna mambo mengine ambayo hayamo katika lile tulilo likusudia haya yalikuwa yakileta tabu katika utekelezaji wa katiba yenyewe tuliyokuwa nayo, na wakati wote inapotokea nafasi basi nafasi ile

itumiwe vizuri kwa sababu unapotumia nafasi wenyewe wachezaji mpira wanasema nafasi moja ni goli, sasa ukiizembea nafasi ukilikosa goli utafungwa wewe.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naona hapa tumefikia pahali pazuri sana na sitaki niingie ndani ya mswada kwa sababu kamati imefanya kazi nzuri sana katika mswada, isipokuwa tu kuna jambo dogo tu kama kawaida yangu naomba yale mambo ya lugha yarekebishwe rekebishwe kidogo ambae iwe ambaye, hata katika marekebisho ya kamati pia kumeandikwa vile vile ambae lakini iwe ambaye. Hayo ni mambo ya lugha na wataalam wa lugha wayaangalie angalie.

Mhe. Spika, naomba nimalizie suali hili nililokusudia kuzungumza hapa leo kwa kuzungumzia habari ya hili jengo tulilona jipya, namshukuru sana mjenzi wa jengo hili na waliofanya jengo hili lijengwe wote nawashukuru. Lakini nina pendekezo moja tu dogo kuwa kama kutatokea jengo jengine zuri linalotaka kujengwa Zanzibar basi ikiwa mjenzi huyu nae ataingia katika tenda basi afikiriwe upesi zaidi yeye kuliko wengine, maana yake hapa katufanyia kitu kizuri kinachopendeza. Kwa hivyo hili nilikusudia nae nimuombe kama litatokea jengo jengine ambalo ni zuri sana basi aangaliwe na yeye katika tenda yake kama ataleta kwa sababu hili kaweka mfano.

Mhe. Spika, jambo zuri halihitaji mambo mengi lakini kilichobaki ni kufanya vitendo tukaendelea mbele, nakushukuru Mhe. Spika, naunga hoja mkono mia kwa mia mimi pamoja na wananchi wa jimbo langu la Mkoani kama walivyozipiga kura zao lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hili na namuomba atuongoze hapa tulipofika tusije tukabadili njia atuongoze tuende njia hiyo moja kwa moja mpaka kule tulikokusudia. Ahsante Mhe. Spika, (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Moh'd Ali Salim kwa maneno mazuri ya Mhe. Nelson Mandela mzee wetu katika Afrika na juzi tu ulitaka kwenda kumsalimia huko huko lakini ikawa hukupata nafasi, ukapata kwenda pale Mkumalanga.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuzungumzia machache kuhusiana na mswada huu muhimu wa marekebisho ya katiba, kwa ajili ya kuelekea katika serikali ya umoja wa kitaifa kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na wazima tukaweza kuidiriki siku hii ambapo mambo mawili kwa pamoja mazuri yanatokea. Kwa upande wa kimaadili tunaingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ni muhimu sana, lakini pia tumebahatika kuingia katika jengo jipya ambalo hata ule ushindani wenyewe utakuwa haupo wa kubezana na kupeana vijembe.

Mhe. Spika, kwa sababu naupenda ukumbi huu kwa sababu ukumbi ule wa kutizamana usoni ulikuwa unatupa tabu sana. Lakini sasa hivi akizungumza mtu hamtizami mwenzake usoni pengine itakuwa anazungumza *free* zaidi kuliko vile ilivyokuwa katika ukumbi ule. Kwa hivyo, jambo hili ni la kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu mambo yote mawili yamekuja katika wakati moja.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ni kwamba serikali tukitizama ulimwenguni inaendeshwa na watu wote walioko katika nchi. Kila kabila, kila eneo na kila aina ya watu Mwenyezi Mungu kawapa kipaji fulani ambapo pengine hawa huwa hawana. Hivyo, wakishirikiana watu wale basi panapatikana jambo ambalo ni zima. Mhe. Spika, mfano, mtu ambaye ana kifua kipana ikitokezea ugomvi atawekwa mbele awe ni *boxer*, lakini ikiwa kuna haja ya kupanda mti yule *boxer* itakuwa hafai atatafutwa mtu mwembamba kwa sababu aupande ule mti ndio utakaom-*support* na ikitokezea haja ya kupenya mvunguni atatafutwa mtu mfupi ili apenye kule mvunguni.

Mhe. Spika, watu watatu hawa kila mmoja katumika katika kazi mbali mbali na kwa haja maalum. Hiyo ndio ilivyo katika taifa kila watu wanaotoka katika eneo tofauti wana vipaji vya aina fulani na wana uwezo wa aina fulani na wengelitumika kikamilifu basi taifa lile lingepiga hatua ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wa Tume ile ya watu sita pamoja na wajumbe wake wote wa Baraza letu la Wawakilishi kwa kazi nzuri waliyoifanya na elimu ambayo waliyokuwa wakitoa.

Mimi ni mmoja wapo niliyekuwa nikitizama *cabl*e televisheni katika vipindi vyao vingi walivyokuwa wakielimisha. Moja katika kitu muhimu Mhe. Spika, ni kuona kwamba sisi *system* zetu tulizokwenda nazo zimefeli na zimefeli si kwa sababu hazikuwa na nia nzuri, lakini zimefeli kutokana na historia inaonesha kwamba uungwaji mkono wa kila upande katika historia yetu umekuwa ukikaribiana sana.

Mhe. Spika, tukichukua uchaguzi wowote ule uliopita na hivi sasa katika mfumo mpya wa vyama vingi tumekuwa tukipata matokeo yaliyokaribiana sana katika chaguzi zetu. Kwa hivyo, ule mfumo wa pata yote chukua yote haukutufaa sana kwa sababu ni kundi kubwa lilikuwa linaachwa katika kuunda serikali. Mhe. Spika, kwa hiyo mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hauko katika kupunguza labda kasi ya ushindani au kupunguza kasi ya upinzani lakini imekuja historia kuziba lile pengo ambalo lilikuwepo.

Kwa hivyo, mimi nawaomba sana pamoja na kwamba mimi mwenyewe binafsi kwa niaba ya jimbo langu naiunga mkono sana hoja hii ya kuwepo mabadiliko haya ya Katiba kwa asilimia mia moja. Lakini nawaomba sana Wajumbe kwa maslahi ya Zanzibar, kwa maslahi ya kizazi kijacho tuiunge mkono hoja hii ili tuweze kupata manufaa.

Mhe. Spika, sitaki kwenda mbali asubuhi tu hapa tumesomewa kwa sababu waswahili wanasema “mkataa wengi mchawi” hapa tumesomewa jinsi ulimwengu unavyotuunga mkono katika maamuzi yetu haya. Mhe. Spika, itakuwa si vizuri kwamba wananchi wamepitisha kwa asilimia kubwa tukatokezea Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukawa hatukuyaunga mkono, tutakuwa tumeangusha mawazo ya wananchi wetu. Mhe. Spika, hilo ni jambo la pili.

Mhe. Spika, jambo la tatu ni kwamba katika kuendesha shughuli zetu kitu ambacho kilikuwa kinakosekana ni kitu cha kuaminiana. Wakati mwingi ilikuwa upande huu hauamini huu, na upande huu hauamini huu. Kwa hivyo, hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa italeta ile nafasi nzuri ya kujenga kuaminiana, tukianza kujenga kuaminiana tunaanza kujenga ukaribu na kuanza kujenga ufanisi katika kazi kwa sababu serikali itakayokuwepo madarakani itakuwa ni ya wote kila mmoja anashiriki. Hii ina tofauti na serikali ya mfumo wa chama kimoja kwa sababu mfumo wa chama kimoja unakuwa na mawazo ya aina moja, lakini Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya mfumo wa vyama vingi inachukua mawazo tofauti na yale mazuri yanapelekwa mbele na yanafanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi.

Mhe. Spika, kwa hivyo hakuna kubwa la kuzungumza isipokuwa wananchi wa Zanzibar wanahitaji hii na hii imeonekana wazi wazi sasa hivi. Kwa hivyo, naiomba sana Tume ya Uchaguzi baada ya kuipa pongezi kubwa sana za kuwaonesha Wazanzibari katika uchaguzi huu wa kura ya maoni kwamba wasiuchukue uchaguzi. Mhe. Spika, kwa taarifa yako watu wetu wengi walikuwa wameshauchukia uchaguzi na mimi binafsi kuna msemo mmoja unaitwa *guilty conscious* nilikuwa nimeshafikia kiwango hicho. Mimi nilijihisi mimi nikienda nikiomba kura nawatia katika dhiki wale wananchi. Kwa hivyo, kuna kipindi nilijihisi kwamba mimi niko *guilty conscious* kwa nini?

Wanapokuambia kwamba tukupatie wewe pato kumbe kuna mambo mengi ambayo katika uchaguzi wanajiamulia wao wenyewe sio kumfuatia mwakilishi au kiongozi mwengine pato. Lakini ni kwa sababu walifikia kusema vile kwani ile tabu inayowapata katika uchaguzi na wengine walikuwa hawaamini kwamba uchaguzi Zanzibar unaweza ukafanyika kama hivi ulivyofanyika wa kura ya maoni. Kwa hivyo, mimi kwa heshima na taadhima kubwa natoa pongezi za aina yake kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Tume ya Uchaguzi kwa kuendesha uchaguzi uliyowarudishia watu matumaini ya kwamba sasa nende kupiga kura kwa sababu kupiga kura sio dhiki, sio kero.

Hilo naliomba nilisisitize sana na kwa njia hiyo basi, naiomba sana Tume ya Uchaguzi ichukue nafasi yake ya kuhakikisha kwamba uchaguzi unaokuja unafanywa katika utaratibu ule na kuongeza kasi zaidi ya uzuri ili kila mwananchi ajihisi kwamba yuko huru kwenda kupiga kura na aone kwamba ni fursa muhimu katika kupiga kura.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza viongozi wetu wakubwa wawili, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Dk. Amani Abeid Karume) kwa uamuzi wake wa busara kwa sababu waarabu wanasema mtu mwenye kusamehe ni yule

mwenye uwezo wa kusamehe, lakini wakati yeye ni Mhe. Rais ana kila nguvu za kutumia nafasi yake, lakini akasamehe huo ndio msamaha Mhe. Spika. Kwa hivyo, yeye ilivyokuwa ni Mhe. Rais na akaweza kuja chini akakaa kitako na kiongozi wa upinzani Maalim Seif Sharif Hamad yeye alistahiki nafasi ya kwanza ya kupewa pongezi.

Vile vile natoa pongezi sana kwa Mhe. Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF (Maalim Seif Sharif Hamad) baada ya yote yaliyotokea na akasema yote yaliyotokea ni kwamba yamepita sasa hivi tuende hapa. Pia na sisi wajumbe ambao tumeingia kwa niaba ya Chama cha CUF katika Baraza hili ametupa nafuu kubwa ya kuweza kuzungumza mambo ya kitaifa. Mhe. Spika, baada ya hapo kwa sababu marekebisho haya ya Katiba yalifanywa kwa nia safi na Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala Bora mimi nawapongeza sana kwa kuviona vifungu tofauti na kukubali ushauri wote uliotolewa na Kamati ya Katiba na Sheria. Mhe. Spika, kwa njia hiyo naipongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzito katika kipindi hiki kikaturahisishia sisi humu ndani ya Baraza kuweza kuyafahamu na kuyapitisha.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba niwaombe wananchi kwa sababu Katiba hii tunayoitunga ni kwa wananchi wote tuyakubali haya mabadiliko yaliyokuwepo. Mhe. Spika, Serikali ya Umoja wa Kitaifa inaletwa kwa maslahi ya wananchi wote hivyo nawaomba wananchi naanza na jimbo langu kama walivyoipigia kura sasa nawaomba wananchi wa Jimbo la Ziwayi wayakubali mabadiliko ya Katiba yatakayoletwa yakiwagusa wao au yakiwagusa wengine wao wayakubali.

Mhe. Spika, kwa sababu ndivyo tutakavyokwenda na wale wananchi waliopiga kura ya maoni nawaomba sasa wayakubali haya mabadiliko yaliyoletwa. Lakini kuna wananchi wenzetu ambao kwa sababu moja au nyengine ni kwamba wamepiga kura ya hapana.

Mhe. Spika, hao kwanza wametumia demokrasia yao ile kujitokeza wakaenda kwenye uchaguzi ni sehemu moja kubwa kwamba wamekubali kwamba upo uchaguzi. Kwa hivyo, ni jambo ambalo wao wanastahiki sifa, kama ingelikuwa wamegoma hawakwenda ingeonesha wamechukiwa hawajulikani na lolote. Lakini madhali tunajua kwamba wako waliokuwa wametia hapana sisi tunawaomba sana wafahamu kama kulikuwa na watu waliowapotosha sasa wajirudie waseme kwamba sisi hatukufahamu vizuri lakini ni kwamba tushirikiane nao katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayokuja ili tufike katika maendeleo ambayo yako katika ulimwengu huu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie hapa kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuweza kuchangia marekebisho haya ya Katiba. Mhe. Spika, nataka nimsifu Mhe. Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu, nawashukuru sana viongozi wetu wakuu tukianza na Mhe. Waziri Kiongozi, Naibu Waziri Kiongozi pamoja na mnadhimu wetu kwa kufika pahali pazuri na kumaliza miaka mitano kwa salama usalimini.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia kwanza nataka nimsifu zaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa yale ambayo aliyoyalenga kwenye ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi amefikisha katika asilimia mia moja. Leo Alhamdulillah tunaona yale mambo yaliyooneshwa kuwa atayarekebisha na atatekeleza hususan afya sasa hivi tuna vyombo vya kisasa tunashukuru, barabara tunaona mambo ni mazuri. Pia katika majenzi juzi tu tumeona amefanya vizuri kabisa, gati sasa hivi ni za kileo. Mhe. Spika, hivi sasa tukiwa katika jengo hili zote hizo ni katika hizo ahadi za Mhe. Rais, hivyo tunamuomba mapumziko ya kheri na salama.

Mhe. Spika, pamoja na hayo ni kwamba jana katika *briefing* yetu pale tulisema eneo hili tulipewa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye tunampongeza sana kwa jitihada zake kubwa kutupa eneo hili kwa kusamehe kufanya lile lengo lake na akaona bora atupe eneo hili kwa kuwa na Baraza jipya na leo tunajivunia kabisa. Mhe. Spika, pamoja na hayo amemaliza na sehemu ya nyuma kule tuichukue yote ili kuweza kuweka mambo mengine ambayo yanastahiki na Baraza.

Mhe. Spika, sasa nije katika mchango wa marekebisho. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 81 kidogo nina wasi wasi unajua katika lugha kila mtu ana ufahamu wake. Siku moja Mhe. Moh'd Ali Salim (Mulla) alisema kuwa lugha ina tafsiri mambo mengi sana, na nimeona kuwa ni kweli utavyoona wewe, mwengine sivyo atakavyoona.

Mhe. Spika, mimi akili yangu ni kwamba hapa haijatulia ilipoambiwa kuna kikosi maalum cha kuzuia magendo halafu kufutwa kikawa kikosi maalum. Mhe. Spika, kidogo hapa namuomba Mhe. Waziri aniweke sawa akili yangu mpaka sasa hivi sijafahamu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleweshe vizuri kwa sababu huko nyuma tulikuwa na lugha hiyo ya kikosi maalum cha kuzuia magendo, lakini leo vikosi hivyo vinaondoshwa vinawekwa tena vikosi maalum. Mhe. Spika, hivi vyengine sijui vitaitwa vipi maana yake humu havikuoneshwa hivyo. Namuomba Mhe. Waziri anisaidie hili ili na mimi katika ile asilimia yangu ya kuchangia ikamilike.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 82 vile vile kwa masikitiko zaidi kuambiwa leo Wakuu wa Mikoa wanatolewa katika Baraza. Mhe. Spika, hili nalo naomba liangaliwe kwani limeshazoeleka na tumeona umuhimu wao wakiwa humu katika Baraza, leo hapa tunaambiwa wanaondoshwa. Kwa hivyo, na hili nalo namuomba Mhe. Waziri aweze kutusaidia kwani hawa kuna umuhimu wake wakiwemo ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, ni kwamba kuna sababu gani ya kuwaondosha au labda kuna utaalumu zaidi au kuna sheria zaidi juu ya jambo hili la kuwaondosha hawa wakuu wa Mikoa. Kwa hivyo, ningepomba Mhe. Waziri atusaidie ili tuweze kufahamu kuwa wanaondoshwa kwa sababu gani. Pia tukae tufikiri tukiwaondoa hawa kutakuwa na hasara au kutakuwa na faida, nalo hilo namuomba Mhe. Waziri aweze kutusaidia.

Mhe. Spika, kama nilivyosema watu wengi wamezungumza tangu mapinduzi, wazee wetu wapo hapo kina Mzee Hassan Moyo, hilo nakubaliana nalo kwa mzunguko wote huo wa wenzetu walivyochangia. Mimi kama nilivyosema sitakuwa na mengi katika mswada huu isipokuwa nitaunga mkono asilimia 70 na Mhe. Waziri atakaponijibu hayo maswali yangu mawili nitakamilisha ile asilimia mia moja yangu kama kawaida yangu. Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo ili na mimi niweze kutia baraka juu ya mswada huu. Mhe. Spika, awali ya yote napenda sana kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia leo hii katika mipango yake ambayo ameipanga muda mrefu. Lakini ikafikia wakati kwamba umetukuta na sisi tupo.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu huwa amelikadiria kila jambo kwa wakati wake tofauti na binadamu tunapanga kwamba liwe lakini haliwi, na haliwi si kwa sababu kwamba halitakuwa lakini ni kwa sababu ya ule muda ambao limepangwa liwe ulikuwa haujafika. Kwa hivyo, nadhani hili tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujaalia kwamba limefika na sisi tukiwa tunashuhudia.

Mhe. Spika, nitoe shukurani za dhati kwako na mimi kwa kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu. Mchango wangu sana utakwenda katika kutoa shukurani kwa kila ambaye nahisi anahusika na suala hili kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, wenzangu wametangulia kusema hapa kwamba bila ya uamuzi wa wananchi uliofanywa tarehe 31 Julai, 2010 kupitia kura ya maoni basi kikao hiki pengine kingelikuwa ni ndoto. Mimi nataka nikubaliane na wao kwa hilo, lakini vile vile tujue kwamba pamoja na yote haya ni sababu ni Mwenyezi Mungu alishapanga kwamba hili wakati wake ni huu wa kuwa jambo hili. Kwa hivyo, kuna zile sababu za kuzifanya lile jambo litekelezeke.

Mhe. Spika, hapa nitachukua nafasi hii kuwashukuru sana wazee wetu Mzee Hassan Nassor Moyo na mwenzake Marehemu Mhe. Mzee Shaabani Khamis Mlooo ambaye leo hii hayupo katika dunia hii lakini Mwenyezi Mungu atamfikishia kheri zake huko aliko amsamehe makosa yake yeye na sisi na waliotangulia kwa kujaalia kuwa wao ni chachu ya hili.

Mhe. Spika, pale walipolipeleka ikawa kama chumvi na ikakolea kwa hiyo nimshukuru sana pia Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad kuwa wao walilichukua suala hili na wakakubaliana na hatimaye ikapelekea Mhe. Abubakar Khamis Bakary kutuletea hoja binafsi katika Baraza na tukafikia kupata kura ya maoni. Namshukuru sana Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Kamati ya watu sita.

Mhe. Spika, pia nisiwe mwizi wa fadhila niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kukubali kuipitisha hoja ile na ikawa ni hoja ya Baraza ikapelekea kutufikishia kwa Wazanzibari. Napenda kuwapongeza sana kwa kuona haja ya kuleta mabadiliko katika nchi yetu na ili tuweze kuwa na amani na utulivu ambao wao ni miongoni mwa wanayoendeleza. Vile vile kuweza kufikia maendeleo ya kweli kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda tena nimshukuru sana Mhe. Ali Mzee Ali pamoja na Katibu wetu wa Baraza Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim kwa elimu kubwa ambayo walitupatia. Mimi nilikuwa naona labda masuala ya maridhiano yameanza pale alipoanzia tu Maalim Seif na Mhe. Rais Amani Abeid Karume, lakini kwa elimu ambayo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hiyo ametupatia kumbe hili si suala la leo na jana. Lakini ulikuwa wakati wake haujafika na ndio maana kuna waraka huu leo Wajumbe wote wa Baraza mmeupata wa Sheria ya Rais Nam. 6 ya 1964 ambayo imesainiwa na mwenyewe Mhe. Mzee Abeid Amani Karume unaosema kwamba ni Sheria ya Katiba inayotambua kuwepo kwa usawa, maridhiano na umoja kwa watu wa Zanzibar. Kwa hivyo, hili halikuwa jambo geni Mhe. Spika, lakini ilikuwa wakati wake muwafaka labda niseme hivyo ulikuwa haujafika.

Kwa hivyo, sheria hii ikajulikana kama ni Sheria ya Usawa wa Maridhiano na Umoja wa Watu wa Zanzibar ya Mwaka 1964. Sasa hapa nilikuwa napenda sana nikumbukie enzi zangu za ujanafunzi, wakati ule Mzee Abeid Amani Karume alipofariki basi kulikuwa na maneno yakizungumzwa. Maneno hayo nitapenda niyanukuu kwa ruhusa yako Mhe. Spika yalikuwa yanasema hivi:

“Mzee Abeid Amani Karume amekufa na amezikwa, lakini kilichokufa na kuzikwa ni kiwiliwili chake tu, busara, mawazo na fikra zake zipo na zitaendelea kudumishwa milele”.

Miongoni mwa haya ambayo tunatakiwa kuyadumisha milele ni waraka huu wa Sheria ya Raia ya Nam. 6 ya mwaka 1964 iliyoweka kinagaubaga kuainisha masuala haya ya maridhiano na umoja.

Lakini pia Mhe. Spika, madhumuni makuu ya mapinduzi kifungu cha pili cha sheria hiyo kinasema kwamba, “Madhumuni Makuu ya Mapinduzi ya Watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii na kisheria na mapungufu yote yaliyopita yaliyokuwa yanawagawa wananchi na makundi mbali mbali ya raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini, usaili wa mtu na madhumuni hawa ya Mapinduzi ni kukuza usawa wa maridhiano”. Ilikuwa inajirejea hii lakini ni kwa umuhimu wake. Sasa na mimi napenda sana kusema kwamba madhumuni haya bado yana nafasi ya kuendelezwa. Kwa hivyo, tunarudi pale pale kwamba yawepo na yaendeleo kudumishwa milele.

Mhe. Spika, hapa katika kifungu cha 3 kwa msingi huo kinasema hivyo. “Kwa msingi huo kila raia wa Zanzibar anatangazwa kuwa na haki sawa, fursa na hifadhi ya uraia wake kama vile ambavyo anatekeleza majukumu na wajibu wake wa kiraia. Hakuna hati, fursa au hifadhi inayoweza kufutwa kisheria kwa raia yeyote kwa kutumia vyombo vya dola au kwa kutumia hatua za mtu binafsi kwa sababu ya misingi au kisingizio cha ukabila, dini, jinsia au usaili wa uraia huyo.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa naomba sana kuiasa nafsi yangu na wale wote wote ambao watahusika kwa namna moja au nyengine ya kutenda haki au kutoa fursa au hifadhi kwa wananchi kulizingatia sana suala hili. Kwanza tutakuwa tunafanya lile ambalo tumelikusudia, lakini pili katika kuwaenzi

viongozi wetu kuanzia huyu Mhe. Rais wa kwanza na muasisi wa taifa hili Marehemu Mzee Abeid Amani Karume basi hiki ni kifungu ambacho kwa ujumla wetu na kila mwenye jukumu kwa namna yoyote katika sehemu yake tukifanyie kazi kama inavyopaswa.

Mhe. Spika, kuhusu mswada huu ambao uko mbele yetu na marekebisho yake, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini napenda nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati yangu ya Watu Sita chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Ali Mzee Ali kwa jinsi na namna tulivyoweza kufanya shughuli nzima ya uelimishaji. Lakini pia kwa namna ya pekee tuwashukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mhe. Haji Omar Kheir na kundi lake kwa kukaa na kutafakari kwa kina kuweza kutuletea leo kitu kilichokamilika hapa.

Mhe. Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie sheria hii tukishakupitisha tuweze kuifanyia kazi kama ambavyo tumekusudia. Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu atuelekeze kwenda katika njia ambazo ndizo zinazotakiwa kibinadamu na tuweze kupata mafanikio zaidi ya hapa tulipo na tuweze kupata maendeleo ya kweli na ya haraka katika nchi yetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba sana kukushukuru na ninaunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria kikao hiki cha Baraza ambacho tunatekeleza majukumu tuliyopewa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba vile vile nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji katika marekebisho haya ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Barazala Mapinduzi pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukaa pamoja na hatimaye leo hii tunazungumza masuala ambayo wao walikaa katika kufanya maridhiano katika vyama vyetu hivi vitukufu.

Mimi kwanza nianze na mchango wangu kwamba Zanzibar kama ilivyoelezwa hapa katika Katiba kuwa ni nchi. Ninakubaliana na hilo lakini vile vile Zanzibar ina historia yake. Mhe. Spika, Zanzibar ilianza kuwa na marekebisho ya utawala wake mara tu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na uongozi wa kwanza wa Zanzibar ndio ulioleta mabadiliko makubwa katika nchi hii ya kuwafanya wananchi wa Zanzibar kuwa wamoja bila ya kujali dini, itikadi na ukabila.

Mhe. Spika, mara baada ya Mapinduzi kama tunavyoelewa kwamba mapinduzi yoyote katika nchi zote duniani basi serikali inakuwa kali mno. Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar toka wakati wa Afro Shirazi baada ya kutawala, iliweza kufanya marekebisho yake kidogo kidogo na kuweza kuwarekebisha wananchi wake na kuwavuta karibu pengine hata wale waliokuwa hawaungi mkono Chama cha Afro Shirazi wakati huo.

Katika hili Mhe. Spika, nataka nitoe mfano mmoja mdogo, ilikuwa si rahisi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa Afro Shirazi kwamba mtu ambaye alikuwa chama chengine kuingia serikalini. Lakini kidogo kidogo serikali iliweza kuwavuta wale ambao walikuwa nje na kuwaingiza serikalini. Kwa hivyo, suala hili halikuanza leo kama tunavyoliona.

Mimi nakumbuka ilikuwa kiongozi katika tawi, yaani kama wewe ulikuwa ni mtu ambaye hukuwa katika Afro Shirazi asili uko chama chengine, basi uliweza kufukuzwa kwa wakati huo hata kama wewe ulikuwa ni kiongozi, ulifika wakati huo. Sasa haya ni mambo ambayo inafaa tuyaone katika historia ya nchi yetu.

Kwa sababu nakumbuka Mkoa wa Kaskazini pekee ndio Mkoa ambao ulikataa hili wazo la kwamba wale ambao walikuwa si wana Afro Shirazi kuwa katika uongozi kama wenyeviti na nafasi nyengine.

Kwa hivyo, pia ningependa niwapongeze sana watu wa Mkoa wa Kaskazini wakati ule nakumbuka Mwenyekiti wa Mkoa alikuwa ni Mzee Abdul Mahmoud Jecha. Yeye ndiye aliyeongoza hilo zoezi na kwa kweli tuliweza kukaa vizuri na kuanzia hapo nafikiri ndio ambapo wananchi wetu waliweza kujua kwamba nia na madhumuni ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuweka wananchi wote katika hadhi moja.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka kulizungumza kwanza niseme kwamba naunga mkono marekebisho haya ya Katiba na nina sababu mbili kuu. Kwanza naunga mkono nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ambaye nimechaguliwa pale kwa kura katika kipindi kilichopita, lakini vile vile Mhe. Spika, ni kwamba nikiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi vile vile nimekula kiapo kwamba nitahakikisha kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar katika shughuli zake zote za kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hivyo, kwa kuwa Rais ameamua hili pamoja na Katibu Mkuu wa *CUF* kwa maslahi ya taifa, basi moja kwa moja mimi naunga mkono hoja hii bila ya kinyume kwa asilimia mia moja.

Jengine ambalo ningetaka kulizungumza ni kwamba nataka niunge mkono ile hoja inayozungumzia kuwepo au kujulikana kwa Rais wa Zanzibar katika haya marekebisho ambayo yamefanywa kikatiba, kuwa Rais wa Zanzibar ataendelea kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Kwa hivyo, hii nayo Mhe. Spika, nataka niunge mkono.

Lakini jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba ile hoja iliyozungumzia kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hili Mhe. Spika, ningependa sana kwamba marekebisho haya nayaunga mkono na kuomba kuwa wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao wakakubaliana na sheria hii. Kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar ni Katiba zote ambazo ziko sawa. Jamhuri ya Muungano ipo kwa mujibu wa sheria na Katiba ya Zanzibar ipo kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, wenzetu vile vile wanatakiwa wahakikishe kwamba Katiba ya Zanzibar wanaiheshimu.

Mhe. Spika, anapotokea mtu au kiongozi fulani kutoka upande wa Jamhuri ya Muungano akakataa ile kauli tunayoiuzungumza sisi kwamba Zanzibar ni nchi, maana yake ni kuleta tofauti katika Jamhuri moja ya Muungano. Mimi naomba kuwe na maelekezo mazuri kama ambavyo amezungumza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake aliyoitoa. Nakumbuka siku ile tulikuwa tunakwenda Arusha baada ya mtafaruku mkubwa uliojitokeza kwamba Zanzibar si nchi au nchi.

Mhe. Spika, imesemwa wazi kwamba Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi, lakini pale tunapotoka nje ya Zanzibar basi Zanzibar inakuwa inabebwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nchi pale inajulikana ni Tanzania. Lakini ndani ya nchi zetu mbili basi Zanzibar ni nchi sawa na ile ya Tanganyika kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mimi kwa sababu sikuwa na maelezo mengi katika mswada huu lakini niliona sitotenda haki. Mimi mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani iwapo sitaunga mkono hoja hii ambayo iko mbele yetu na hasa baada ya wananchi wetu kupiga kura ya asilimia 66.4 na kukubali hoja hii. Kwa hivyo, kiufupi ni kwamba nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kutoa mawazo yangu kidogo katika mswada ambao uko mbele yetu.

Mhe. Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais. Nampongeza Mhe. Rais kwamba pamoja na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini pia kuondoa kero mbali mbali za wananchi na pia amekuwa akitekeleza yale ambayo yalikwishakubalika huko nyuma.

Mhe. Spika, waraka huu tuliopewa wa Sheria ya Rais Nam. 6 ya mwaka 1964, inatoa ufafanuzi wa haya ambayo leo tunayazungumza hapa. Kupitia kiti chako ninaomba sana Mheshimiwa waraka huu uandikwe kwenye magazeti ili wananchi wauone. Kwa wale wachache ambao wanasema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ama Rais kwamba tumeza nchi, basi waone kwamba sisi sio tuliouza nchi lakini haya ni maazimio tokea mapinduzi yaliyokuwa yamekusudiwa.

Sio haya tu Mhe. Spika, kwamba Mhe. Rais anatekeleza yale ambayo yalikubalika, hata tukiangalia nyumba za Michenzani kulikuwa na deni watu wakidai pale tuliziacha kwa miaka mingi lakini Mhe. Rais ameweza kusimamia na kuweza kulipa deni lile ambalo lilikuwa ikidaiwa serikali kwa miaka mingi. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa mambo mazuri sana ambayo ametufanyia katika nchi yetu.

Sasa wale wote kawaida binadamu wengine watakupenda na wengine hawatokupenda, sasa wale waliokuwa na roho za korosho kidogo naomba roho zao waziweke sawa.

La pili Mhe. Spika, nilikuwa nikiangalia ile asilimia 33 na kidogo walioyosema hapana. Mimi nilifanya *research* kidogo kwa nini waseme hapana? Nimegundua kwamba wamesema hapana wana wasi wasi na wasi wasi waliokuwa nao walihisi kwamba labda katika sheria hii neno Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar litafutwa. Hivyo na wao wakasema aah, hili haliwezekani ndio maana wakakataa.

Lakini bahati nzuri *concern* yao imeonekana na hakuna suala la kufutwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kifungu cha 26 Nam. 5 kinasema, “Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais” hii inaonesha dhahiri kwamba hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikufutwa.

Lakini wasi wasi wao wa pili wanasema, baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 wapinzani walikwenda kusini na kaskazini kuzuia misaada tusipate leo unawatia ndani ya serikali mambo yatakuwa vipi? Sasa nasema wasi wasi huo waondoe.

Tatu walikuwa wanasema, baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 kulikuwa na *sabotage* nyingi ndani ya serikali, leo wapinzani mnawaleta tena ndani ya serikali mnafikiria vipi? Sasa hizi *concern* zao zilikuwa ukizitizama zina mantiki, lakini hawakupata elimu ya kutosha ndio maana wakajenga hoja hizi na wakasema hapana. Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri hebu awatoe wasi wasi hawa 33 *point something* walioyosema hapana. Kwamba haya mambo ambayo wanafikiria hayapo. Sasa awatoe wasi wasi ili tutoke kwenye hiyo asilimia 33 walisema hapana na sisi 66.4, walioyosema ndio tuwe asilimia mia moja tunasema ndio. Hiyo inawezekana kwa kutumia haya haya marekebisho.

Kwa sababu kifungu cha 42 kinasema endapo Makamo wa Kwanza wa Rais au Mawaziri kutoka vyama vya upinzani watajiuzulu au wataacha kutekeleza kazi zao kwa zaidi ya siku saba. Sasa hapa imewapa na wao nafasi kuonekana kwamba ule wasi wasi waliokuwa nao na serikali imeona imeutia hapa. Hapa Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Waziri akija akijumuisha awatoe hofu na tutafika hiyo asilimia mia moja na haitokuwa tena asilimia 66.4.

La mwisho nataka nimpongeze sana Mhe. Ali Mzee Ali kwa kazi nzuri aliyoifanya. Ameelimisha vya kutosha na matunda ya elimu yake ndio tunayaona leo. Nilimwambia Mhe. Ali Mzee unafaa ulindwe kidogo je, mimi niwe *bodyguard* wako? Akaniambia aah! Mhe. Spika, atanitafutia *bodyguard*.

Mhe. Spika, Mswada ni mzuri, marekebisho mazuri ni kuleta umoja, mshikamano na maendeleo endelevu katika nchi hii. Mimi kwa niaba ya Jimbo langu la Ikulu naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naomba nianze kuchangia Mswada huu wa Mabadiliko ya Katiba kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wetu Dr. Amani Abeid Karume kwa juhudi zake za kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Zanzibar na kutufikisha hapa ambapo tupo leo.

Tatu naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wa pande zote mbili wa Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi *CUF* kwa mshikamano mkubwa waliouonesha kwa kipindi takriban cha mwaka mmoja sasa.

Lakini nne, niwashukuru na kuwapongeza sana watendaji wetu wa Baraza chini ya Katibu kwa jitihada zao ambazo zimewezesha Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa umoja wao kuja kulionja Baraza hili au jengo hili. Tunajua kwamba ilikuwa ndio kiu yetu kuwa tuliwahi na wamejitahidi tumewahi.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri mimi nilipata fursa kubwa ya kuupitia mswada huu au maandalizi yake kama walivyo mawaziri wengine, tuliujadili nafikiri siku tatu kifungu kwa kifungu na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii lazima tumshukuru Mwanasheria Mkuu alitusaidia sana pamoja na hali yake ya kiafya, lakini alishiriki kikamilifu na tulikuwa tukiulizana kwamba kumbe kichwa chake kinafanya kazi vizuri sana na alitusaidia sana.

Mhe. Spika, mchakato huu ulikuwa mrefu sana na kwa hatua tuliyofikia sasa hivi ni hatua ya mwisho. Kwa sababu kama walivyozungumza wengine mchakato huu ulianza kwenye vyama, Chama cha Mapinduzi, chama tawala na Chama cha Upinzani cha *CUF*. Kulikuwa na kamati za wajumbe, kazi hiyo waliifanya hatua baada ya hatua. Baada ya kumalizika zoezi ndani ya chama hatua muhimu nyengine ilikuja katika Baraza la Wawakilishi na sisi Waheshimiwa Wawakilishi kwa kutumia Katiba ya Zanzibar hii ambayo tunairekebisha, kifungu cha 9 tukasema kwamba maamuzi makubwa ya nchi lazima wananchi wenyewe washirikishwe kufanya uamuzi.

Sasa wananchi nao kulikuwa na wengine wana hofu kwamba serikali haitotekeleza haya maamuzi, lakini serikali ikafanya marekebisha katika sheria ya kura za maoni nayo ikaelezwa kwamba uamuzi wowote utakaotolewa utaheshimiwa. Bahati nzuri wengi wakasema ndio, nafikiri ni asilimia 66.4. Kwa hivyo, uamuzi huu umeheshimiwa na ndio maana leo tumekuja hapa kurekebisha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, demokrasia ina gharama zake na faida kwamba suala lolote ambalo linapelekwa kwa wengi kufanyiwa uamuzi na likifanyiwa uamuzi basi lazima liheshimiwe. Kwa sababu hiyo basi, sisi Waheshimiwa na wananchi wote wajibu wetu sasa ni kuangalia tunaelekea wapi bila ya kuangalia tulitokea wapi. Sasa ni muhimu kushikamana na kushirikiana.

Mhe. Spika, siku moja niliangalia *film* ya Afrika ya Kusini wanaaita *screen box*. Mchezo huo ulikuwa ukichezwa na Makaburu wenyewe wakati huo na ulikuwa na washabiki wengi weupe, weusi walikuwa si washabiki wa mchezo ule na waliuchukia kwa sababu ya ubaguzi wa rangi. Lakini Rais wao wa kwanza Mhe. Nelson Mandela baada ya kupata Urais akaamua kuutumia mchezo ule ule kuirekebisha Afrika ya Kusini, kuileta katika umoja na mshikamano. Katika hatua za kwanza alipata tabu kubwa sana, kwa sababu wale weupe wenye ule mchezo walikuwa wanawaogopa Waafrika au wanawanyanyapaa.

Katika mchezo ule kulikuwa kuna mchazaji mmoja Muafrika ambaye ni mchezaji mzuri, yeye akirudi kwa ndugu zake anaonekana kama msaliti. Kwa hivyo, ilikuwa ni kazi kubwa sana, hata wale wasaidizi wa Mandela alivyoanza kuwaita wale wachezaji alimwita kapteni wa ile timu basi wao walikuwa wana hofu na kuona kama kiongozi wao kachanganyikiwa. Lakini kwa bahati nzuri kutokana na busara za kiongozi aliendelea taratibu na hatimaye wakaanza kupata ushindi katika mataifa mbali mbali.

Kwenye mechi ya *final* ambayo na yeye mwenyewe alihudhuria kiwanjani, nje ya uwanja kulikuwa na askari wa kikaburu wanalinda. Sasa wakati mchezo unaendelea na kule unaoneshwa kwenye televisheni kwa nje, wale askari wakatoka kwenye gari wakawa wanaangalia. Walikuja watoto wa Kiafrika nafikiri wawili wakawa na wao wanafuatilia ule mchezo, lakini wakawa wanawafukuza pale kwenye gari lao wale askari Polisi, kila wakikaribia wanawafukuza. Kila muda wa mchezo ukienda na yale matokeo ya mchezo yalivyokuwa yakitokea kule kiwanjani wale waskari wakasahau wale watoto

kuwafukuza na wakawa wanasogea zaidi kufuatilia, hatimaye dakika ya mwisho walishinda Waafrika ya Kusini. Basi wale askari wa Kikaburu waliokuwa wanalinda ikabidi wawabebe wale vijana wa Kiafrika na kukumbatiana kwamba ule ushindi ulikuwa wao wote.

Sasa hii ilitokana na nini? Ilitokana na kwamba uadilifu wa kiongozi na ustahamilivu wake, alipitia katika mawimbi magumu sana na kuweza kuwaunganisha watu wa Afrika ya Kusini.

Kwa hivyo, na sisi Zanzibar Rais wetu kafanya kazi kama hiyo, katuunganisha sote sasa hivi ni wamoja, hakuna wasi wasi hata kidogo. Niishukuru kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali imefanya kazi nzuri sana. Asubuhi nilimwambia Mhe. Ali Mzee, kwa nini wakati mnaanza ule operesheni ya kutoa elimu hamkuzisambaza kwa waheshimiwa wote wakapita nazo wakazizungumza hizi kwa sababu hii ni kazi kubwa na nzuri.

Lakini kwa ujumla kazi yote imekwenda vizuri na sisi tuna imani kwamba jambo hili litatuunganisha zaidi Wazanzibari. Ukichukulia kijumla jumla watu wawili wakikutana mtaani basi wanazungumza vizuri zaidi, yaani huwezi kuona tofauti ya chama na chama, hata yule ambaye kapiga kura ya hapana, lakini akikutana na mwenzake mwengine anataka umoja. Kwa sababu siamini kama kuna mtu ambaye katika roho yake hataki kushirikiana na mtu, kuelewana na mtu na hataki umoja na mtu basi mtu huyo anakuwa ni wa ajabu sana.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuona kwamba tumepiga hatua. Katika hili sote kwa umoja wetu Wazanzibari aliyepiga ndio na aliyepiga hapana, nafikiri sasa ni wakati muwafaka kuungana na kwenda mbele katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, lazima tuondokane na kufikiria kwamba kila jambo ni siasa, kwamba maisha ya binadamu yanatawaliwa na siasa. Mimi naamini kwamba siasa ni muhimu sana na mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, lakini lazima siasa isaidie kupeleka mbele maendeleo ya mtu na siasa itumike katika kuleta umoja miongoni mwa watu, siasa isiwabague watu kuwafanya kwamba wawe mbali mbali na tunaweza.

Tulipokwenda kwenye mchakato wa kugombea Urais, wengi wa mawaziri na wajumbe wa kawaida wa CCM walikuwa ni wa *NEC*. Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto bajeti yake ilikuwa inafuatia siku ya pili ile, lakini sisi wengine hatukuwahi kurudi Barazani, lakini aliporudi yeye bajeti yake haikupata shida na nikamwambia Mheshimiwa laiti ingekuwa bajeti hii miaka miwili nyuma kwa makusudi ingelisimamishwa na isingepita kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini kwa nini wakaona ina mantiki ipitishwe? Kwa sababu sasa hivi mtu anakukosoa kwa jambo ulilolikosa, anakusaidia kukuongoza kwa jambo ambalo umelikosea.

Kuna kipindi ilikuwa hata ukifanya vyema unajua hasa mimi nikifika Barazani asubuhi hii hata kama nimemjengea barabara ya dhahabu lakini lazima atanigonga kwa sababu ilikuwa ndio utamaduni huo. Lakini sasa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii akipeleka dawa itasemwa kaleta dawa, hakuleta dawa itasemwa bado Mheshimiwa hujaleta dawa na itatumika lugha ya kusaidiwa sio lugha ya kukomoa.

Sasa hapa tulipofikia mimi nafikiri ni sehemu nzuri sana na hii sio kwa waheshimiwa tu, hata kwako Mhe. Spika, itakusaidia, makatibu wa Baraza. Kwa sababu kuna kipindi ilikuwa ukienda ofisini kwa Katibu Mtu unamchungulia anaingia nani kwa Katibu umngoje atoke ndio uingie wewe lakini sasa hivi nina hakika kwamba wanaweza kuingia hata watu wa vyama mbali mbali kwa wakati mmoja na wakafanya kazi vizuri. Sasa Mhe. Spika, mimi naomba nimalizie, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi labda atazungumza jioni.

Mimi niseme tu kwamba jambo hili linatuwekea historia sana Zanzibar. Wale wanaopata bahati ya kusafiri wakisafiri wanaulizwa huko nje vipi mnaendeleaje? Hali yenu ikoje sasa? basi wale wanaoulizwa kwa sababu hali hii sasa unapata kujibu kuwa hali nzuri na tunaendelea vizuri na nchi yetu imetulia na kweli imetulia. Hatukuwahi kupongezwa hivyo hapo zamani na Umoja wa Mataifa,

halikuwahi kutokezea hilo, lakini sasa linatokezea. Kwa sababu ni jambo zuri litakuwa letu sote hilo, lingelikuwa baya lingekuwa ni la Zanzibar peke yake kwamba huko hakwendeki, lakini sasa kwa sababu jambo jema basi tukubali kwamba lote la Tanzania kwa sababu na wenzetu walisaidia kufikia hatua hii. Kwa hivyo, tunahisi kuwa ni jambo zuri.

Sasa madhali jambo zuri tunapongezwa, isitokezee tena jambo hili kutokezea mmoja akataka kuja kuliharibu kwa maslahi yake binafsi. Limeshaka vizuri, makosa ya kibinadamu yapo lakini tusihukumiane tukasema yule alikuwa hivi, sasa twende mbele tuangalie tunafanya nini mipango yetu ya maendeleo. Mimi nina hakika kwamba kwa umoja huu tulionao tutafika malengo yetu tuliyojiwekea.

La mwisho niseme kwamba, tujitahidi basi tufanye kazi kwa bidii kwa kushirikiana, kwa kuipenda nchi yetu ili tuweze kufanikiwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi. Namuomba radhi Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi nimemtaja kwamba achangie baada ya Mheshimiwa aliyemaliza, lakini muda kwa wakati huu hauturuhusu hivyo nafasi ipo kwa jioni kuendelea na mswada huu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa katika kuongoza kikao hiki na sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni ambapo watendaji pamoja na mafundi watarekebisha ile hali iliyokuwa haikuridhisha viti vyetu humu ndani ili tukiingia jioni mambo yende vizuri zaidi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa wasaa huu wa nafasi ya mwanzo kabisa jioni hii ya leo kuchangia hotuba ya mswada wa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mswada wa Sheria ya Marekebisha ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, kwa kweli wenzetu wengi sana wametoa sifa kemkem, wamechangia ipasavyo na mimi niungane mkono nao na sitokuwa na mengi, lakini nidonoe tu kidogo hapa na pale.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba niwashukuru sana na mimi wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kunipa fursa ya kuongoza kura ya maoni katika jimbo langu na wakinipa imani kwamba *inshaallah* tamaa kubwa ya kurudi Barazani bado mchakato haujakamilika.

Mhe. Spika, kazi aliyofanya Mhe. Waziri ya kutuwasilishia mswada huu kwa kweli ni kubwa na kama walivyosema wenzangu kwamba hatuna budi tuwashukuru wao katika Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora na hasa Mwanasheria Mkuu kwa kututengenezea na kuyafanya mambo yawe rahisi kabisa kwa mjadala wetu huu wa leo.

Mhe. Spika, ushindi tuliupata wa asilimia 66.4 ni wa kujivunia kabisa. Niseme kwa nini ni wa kujivunia? Mhe. Spika, najaribu kutazama nchi za wenzetu jirani Kenya zoezi kama hili siku chache zilizopita na wao nimepata salamu kwamba ushindi waliupata ni wa asilimia 67. Sasa wao walikuwa mambo yao takriban yanalingana na sisi, lakini wao walikuwa wanasema Katiba mpya au ya zamani? Wakaamua mpya. Yaani kwa kweli yamefanywa marekebisha.

Sasa sisi tulikuwa na kura yetu ile tukasema aaa tunataka Serikali ya Umoja wa Kitaifa au la? Baada ya kukubali kule sasa Katiba wenzetu wa wizara wamechukua jukumu wameirekebisha na wameturahisishia kazi kubwa kabisa. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba msingi wa yote haya ni nini? Msingi wa yote haya ni umoja, amani, utulivu na mshikamano.

Mhe. Spika, wenzetu Kenya wameona wenyewe nini kilichowakuta ndio maana wakajitokeza kwa wingi kabisa. Mimi nilikuwa nikifuatilia sana yale matangazo yao kwa *channel* yao ile kwa kweli inafurahisha sana jinsi walivyojitokeza. Ninaamini hata sisi watu wamejitokeza kwa wingi lakini kulikuwa na *element* kidogo ya watu kutokufahamu.

Mhe. Spika, nitatoa mfano jimboni kwangu watu wengi sana waliniuliza Mwakilishi twende tusende? Nikawaambia kwa nini msende? Kura hii ni yenu, ni haki yenu na mmepewa fursa ya kuamua mustakbali wa nchi yetu. Mustakbali wenyewe tunataka tujue twende vipi serikali yetu. Kwa hiyo, mna wajibu wa kila busara kwenda. Haya tukishakwenda tupige ndio au hapana. Nikawaambia kwa nini mpige hapana. Aaa maana yake tunapotoshwa huko serikali ya mseto, hatusikilizani, tunaiuza nchi. Nikawaambia kakwambieni nani?

Kwa hiyo Mhe. Spika, nilifanya kazi ya ziada na nilipokuwa nazungumza nao walisema duh, tulikuwa hatuna habari hizi sisi tunasikia mseto tu na sisi tunafuata. Nikawaambia si mseto bwana, ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kuna tafauti na huu mseto mnaosema. Nikachukua jukumu Mhe. Spika, nikawafahamisha lakini kama walivyosema wenzangu kidogo iliangukia siku mbaya, ikaangukia siku ya mkeshwa wa hatima yetu wengine humu ndani. Sasa kidogo tulijitahidi kwa ukomo wetu na tumefikia tulipofika.

Sasa Mhe. Spika, haidhuru tumelishavuka hili lakini mimi naomba sana bado ile kazi waliyokuwa nayo kamati inayoongozwa na Profesa Ali Mzee Ali iendelee na kazi yake. Zaidi kwenye televisheni tumeiona na kama alivyosema Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry kwamba wenye *cable television* wameona, lakini kwangu Dimani *cable television* haijafika. Sasa ningeomba mimi niko tayari nitawaongoza tufanye vikao maalum hasa jimboni kwangu wakawafahamisha watu vizuri wafahamu na ninaamini nilivyoanza mimi wataimaliza. Mhe. Spika, ningeomba sana na majimbo mengine.

Haidhuru kazi nasema tumeshaifanya lakini ile watu wafahamu iwaingie hasa kwa nini hili jambo serikali na chama chetu tawala na chama cha CUF tumekubaliana tufanye hivi. Imebidi tuwafahamisha kwa dakika chache wamekubali. Sasa naomba hii taaluma Mhe. Spika, kupitia kamati yako iendelee na tuwafuate hasa watu. Kwa sababu hii itatusaidia kutilia nguvu zaidi hii hoja yetu ya umoja na mshikamano.

Mhe. Spika, Zanzibar tunafanya mambo mengi mazuri na ya kupigiwa mfano. Wakati mwengine labda tunalaumiana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu hatuoni ule upeo wa mambo yetu. Lakini mambo yetu ninaamini kabisa tunakaa tunapanga tunatekeleza kwa busara na hekima kubwa na mifano iko hai kabisa.

Mhe. Spika, asubuhi niliangalia juu kule mbali ya wenyeji niliona wageni tu walikuwa wengi mno labda mchana sasa hivi wamepungua. Sasa nikajiuliza hawa wana mambo gani kwa Zanzibar, wanaitakia nini Zanzibar hawatuachii wenyewe. Lakini kumbe Zanzibar ni kisiwa cha amani, huo utalii, biashara, mambo yote mazuri, *honeymoon* wanayokuja maharusi yanafanyika pakiwa na amani na utulivu. Sasa wao nafikiri wanatutakia mema na ninasema zaidi ya tunavyotakiwa sisi. Kwa hiyo Mhe. Spika, si ajabu sifa tunazozipata kutoka *EU*, *UN* yenyewe, *ADB*, *World Bank* na wengineo ni za kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, hivi karibuni vikundi vyote vya ujumbe vinavyokuja kututembelea hapa na hasa kumuona Mhe. Rais, basi salamu ya kwanza ni kutupongeza. Wanatupongeza kwa sababu ile wenyewe kukubaliana tukaridhiana mpaka tukafikia hatua ya kufanya kura ya maoni ya kuipitisha na hatimaye leo tunafanya marekebisha ya Katiba. Huu mtiririko mzima Mhe. Spika, tulivyojipanga na tunavyoutekeleza bila ya matatizo yoyote ni suala la kupigiwa mfano sana.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Ali Mzee Ali baada ya Mhe. Rais kumpokea Mhe. Balozi Asha-Rose Migiro kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, baada ya kumpa Mhe. Rais salamu zake maalum Mhe. Ali Mzee yeye mwenyewe alisema ni rafiki yake Asha-Rose na mimi nakubali ni rafiki yake. Lakini ninaamini kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa ile Kamati alimuona Mhe. Asha-Rose na akampa hizo salamu maalum na mimi nilimtania Mhe. Ali Mzee nikamwambia Mhe. Ali ungefanya mapicha yale mazito mazito ingekuwa *very historic* na ninaamini zile picha kazipiga. Kwa hiyo Mhe. Spika, nakuomba sana kupitia.

Juzi nilimzungumza kiutani lakini mbele yako leo namuomba tena Mhe. Ali Mzee Ali zile picha alizopokea hati Mhe. Ali Mzee za pongezi na sifa zile, hizi kwa niaba yetu uzipate Mhe. Spika, hizi ziwe kumbukumbu kwetu Barazani na kwengineko. Hii sisi tunaiona ni kazi ndogo lakini si kazi ndogo hata kidogo na ya kupigiwa mfano, wenzetu wanahangaika kuitafuta hali kama hii. Kwa hiyo Mhe. Spika, mimi naomba kusisitiza tu kwamba kwa kweli tusingoje kusifiwa tuanze wenyewe na tupongezane kazi tuliyoifanya ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hii kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali kama tulivyokubaliana tuiite kwa kweli mimi niseme ni kamati uliyoiteua sijui kwa vigezo gani lakini kwa kweli ilitimia. Kwa sababu mbali ya kwamba pande zote mbili lakini ukachagua watu wenye busara, wenye hekima, wenye kujua Zanzibar na wenye falsafa. Mhe. Sli Mzee tunapomsifia sifa hizi tunaomba azipokee kwa undani kabisa. Yeye alinitania akanambia aaa Dk. Mwinyihaji wewe ndio ulikuwa wa kwanza kunipa cheo cha uprofesa Pemba tokea kikao cha mwanzo. Ulikuwa unanitania, ulikuwa unanidhihaki? Nikamwambia Mhe. Ali upeo wako niliiona mapema sana mimi na ile falsafa yako ni ya hali ya juu kabisa. Mimi nikamshauri hebu nakuomba ujiunge na *Open University* uchukue *PhD*. Kwa sababu ninaamini tutakosa mambo mengi sana ambayo unayo kichwani tu. Sasa ni jambo jema sana mtu kama huyu niseme ni hazina.

Mhe. Spika, mimi na Mhe. Ali Juma Shamuhuna ni watu wa Wizara ya Kilimo tulikuwa tunamwita Bingwa Mzee Ghassany. Bingwa yule ni bingwa kweli wa kilimo maana yake ni *dictionary*, wewe unachomtaja tu anakijua kwa uzoefu wake na mambo yake. Sasa mimi niungane na wenzangu kwa kumpa sifa kemkem Mhe. Ali Mzee Ali na bado tunamhitajia tuwe nae atuongoze atushauri.

Bahati nzuri Mhe. Spika, zile picha nilizosema Mhe. Ali Mzee Ali kaniletea ninazo hizi hapa na kwa kweli ndio anakabidhiwa hiyo shukurani hapa na Mhe. Asha-Rose Migiro. Hii picha ni *very historic* naomba Mhe. Ali hizi uzipitishie watu wote wazione na picha moja kapiga na kamati yake hapa. Kwa kweli ningepomba sana hii tuinunue sote, mimi mmoja nitakuwa tayari kuinunua niwe nayo tuitie fremu hasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nafikiri mimi mengi sina isipokuwa naomba kusisitiza moja tu. Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali asubuhi alizungumza kwamba yeyote atakayetusali katika suala hili na atakayewasaliti viongozi wetu basi huyo tumuandame ipasavyo. Mhe. Spika, hili na mimi nalisisitiza ni suala muhimu maana yake vikao vyetu vipo, kama mtu kidogo haridhiki na mambo basi aseme kwenye vikao. Lakini kukaa nje tena akanung'unika iwe hivi, iwe hivi, nafikiri hivyo sivyoy. Kwa hiyo, hili ni suala letu tulilinde, tuliendeleze kwa faida ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Mswada huu wa Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea nampongeza Mhe. Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ya kutayarisha mswada huu na hatimaye kuuwasilisha katika Baraza lako tukufu.

Pia nichukue nfasi hii kuungana na Waheshimiwa Wajumbe

Mhe. Spika, kabla sijaendelea nampongeza Mhe. Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ya kutayarisha mswada huu na hatimaye kuuwasilisha katika Baraza lako tukufu.

Pia nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waliotangulia kwa michango yao mizuri. Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kupitia Baraza lako tukufu kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Shariff Hamad kwa mazungumzo yao ya maridhiano yaliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2009. Tunayapongeza maridhiano hayo kwa sababu ni hatua moja kubwa sana ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea nisije nikasahau lakini maamuzi itakuwa kiti chako ilivyokuwa hili ni Baraza letu la mwisho kwa awamu hii, basi ningeliomba kwamba zikapigwa picha za ukumbusho kwa watoto wetu na vizazi vyetu vijavyo na vile vile kumbukumbu kwa Mabaraza mapya yajayo.

Mhe. Spika, nawapongeza wananchi kwa kutumia uhuru wao katika kupiga kura ya maoni kufikia asilimia 66.4 kama ilivyoelezwa jambo ambalo lilifanyika tarehe 31 Julai mwaka huu.

Mhe. Spika, suala hili kutokana na umuhimu wake nashauri vyombo vyetu vya habari TV na hata ikiwezekana zifanywe semina mbali mbali Tume yetu ya Uchaguzi na sisi wenyewe viongozi wawakilishi tuendeleo kuwaelimisha wananchi wetu kutokana na umuhimu wa jambo hili. Ni jambo muhimu sana na la kihistoria katika nchi yetu hii kwa hivyo tulipe kila uzito. Yaani nakusudia kusema kwamba wananchi wetu waelimishwe kwa kiwango kikubwa sana waweze kufahamu umuhimu wa suala hili, ili ile asilimia iliyobakia nao wawe pamoja washirikiane na wenzao wale asilimia 66.4 kwa ujumla wawe asilimia yote 100 tuwe suala hili tumelifahamu vizuri na tuliunge mkono.

Aidha, nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwa kulijadili suala hili katika kikao kilichopita cha Baraza letu la kulipendekeza kwamba ipigwe kura ya maoni ambayo ni moja katika hatua kubwa sana tuliyochukua Baraza letu lililopita na ni hatua ya kihistoria. Hivi leo kwa mara nyengine tena tutakutana hapa kumaliza kazi iliyobakia kuweza kupitisha sheria hii ambayo ninaamini wajumbe wote tutakuwa pamoja katika kuiunga mkono sheria hii, ili iweze kufanyiwa kazi na lile lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa usimamizi wao na ufuatiliaji wa upigaji wa kura ya maoni kwa mafanikio makubwa sana. Naiomba Tume ya Uchaguzi isichoke. Tutakuwa na uchaguzi katika mwezi wa Oktoba tukijaaliwa, basi pia tunaomba wasimamie na watekeleze kwa mafanikio makubwa sana katika uchaguzi wetu wa mwezi wa Oktoba.

Mhe. Spika, nisiwe mwizi wa fadhila kumpongeza Mhe. Ali Mzee Ali kwa kufanikisha vizuri sana majukumu yao waliyopewa. Tunawatakia kila la kheri na mafanikio mema.

Mhe. Spika, jengine ninaloliomba ambalo kwa kweli nimeshalisema kwamba kupendekeza au kushauri sheria hii tuliyonayo. Vile vile na hii sheria ambayo wajumbe sote tumepewa Sheria ya Rais Nam. 6/1964 inayohusika na Sheria ya Katiba inayotambua kuwepo kwa Usawa, Maridhiano na Umoja wa Watu wa Zanzibar. Mhe. Spika, vitu viwili hivi ni muhimu sana. Kwa hivyo, ipo haja wananchi waelimishwe kwa sababu hii ni mwaka 1964 ni watu wachache sana ambao wanaijua. Mhe. Spika, ningeliomba hasa vyombo vya habari kwa makusudi wakafanya vipindi vya kuelimisha wananchi warka huu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi sitokuwa na mengi kwa sababu mengi sana yameshasemwa na wenzangu waliotangulia. Isipokuwa nichukue nafasi hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu Iddi Pandu Hassan tulikuwa nae katika Baraza kwa muda wa siku nne juu ya hali yake kuwa si nzuri, lakini kwa kweli aliamua na muda wote huo tangu asubuhi tunaanza mpaka saa kumi yuko pamoja na sisi. Isitoshe muda waliopewa kukamilisha sheria hii kuiweka katika *format* hii tuliyopewa haikuwa rahisi. Kwa hivyo, walifanya kazi ya ziada hata

tukaweza kuipata sisi wajumbe. Tunampongeza sana Mhe. Iddi na tunamtakia kila la kheri Mwenyezi Mungu ampe afya njema *inshaallah*.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza naomba umoja na mshikamano wa dhati kabisa baina yetu kwa ajili ya kuendeleza na kudumisha amani na maendeleo nchini kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, mwisho kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi siku ya leo kubwa adhimu ya kulionja hili Baraza na nikaweza kutoa mchango wangu mdogo kwenye marekebisho ya Katiba.

Mhe. Spika, furaha yangu nataka kusema inaweza kunichania nguo kwa sababu hili jambo tulikuwa tunalitifuta siku nyingi lakini lilikuwa kidogo liko mbali. Lakini leo *Alhamdulillah Rabil Alamiyn* Wazanzibari tumekuwa kitu kimoja kama asili yetu tunakotoka. Wazanzibari zamani tulikuwa baba mmoja mama mmoja, lakini kitu kidogo tu kikatuparaganya kikatutenganisha tukawa hatusemani, hatuchekani, hatuambizani wala hatuendeani. Lakini leo umoja ule kuwa umerudi kwa salama na amani hakukwaruza mtu, hakuchapwa mtu, kila mtu kwa hiari yake, kwa umoja wetu Mwenyezi Mungu katuelekeza tumerudia pale pale tulipotoka zamani sana na wazee wetu tuliokuwa nao mwanzo walivyotuelekeza.

Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kutuongoza vizuri kwenye Baraza hili hata tukafikia hili jambo kwenye muafaka.

Lakini pia nisiache kumshukuru Mhe. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Shariff Hamad. Hawa ndio Mwenyezi Mungu aliwajaalia wakaleta hiyo fikra baada ya kuongozwa na Mhe. Hassan Nassor Moyo kupewa shauri. Mhe. Spika, kweli Waswahili wanasema “Iso kongwe haivushi”. Lakini Mwenyezi Mungu alituletea hiyo kongwe ikawaelekeza watoto wake na wao wakakubali wakakaa pamoja baadae kututeremshia na sisi wenzao.

Sisi tulikaa Barazani kule kwa zamani kidogo leo tuko kwenye Baraza jipya kwenye Kasri la Mwinyi Fuad *Alhamdulillah*. Tulivyokaa pale tulikaa kwa umoja wetu tukafikiri tukasahau mambo yetu yote yaliyokuwepo nyuma tukayaacha yakakaa pembeni, tukaufikiria umoja wetu na udugu wetu na tukakubaliana tukawapelekea wananchi waliamue hili na wameliamua na *Alhamdulillah* tumepata asilimia 66.4. Ni asilimia kubwa na ambayo inatuwezesha kufanya kazi bila wasi wasi.

Mhe. Spika, asilimia 66.4 si Wazanzibari kidogo waliosema ndio, ni wengi wa kutosha. *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu atawajaalia na hao waliobakia watasema na roho zao na ninajua kwa sababu walikuwa hawajafahamu nini ndio maana walitia hapana. Lakini wakielimishwa watajua nini kusudio la sisi wenzao tulisema ndio.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Mzee Ali na kamati yake wamefanya kazi kubwa sana na tuna haki ya kuwampongeza na hata kuwapatia tunza kwa kazi nzuri waliyoifanya wakishirikiana na Katibu wetu wa Baraza. Kweli Katibu wetu ni Mwanasheria na kakutana na wanasheria wenziwe wakaifanya kazi vizuri.

Lakini mimi kidogo nitakuwa na ushauri hili si jambo baya tukawa tunalifanya kwa vitu vyengine yaani kuelimisha, elimu ni kitu muhimu. Kesho kutwa tarehe 31 Oktoba tuna uchaguzi wenzangu, sio sote tunaofahamu nini maana ya uchaguzi wala nini maana ya kupiga kura. Tunahitaji mafunzo kama yale yaliyokuwa yametolewa yatolewe kwa kila nyanja kuanzia chini mpaka kwenda juu tujue tunakwenda kufanya nini tarehe 31, ili tuweze kuchagua serikali ambayo itafanya kazi zake kwa umoja, amani na utulivu. Tusrudie tena kule nyuma na Mwenyezi Mungu hatoturudisha tena. Tukipata walimu wakatusomesha *civic education* tukajua nini tunakwenda kufanya, basi nafikiri

tutapata umoja na nguvu nyingi sana kuliko kitu chengine. Elimu ni kitu muhimu siku zote hatuomeshani sasa tusomeshane.

Mhe. Spika, tuone mfano mmoja tu kwamba Kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali ilisomesha na ikafundisha na wengine tukasaidia tukapita tukiwaelimisha watu mpaka wakatufahamu tunasema nini na wakatupigia kura ya ndio. Kwa hivyo na mengine pia yanahitaji elimu, tusomeshwe na tufundishwe ili tuweze kufanya kazi zetu na udugu wetu uendelee vizuri katika nchi hii. Hatupendi kuwaona watu ambao hawashirikiani, tunapenda haya mashirikiano. Itoni raha tuliyokuwanayo sasa hivi hapa kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi kwenye miaka miwili ya mwanzo ile tulikuwa tunaparana tu, tunawacha kazi ya wananchi walivyotutuma tunafanya mengine. Lakini tizama sasa hivi tulivyo, kila kitu chetu tunafanya kwa pamoja, kwa ridhaa, kwa furaha na kwa kicheko. Mwenyezi Mungu pale anapatia baraka mahala kama pale. Lakini leo tukiwa tunaparana hakuna kitu kitakachokwenda humu, na ikiwa sisi viongozi hatutaki basi na wananchi huko nyuma wanatutizama sisi viongozi. Kwa hivyo, madamu sisi viongozi tumeshakubaliana na tumeshakaa pahala pamoja, wacha tukae kila mtu na chama chake lakini tushirikiane katika kuwaendesha wenzetu kwa vizuri.

Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu atatupa moyo, atatusaidia tutaweza kufanyakazi zetu kwa pamoja na kuwaelimisha watu wetu kwa sababu sisi sote ni ndugu, hakun Upemba wala hakuna Uunguja sote ni ndugu ambao tumezaana. Kila mmoja hapa kaolewa na Mpemba kaowa Mpemba au kaolewa na mtu wa Unguja au kaowa mtu wa Unguja sote ni kitu kimoja. Kwa hivyo, tuendeleze umoja wetu kama Mwenyezi Mungu alivyotuumba, kwa sababu tuliumbwa hivi hivi, kila mtu hajui tulianza lini.

Mhe. Spika, mimi nawaomba wenzangu sisi viongozi ndio wenye mambo yote, tuwacheni mambo yetu tukae na watu wetu, tuwaelimishe vizuri na sisi tuelimike ili tuweze kufanya kazi zetu kwa pamoja na umoja wetu na ile serikali yetu ya kitaifa ipate kufanyakazi vizuri na kwa nguvu. Tuisikilize maneno ya mtu, isipokuwa tuambizane tu, mtu anapokosa basi arekebishwe tu ndio tutakapoweza kwenda. Lakini ikiwa tutakaa kitako tuparane yatakuwa mambo hayaendi.

Mhe. Spika, kwa kweli maneno mengi hapa yameshasemwa, leo tunapongezana tu. Kila mmoja anampongeza mwenziwe na tumeshapongezana sana. Kwa hivyo na mimi nimetoa mchango wangu, maana yake nimeonja Baraza leo. Nimetoa mchango wangu ili na mimi nipongeze haya mambo yalivyokwenda vizuri na *Inshaallah* hapa palipobakia tutapamaliza vizuri sana na watakaojaaliwa kuingia katika madaraka na serikali basi wateendesha serikali *Inshaallah* vizuri kwa umoja, amani na udugu, ahsante sana.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kutupa afya tukaweza kuhudhuria leo katika kikao hiki adhimu, kikao cha historia katika Baraza letu hili jipya Mhe. Spika.

Kwanza Mhe. Spika, nataka nianze kwa kuunga mkono hoja, naunga mkono hoja Mhe. Spika, kwa niaba yangu mia kwa mia na kwa niaba ya wanawake walionileta hapa, lakini pia wanawake wote wa Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, ni lazima niunge mkono hoja hii kama mwanamke, kwa sababu sisi wanawake wa Zanzibar Mhe. Spika, ndio ambao tumeshuhudia kufeli kwa siasa zetu za Zanzibar. Leo tukifikia hatua kama hii basi ni lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu na ni lazima tuunge mkono.

Mhe. Spika, la pili nataka niwapongeze viongozi wetu kwa dhati kabisa. Kwa kweli wanastahiki kuwapongeza, kwa sababu wao ndio chanzo cha sisi leo kutufikisha hapa. Yale wanayosema watu kwamba dereva mzuri gari haiendi mrama, ni kweli Mhe. Spika, viongozi wetu wamekuwa ni madereva wazuri na ninaamini gari yetu hii haitakwenda mrama. Kwa haya ambayo Mhe. Spika, naamini tutakwenda au tutapata Zanzibar mpya, Zanzibar yenye neema, Zanzibar yenye furaha na

Zanzibar yenye mapenzi ya kweli, lakini Zanzibar ambayo itakuwa namaendeleo na naamini maendeleo haya yatakuwa ni ya haraka sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hawa viongozi wetu niseme ni watoto wa halali wa marehemu baba zao. Kwa sababu wanafuata zile zile nyayo za wazee wao. Mhe. Spika, Rais wetu wa kwanza muasisi wa nchi yetu marehemu Mzee wetu Mhe. Abeid Amani Karume katika sheria yake ile ya mwaka 1964, sheria ambayo iliitwa ya usawa maridhiano na umoja. Ndio huu Mhe. Spika, viongozi wetu hawa wawili walikutana na kutanabahi na wakakumbushana, tunakwenda wapi, mbona tunatoka kule kwenye malengo yetu makuu ya Mapinduzi. Mbona tunatoka kwenye usia wa Mzee wetu.

Mhe. Spika, walikumbushana na wakasameheana basi na sisi kwa kweli tuko pamoja nao. Nataka niungane na wenzangu Mhe. Spika, kwa kusema kuwa elimu ni kitu muhimu, tuwashukuru wenzetu wale sita wa Baraza lako hili tukufu. Nataka niwapongeze sana kwa jitihada ambayo walichukua na wakatoa elimu kwa Wazanzibari naamini ushindi ule wa ndio ambao ulipatikana wa asilimia 66.4 ni wao ambao walichangia kwa kiasi kikubwa Mhe. Spika.

Kwa kweli Mhe. Spika, wenzetu walikuwa hawana uelewa wa hili jambo lenyewe lilivyokuwa likienda. Naamini hata wale ambao walisema hapana, japokuwa Mhe. Spika, demokrasia ina gharama zake na huu ndio upana wenyewe wa demokrasia, sio kila kitu ambacho unakiona wewe kizuri na mwenzako atakiona ni kizuri. Lakini naamini kama elimu haikufika ya kutosha. Kwa hivyo, kuna haja tusiache hapa ambapo tumefikia, lakini elimu itolewe zaidi ili hili jambo licha ya kuwa limepita kwa asilimia hii, lakini Wazanzibari wote wameliridhia kwa moyo mmoja. Kwa sababu munapokuwa na umoja nyote basi baraka na neema Mhe. Spika, inaingia. Naamini ushindi ule ambao umepatikana, sio ushindi wa mtu au wa kundi fulani ni ushindi wa Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, pia naomba kama kuna tunzo yoyote na zipo ambazo wanapewa viongozi kwa kazi nzuri ambazo wamefanya kwenye nchi zao, basi naamini viongozi wetu hawa wawili wanastahiki kupewa tunzo hizo. Sisi Wazanzibari kwa kweli inatupasa tuwaenzi viongozi hawa. Kwa sababu watu wanasema 'Mhe. Spika, raha mtu anajipa mwenyewe'. Kwa hivyo, sisi wenyewe kwanza tujipe raha ya kuwaenzi hawa viongozi wetu kwa hatua hii au kwa kulichukua jahazi mpaka wakalifikisha hapa.

Mhe. Spika, katika hili mengi yamesemwa, lakini na mimi nilikuwa mmoja kati ya wajumbe wa kamati hii ya sheria na katiba ambayo imepitisha suala hili. Sitokuwa na mengi katika suala hili, lakini nitakuwa mwizi wa fadhila pia iwapo kama sitowapongeze kwa dhati Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kweli ilifanya kazi ya ziada na kama kamati iliturahisishia kazi yetu kuwa nyepesi sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna nafasi za wanawake ni kwenye kifungu cha 42 cha mswada, lakini pia ni kifungu cha 67(1) cha katiba. Kimerekebisha kutoka asilimia 30 na tunataka tufikie asilimia 40. Mhe. Spika, kwa dhati kabisa, naomba kuishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa mwanamke na kwa kuona ile asilimia 30 tuliopewa kwa kweli Mhe. Spika, tuliifanyia kazi. Tuliifanyia kazi na nadhani tumeisaidia sana nchi yetu na hii asilimia 40 nataka niahidi mbele yako Mhe. Spika, wanawake hatutoiangusha serikali yetu. Tutaendelea kuihakikishia serikali kwamba kweli tunaweza na tumeonesha mifano ya kuweza kwa wawakilishi wako wote tuliomo kwenye Baraza, lakini kwa mawaziri wetu wanawake ambao wamo katika Baraza lako hili, ni namna gani ambavyo tunaona wanachapa kazi.

Lakini Mhe. Spika, naomba hii asilimia 40 isimalizie tu katika Baraza lako hili, iende mpaka kwenye ngazi za utendaji. Tunatarajia Mhe. Spika, tuone mabadiliko katika nafasi za Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na Wakurugenzi tuwemo kwa kiwango hiki cha asilimia 40. Namalizia kusema Mhe. Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Saleh Ramadhan Feruz: Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuwa sehemu ya waja wake ambao bado wazima wenye afya, lakini zaidi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezeshwa kuweza kukutana leo hapa Mbweni katika ukumbi

wetu huu wa Baraza la Wawakilishi, kwa madhumuni makubwa ya kujadili na hatimaye kupitisha mswada huu wa marekebisho ya kumi ya katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi, ili na mimi nichangie katika mswada huu.

Mhe. Spika, nianze kuchangia kwa kusema kwamba na mimi naunga mkono kwa asilimia 100. naunga mkono kwa asilimia 100 kwa sababu mswada huu ni mzuri, mswada huu una nia njema kwa Wazanzibari, mswada huu unajenga historia mpya ya nchi yetu na kwa kweli mswada huu ndio utakaoimarisha mizizi ya Wazanzibari kuishi katika hali ya amani, usalama, utulivu na kuishi katika mashirikiano, lakini zaidi kuishi kwa kushikamana.

Mhe. Spika, mimi nashukuru niliposoma skuli, kati ya masomo niliyosoma nilisoma na somo ya historia. Lakini sio hilo tu, nashukuru pamoja na kumaliza kusoma, lakini nimekuwa mpenzi sana na shabiki mkubwa wa kufuatilia mambo ya historia, hususan ile historia nzuri.

Mhe. Spika, katika kusoma kwangu historia, labda wale walionizidi watanisaidia, sijawahi kusoma katika historia ya Zanzibar inayoeleza kwamba Zanzibar ni Muungano kati ya kisiwa cha Unguja na kisiwa cha Pemba, sijawahi kusoma historia hiyo. Historia yote niliyowahi kusoma kuhusu Zanzibar ilikuwa inaeleza kwamba Zanzibar ni visiwa viwili cha Unguja na Pemba na visiwa vidogo vinavyovizunguka.

Mhe. Spika, kwa takriban miaka 15 historia hii ambayo mimi nimeisoma ya kwamba Zanzibar sio Muungano, ilikuwa ina mwelekeo wa kubadilishwa, ilikuwa kwenye hatari, ilikuwa kwenye ukingo wa shimo kubwa. Mazingira yaliyokuwa yamejengeka kwa miaka 15 Mhe. Spika, ambayo mimi yalikuwa yanantia hofu kubwa, yalikuwa yanataka kuijenga Zanzibar kama vile ni Muungano wa visiwa viwili.

Mhe. Spika, leo nanyanyuwe mikono juu namshukuru Mwenyezi Mungu sana, namshukuru Mwenyezi Mungu kupita kiasi na namshukuru Mwenyezi Mungu kuwa hili tukio limetokea leo mwezi 28 Shaaban, kwamba sisi tuliochaguliwa na Wazanzibari na kupewa vyeo vya kuitwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, leo tunairejesha Zanzibar katika uwasili wake. Tunairejesha Zanzibar ile moja tokea asili, tunawarejesha Wazanzibari katika umoja wao, tunawarejesha Wazanzibari katika mapenzi na huba waliokuwa nazo tokea asili.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kitendo tunachokifanya leo, kwa kweli ni kitendo kikubwa sana. Ni kitendo kikubwa kwanza mbele ya Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataalah, pia ni kitendo kikubwa kwetu sisi Wazanzibari. Wale Maulamaa nikikosea watanisawazisha nje, lakini naamini katika kitabu tunachokiamini sisi Waislamu kinatuelekeza kwamba endapo utaliona jambo baya linatendeka, basi unatakiwa kwanza ulizue kwa mikono yako, likikushinda kulizuwia kwa mikono ulizuwie kwa maneno, likikushinda kwa maneno basi ulichukie au ulinunie.

Sasa Mhe. Spika, kazi tunayoifanya leo ni kwamba tumezuia maovu au mabaya kwa mikono yetu. Ninaamini kwa tarehe ya leo, tarehe 09/08/2010 sawa na mwezi 28 Shaaban kwa tukio hili tunalolifanya hapa, basi litachangia kwenye safari yetu ya kuingia kwenye pepo ya Mwenyezi Mungu, maana tunafanya jambo kubwa sana lililoamrisha na mwenyewe Subhanahu Wataallah.

Mhe. Spika, jambo lolote lina sababu na mimi niungane na wenzangu waliotangulia, kuwashukuru na kuwapongeza waliolanzisha hili jambo na hatimaye leo tunafika katika hatua hii. Nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaji Dk. Amani Karume, pamoja naye nimpongeze Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad Alhaji, kwa hatua waliyoichukua mbayo leo inatufikisha hapa. Tumeambiwa kwamba wapo waliowashauri nao tunawapongeza. Nampongeza sana Mzee wangu Mzee Hassan Nassor Moyo.

Lakini Mhe. Spika, kushauriwa ni jambo moja na la pili zito ni kukubali ushauri. Kwa hivyo, nawapongeza tena Rais Karume na Maalim Seifu kwa kupokea ushauri na kuufanya kazi.

Pia nichukuwe nafasi hii kuwapongeza viongozi wa chama cha Mapinduzi kwa hatua zote walizochukua katika kulifanya jambo hili lifanikiwe. Halikadhalika nawapongeza sana viongozi wa CUF nao kwa jitihada walizochukua kulifanya jambo hili liwe.

Mhe. Spika, wenzangu walionitangulia walisema kwamba viongozi wetu wawili hawa wanahitaji kupewa tunzo, wengine walisema tunzo ya *noble* wengine walizitaja nyengine. Katika sherehe ya ufunguzi wa Uwanja wa Ndege, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na yeye alianzisha nishani yake pale.

Jambo moja Mhe. Spika, naomba niliwekee mkazo ambalo limesemwa ya kwamba Baraza hili tukufu ambalo wewe unaliongoza Mhe. Spika, ni vyema likatoka na azimio maalum la kumpongeza Rais Amani Karume pamoja na Maalim Seif kwa kazi kubwa waliyoifanya ambayo leo kila Mzanzibari na kila binadamu mwenye akili timamu anaishangiria.

Mhe. Spika, niungane na mwenzangu ambaye au wenzangu ambao wamezungumzia juu ya kumtunza na kumuenzi Rais Amani Karume. Mhe. Spika, binafsi niliwahi kuzungumza kwenye mkutano mmoja wa hadhara wa chama chetu, nikasema kile Chuo Kikuu cha Marekani kilimtunuku Rais Amani Karume udaktari kama sikosei wa elimu. Pia Chuo Kikuu cha Harbart Kakairuki kimemtunu udaktari wa afya. Pale sikutania lakini nilisema hasa kwamba nadhani upo umuhimu wa Chuo Kikuu kingine kikamtunuku udaktari wa *Political Science*. Sasa kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaama wanatusikia hivi sasa kina daktari Bana na wengineo au Chuo cha SUZA basi wafikirie kumpatia heshima hiyo ya udaktari wa falsafa katika *science* ya siasa.

Mhe. Spika, nilipongeze sana Baraza lako hili tukufu. Baraza hili Mhe. Spika, chini ya uongozi wako limefanya kazi kubwa sana na lilipitia katika mitihani mikubwa sana katika kulifanikisha jambo hili. Kwa bahati nilikuwa sijaingia ndani ya Baraza, lakini nilijitahidi sana kuwa karibu na Baraza kwa kipindi hicho ili kuweza kuona nini kinaendelea ndani ya Baraza. Wakati wa hoja binafsi ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary haikuwa hoja rahisi, ilikuwa hoja nzito, ilikuwa ni hoja ambayo ingeweza kuleta mpasuko zaidi kama busara isingetumika, ilikuwa hoja ambayo kwa lugha nyepesi naweza kusema ulikuwa kama mpira wa kona, ma-*defender* wanataka kuuokoa na ma-*forward* wanataka kutumbukiza wavuni, haikuwa hoja nyepesi. Lakini nashukuru chini ya uongozi wako Mhe. Spika, ukaweza kuisimamia hoja ile mpaka maamuzi ya busara yakapatikana na likapatikana azimio la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kukupongeza sana Mhe. Spika, na Mwenyezi Mungu akubariki na naamini huko tunako kwenda baada ya tarehe 11 ya mwezi huu litakalofunguliwa jipya utakuwa nalo wewe mwenyewe na wala sikupigii debe, lakini kuna msemo wa Kiswahili unaosema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni na mimi ninakupa haki yako. (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Spika, na mimi nijumuike na wenzangu kuwapongeza Wazanzibari kwa kufanya uamuzi, kwa kweli uamuzi ambao umewezesha kufanyika kikao hiki leo. Lakini nirudie kusema kwamba kazi haikuwa nyepesi. (*Makofi*)

Kwa msingi huo Mhe. Spika niipongeze Kamati ya Watu Sita ikiongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali kwa kazi kubwa waliyoifanya, ambayo imeweza kutoa elimu kwa kiwango kikubwa sana na kuweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana kwa ushindi wa asilimia 66.4. (*Makofi*)

Lakini tukirudi kwenye vitabu vyetu tunaambiwa aya ya kwanza ilikuwa ni *Iqraa*, yaani soma. Kwa hivyo, alivyokifanya Mhe. Ali Mzee Ali ni kutusomesha, kutokana na hali hiyo tunakushukuru sana, tunakupongeza pamoja na kamati yako. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mambo mengi yalipita katika kipindi hicho, nadhani si vibaya tukapeana pole kwa sababu tunapongezana sana hapa na wala hatujapeana pole. Kwa hivyo, ni vyema kupeana pole kutokana na maathiriko yoyote tuliyoapata katika harakati kuhusiana na zoezi hili.

Kwa mfano, walioandikwa, waliosemwa, walioumizwa kwenye michakato mingine kwa sababu hiyo. Lakini msingi ulikuwa ni kuirejesha Zanzibar katika uasilia wake. Kwa hivyo, maumivu ya mambo yale si makubwa sana. Vile vile tumeamrisha kwamba wenzenu wanapokukoseeni basi wasameheni na baadaye msahau. (*Makofi*)

Katika kupeana pole huko kwa yale yaliyotukuta basi wale waliotutendea tuwasamehe na tuyasahau na kubwa ni kujenga nchi yetu, tuwe wamoja, pia tuijenge nchi yetu kwa pamoja, ili iweze kupata maendeleo makubwa.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kurudia kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia kukushukuru wewe pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa kuweza kutufikisha hapa tulipofika. Kwa kweli sitegemei kama tutageuka nyuma na ikiwa tutageuka nyuma, basi Mwenyezi Mungu anayo sababu ya kutugeuza mawe na wala siamini kama sisi tuko tayari kugeuka mawe. Kwa maana hiyo, tutasukumu gurudumu letu mbele, ili hatua kubwa zaidi za mafanikio katika nchi yetu ziweze kupatikana.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mhe. Mkongwe Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na salama.

Mhe. Spika, wajumbe wako wote wa Baraza la Wawakilishi wanamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa jinsi alivyotuwezesha kuingia kwenye Baraza hili katika ukumbi huu.

Kwa kweli kulikuwa na wengi ambao ni wenzetu walitarajia nao waonje japo dakika moja, lakini Mwenyezi Mungu hakuwajaalia. Kwa hivyo, sisi Mwenyezi Mungu ametujaalia tokea asubuhi mpaka hivi sasa bado tupo hai, kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kadari yake pamoja na utukufu wake.

Vile vile Mhe. Spika, namshukuru Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume kwa jinsi alivyoweza kutekeleza mambo yake yote katika kipindi chake cha miaka kumi. Kwa kweli Rais wa Zanzibar amejitahidi sana kwa kuipamba Zanzibar, yaani Unguja na Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tukiangalia katika Visiwa vya Zanzibar basi umeme unang'ara ndio tunauona, maji pia hayana mfano, barabara zinaelea na hata kule Bumbwini *bulldozer* tayari limeshaanza kung'oa miti. Kwa hivyo, nategemea kufaidika. (*Makofi*)
Kwa hivyo, kwa kusema kweli Mhe. Rais wa Zanzibar katika mapumziko yake mema Mwenyezi Mungu atamjaalia pamoja na kumsaidia.

Mhe. Spika, wenzangu wengi walionitangulia wameyaeleza mengi, lakini na mimi nimeona japo kidogo nitoe sauti yangu. Kwa hivyo, kwanza ninaipongeza Kamati ya Watu Sita ambayo ikiongozwa na Mwenyekiti Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Mwenyekiti wa kamati alifanyajitihada kubwa sana. Kwa mfano, ninakumbuka wakati tulipokuwa Dodoma Mhe. Ali Mzee Ali, aliwahi kuniambia katika Jimbo letu ya Bumbwini tusiharibu na nimeamini na nadhani amelisikia Jimbo la Bumbwini.
Kwa maana hiyo, namtakia kila la heri Mhe. Ali Mzee Ali pamoja na wajumbe wa kamati yake izidi kuendelea vizuri, kama lipo jambo jengine la kutekeleza basi wapewe kwa lengo la kuendelea mambo kama hayo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kwamba sina mengi ya kusema, isipokuwa ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*) Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kupata muda wa kuchangia mawili au matatu kuhusu Mswada huu wa Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar.

Kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhanahu Wataalla* kwa kunijaalia jioni hii ya leo kuwepo hapa na kwa ajili ya kuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, pongezi nyingi zimetolewa na Waheshimiwa wenzangu. Kwa hiyo, nami niungane na waheshimiwa wenzangu kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Amani Abeid Karume kwa kviendeleza visiwa vyetu hivi hadi kufikia maendeleo makubwa, pamoja na usimamizi wake mwema katika masuala mazima ya amani na utulivu wa nchi yetu. (*Makofi*)

Pongezi peke zimuendee Mwenyekiti wa Kamati Watu Sita Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuweza kusimamia kamati ile, pia kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na marekebisho ya Katiba pamoja na muundo wa serikali.

Mhe. Spika, marekebisho haya ya katiba ni matokeo ya Kura ya Maoni, ambapo wananchi wa Zanzibar walipiga kura siku ya tarehe 31 Julai, 2010, ambapo wananchi walipata nafasi ya kutumia haki ya kidemokrasia juu ya muundo wa serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa kweli wananchi waliweza kuitumia haki yao ya kidemokrasia na matokeo ya Kura ya Maoni yamejionesha kwamba asilimia 66 ya wananchi wamepiga kura ya ndio juu ya muundo huo na asilimia 33 wao wamesema hapana.

Haki hii ya kidemokrasia ni haki ya msingi ambayo imetumika. Mhe. Spika, pamoja na kwamba jambo hili limepita, lakini bado serikali kuna haja ya kutoa elimu zaidi kwa wananchi hususan wale waliosema hapana, kwa sababu nao ni sehemu ya jamii.

Kwa hivyo, tufanye kila linalowezezana kuhakikisha kwamba elimu zaidi kwa wananchi inatolewa, ili sote twende sambamba katika suala hili. Nadhani si vyema kwamba baadhi ya maeneo tukayaacha mbali.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, afanye kila linalowezezana kutoa elimu kuhusu wenzetu hawa ambao inaonekana bado hawajafahamu vizuri na tukitilia maanani kwamba muda ulikuwa ni mdogo mno.

Mhe. Spika, marekebisho haya ya Katiba nimeangalia yapo kwenye maeneo matatu makubwa. Kwanza marekebisho yenyewe ya msingi ambayo yanakusudia kufanya mabadiliko ya Katiba juu ya Muundo huu wa Serikali Shirikishi, pia kuna mabadiliko ya vifungu vya katiba, ambapo serikali imeona ipo haja ya kuvifanyia marekebisho kulingana na wakati wenyewe. Vile vile kuna marekebisho ama ya maandiko pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli mimi mwenyewe nimefurahishwa sana Mhe. Spika na baadhi ya marekebisho ambayo yamefanywa ndani ya katiba hii. Katika kipindi kirefu yameonekana hayaendani sambamba na wakati wenyewe ulivyo. Kwa mfano, marekebisho ya katiba kifungu cha 1, 2 na kifungu cha kidogo cha pili, ni marekebisho ambayo yalikuwa hayaendani na wakati wenyewe. Kwa hivyo, hivi sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba serikali imeyaona hayo na imeweza kuyafanyia marekebisho.

Mhe. Spika, kuna kifungu kimoja ambacho kinahitaji kuangaliwa katika marekebisho haya ya katiba, kifungu cha 17 naomba kunukuu Mhe. Spika,

Kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar kinachosema hivi:-

“Kifungu cha 34 cha katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:- ambapo sehemu ya nne imezungumzia hivi.

“(iv) Bila ya kujali masharti ya vifungu vya 28(3) na 30(1)(b) vya Katiba, endapo mtu anayemfuata Rais kwa madaraka atashika kiti cha Rais kwa kipindi kinachopungua miaka minne ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara mbili, lakini kama atashika kiti cha Rais kwa muda wa miaka minne au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara moja tu.”

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri kifungu ninachokinukuu amekiona. Sasa kuna eneo hapa limeandikwa anayemfuata rais kwa madaraka atashika kiti cha rais, hapa Mhe. Spika ningependa pafanyiwe marekebisho kama yalivyofanywa marekebisho katika sehemu ya kwanza nadhani hapa pamesahaulika.

Kwa hivyo, baada ya kuandika kwa madaraka atashika kiti cha rais, basi iwe kwa mujibu wa kifungu cha 31(1) na hili neno kwa anayemfuata rais kwa madaraka atashika kiti cha urais iondoke na badala yake iwe kwa mujibu wa kifungu cha 33(1), ambapo tukiangalia kifungu hicho kinaeleze hayo. Kwa maana hiyo, hapa nadhani kuna haja ya kufanyiwa marekebisho na wala pasibakie kama palivyo.

Mhe. Spika, eneo jengine la mswada ambalo nahisi linahitaji kufanyiwa marekebisho ni kuhusu kinga ya wajumbe. Kwa mujibu wa marekebisho haya inaonekana kwamba wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wamepunguziwa kinga katika katiba ya zamani, lakini kinga hiyo kwa mujibu wa marekebisho ya katiba hii imeondolewa au imepunguzwa nguvu.

Kwa kweli sijaona haja ya kupunguza kinga za wajumbe. Kwa hivyo, Mhe. Spika nadhani kuna haja ya kuliangalia eneo hilo kwa makini zaidi, ili tuone kwamba kinga kwa wajumbe bado inaendelea kubakia.

Mhe. Spika, kwa sababu kinga hii kwa wakati ule ilifanywa kwa madhumuni halisi na kupunguza kinga kwa wajumbe kunaweza kuleta athari katika utekelezaji wa shughuli zetu za Baraza. Kwa hivyo, kama maelezo yaliyoandikwa hapa hayatoshelezi, basi serikali kuna haja ya kuangalia upya, lakini kinga hii ambayo imetajwa kwenye katiba hii mwanzo bado inahitaji kuwepo na kuondoka kwake kunaweza kuleta madhara hapo baadaye.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika niombe serikali kupitia Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kuliangalia zaidi eneo hilo, ili lionekane kwamba linakwenda na wakati.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa, isipokuwa maeneo ambayo nimehitaji yafanyiwe marekebisho, basi nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako kuwa ayafanyie marekebisho ni hayo.

Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magomeni tunakubaliana na marekebisho haya ambayo tayari tumeshayapitisha katika vikao vilivyopita na pia Kura ya Maoni imeshafanyika na matokeo yameonekana. Kwa hivyo, tunakubaliana na mabadiliko haya na tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*) Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ninafuraha kuona mazingira mazuri ndani ya Baraza humu kwamba wajumbe tuko wengi wa kutosha na ninahofu kuiachia nafasi hii tukaja kufanya maamuzi ya mwisho tukiwa na *quorum* yenye wasi wasi, kwa sababu najua kipindi hiki ni kigumu kidogo na tunayo mambo mengi. Kwa hivyo, nilitaka mazingira haya niyatumie, kwa ajili ya kumaliza kazi hii na wala nafasi hii isiniponyoke.

Nadhani ni vyema kuitimia nafasi kuomba radhi baadhi ya waheshimiwa wajumbe, na ninaomba mnikubalie na hasa baada ya kuwasiliana na Mhe. Waziri. Kwa hivyo, basi niwaite wajumbe watatu akiwemo yule ambaye nimetangulia kumtaja na baadaye nimkaribishe Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na mwisho nimalizie na Mhe. Ali Mzee Ali. (*Makofi*)

Nakushukuruni kwa kunikubalia hivyo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada wa Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, kabla ya yote kwanza nikupongeze wewe kwa dhati kabisa kwa umahiri wako pamoja na uongozaji wako mzuri uliotuongoza Baraza hili hadi kufikia hii leo. *(Makofi)*

Vile vile nikupongeze kwa muono wako, yaani mtu ukimuona tayari umeshamjua ndani ya ubongo yuko vipi. Kwa hivyo, Mhe. Spika nakupongeza sana kwa kutuongoza kipindi hiki na kijacho, yaani utuongoze sisi wajumbe wako pamoja na wale watakaomaliza michakato yao na kurudi hapa akiwemo *Professor Denge* basi nao uje uwaongoze. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nimpongeze Rais wa Zanzibar pamoja na Katibu Mkuu wa Chama cha CUF kwa juhudi yao kubwa waliyochukua na kukutana, kwa lengo la kuzungumzia haya masuala tunayoyazungumza leo. Pamoja na kwamba kulikuwa na mambo ya hapa na pale kwa sababu watu walikuwa hawajafahamu, lakini kila siku zinavyokwenda wanafahamu. Kwa hivyo, niwapongeze sana kwa juhudi yao kubwa sana waliyochukua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa wengi wameshachangia basi na mimi nitachangia katika maeneo machache tu, ili na mimi niwe miongoni mwa waliochangia. Kwa kweli ninachokiomba katika marekebisho ya katiba, basi ninaomba katiba hii iwe yenye kutoa uamuzi na wala isiwe yenye kuamuliwa. Kwa mfano, kwenye marekebisho ya katiba hii ninaomba baadhi ya vifungu vikachambuliwa kwa umakini na kuweza kuwa na maamuzi ya kutambulika kwamba Zanzibar ni nchi.

Kwa maana hiyo, kwenye marekebisho ya katiba hii ningependelea sana vile vifungu ambavyo vina utata basi vifanyiwe masawazisho, ili na sisi tuwe na katiba yenye kujitegemea na kuwa mfano katika nchi hii. Kwa kuwa naamini wazi kama inavyozungumzwa kuwa katiba si Msahafu kwamba wakati wowote ikiamuliwa kurekebishwa basi inarekebishwa kama hivi tunavyoirekebisha leo.

Kwa hivyo, wanaomba wananchi watulie na tusikilize wakuu pamoja na watendaji wa sheria jinsi watakavyoifanyia marekebisho na namna gani kuweza kuwa na katiba yetu nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika masuala haya niwapongeze wanakamati sita wakiongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali kwa juhudi yao kubwa waliyochukua katika kipindi kifupi ya kuhamasisha wananchi na kulielewa suala kwa kushirikiana na vyombo vyetu vya habari. Kwa kweli nawapongeza sana kwa juhudi kubwa waliyoichukua. *(Makofi)*

Tunakubali kwamba mambo haya yamekuja kwa kipindi kifupi ambapo wengi wetu tulikuwa na wasi wasi. Lakini katika kipindi hicho kifupi walielimika wananchi wengi ambapo wengi wao wamefahamu vyema kwamba namna gani serikali shirikishi hizi zinavyotaka kuletwa.

Mhe. Spika, niwapongeze wananchi wa Zanzibar ambao walijitokeza kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kupiga kura ya ndio na hapana. Kwa kweli nawapongeza sana kutokana na kutumia haki yao hiyo. Kwa hivyo, kama nilivyozungumza kwamba kipindi hiki kilikuwa kifupi ndio wengi walitia ndio na wachache wakatia hapana.

Kwa kweli naamini wazi kwa taaluma hii iliyotoka leo pamoja na mfano uliopatikana kwamba tumepata sifa na kupongezwa na mataifa mbali mbali ya nje yakiwemo Uingereza, Marekani, Sweeden nakdhalika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na hali hii ya hivi sasa kwamba wananchi wengi wameshafahamu, basi naamini kama kungekuwa na ruhusa ya kurejewa tena, basi kura za ndio zingekuwa kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, nawapongeza wanakamati hii kwa kuhamasisha kwao kwa kushirikiana na waandishi wa habari kwa kipindi kifupi tu wananchi wameelewa mambo haya kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitoe mfano maji yakiwa kwenye mlima na kutiririka kwa vizuri, sasa labda ukenda kuyazuia kwa lengo kuharibu ule utaratibu wake wa kule yanakokwenda. Hivyo sipati mtandao wake kule yanakokwenda. Kwa kweli matokeo yake maji yale huenda yakakutupa wewe, wewe chini ukaanguka matopeni. Lakini kama utayaachilia yanatiririka mpaka yanafika sehemu yalipokusudia, kama kwenye ziwa au uwanda. Neema ya pale itapatikana kama kutakuwa na rutba, itasaidia kwa wale wahusika wa pale. Kwa hivyo na haya yalivyoanza juu na kuja chini tustahamili tu Mwenyezi Mungu ataleta rehema na tutafanikiwa wananchi sote katika nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi niwapongeze hawa walioleta hoja hii na leo hapa kupata kuifanyia kazi ili kuleta maendeleo ambao wengi wao walikuwa hawafahamu nini kilichokusudiwa. Kipindi cha nyuma tunakotoka ilikuwa sisi tuliokuwa masheha ukimuuliza mtu hali anakuambia kaulize nyumbani kwako, ilikuwa mtu ukimuamkia anakunyamazia kimya. Lakini leo tunaulizana vizuri na tunasalimiana vizuri hapa, kwa upande wa upinzani na upande tawala tunakwenda sambamba vizuri tu. Hapa namshukuru sana Mhe. Subeit Hassan alinishukuru sana na kunipongeza sana kutokana na mambo yetu yanavyokwenda mimi mwenyewe sikutegemea. Lakini namshukuru kwa kuwa tuna maelewano mazuri na tunakwenda vizuri katika kazi zetu zote tulizozifanya za kamati na mambo mbali mbali kwa hivyo hili nalipongeza kwa ushirikiano huu.

Mhe. Spika, kuna mengi tu lakini naona kwa hapa panatosha isipokuwa kubwa tu nitaomba tushirikiane kama tunavyoshirikiana tuondoshe yale ya nyuma ambayo yamepita tujipange upya kwa haya yajayo. Mhe. Spika, mswada huu mimi naunga mkono mia kwa mia ahsate sana. *(Makofi)*

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba: Mhe. Spika, na mimi niungane na waliotangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu wataala kwa kutujaalia leo kukusanyika hapa katika ukumbi mpya wa Baraza la Wawakilishi jambo ambalo tulikuwa na hamu nalo sana, ndio maana hii koramu ikawa hivi. Hii ina mambo mawili kwa hili jambo lenyewe na huu ukumbi wenyewe.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Rais Amani Abeid Karume kwa uamuzi wake huu wa makusudi wa kusamehe na kukubali maridhiano. Kimsingi ni kupevuka kisiasa na kuiwa kidini, kwa sababu tumeambiwa sameheaneni. Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa makusudi kwenda Ikulu na kuonana na Rais ili kutengeneza Zanzibar yetu sasa tunaita Zanzibar mpya yenye maridhiano.

Leo Wazanzibari wote tunaelekea kwenye uchaguzi kwa kawaida utafikiri hatuelekei kwenye uchaguzi maana taimu kama hii sisi wenzetu tulioko Pemba tunakuwa tayari kashkash zimeanza. Lakini leo Alhamdulillah hata ukisikia manung'uniko basi ni manung'uniko yaliyopo kwenye vyama murua kabisa. Nawaomba Wazanzibari wote hali hii ya utulivu ambayo imesababisha na viongozi wetu wa kitaifa hawa tuidumisha hasa pale baada ya kupokea matokeo magumu sana ya tarehe 31 au tarehe 2/10 tutulie na tuendeleo na maridhiano kwa sababu hakuna atakayepoteza. Kuna mtua atakayetangulia tu, lakini mwengine atakuwa yupo hapo chini ya mgongo wa mwengine.

Pia sitafanya haki kama sitaipongeza kamati ya watu sita. Imefanya kazi kubwa sana ya kuelimisha watu na imekuwa pole sana. Pale ambapo imepata maneno mazito, jawabu ya mwenyekiti baadhi ya vikao vyake nilihudhuria anawaambia hiyo ni demokrasia yako. Lakini bado waliendelea na ufafanuzi na wajumbe wake walikuwa wakicheka tu walikuwa hawanuni, hili ndilo ambalo limetufikisha hapa ambapo tumefika.

Mhe. Spika, mimi niangalie kifungu cha 41 kwenye mswada huu pale ambapo panasema kwamba kutakuwa na wajumbe 10 wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi. Watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoлезwa na kifungu cha 66 cha katiba, isipokuwa kwamba wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika

Baraza la Wawakilishi au kwa kushirikiana na vyama vya siasa vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi. Napata tabu kidogo lakini japokuwa jambo hili limekuwa likiangaliwa kila wakati. Mimi nadhani kwa sababu ya kuwa tuna makamo wa kwanza wa Rais, sidhani kwamba kama tutakuwa na Makamo wa Kwanza wa Rais ambaye hatakuwa mtu wa pili kapata kura nyingi za Urais katika Baraza la Wawakilishi.

Fikira zangu ni kwamba Makamo wa kwanza wa Rais huyo huyo kwa msimu huu ndiye atakayetoa kiongozi wa upinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi. Inawezekana labda sijafahamu kwamba kwa mfano labda tumefanya uchaguzi. Chama kimoja cha upinzani kimepata viti kumi na wengine wamepata kiti kimoja au viti viwili. Akili yangu inaniambia kwamba huyu ambaye amepata viti viwili kiongozi wa upinzani atapata huyu mwenye viti kumi zaidi. Kwa kuwa huyu mwenye viti kumi kule kwenye *cabinet* kuna makamo wa kwanza wa Rais mtu wa pili. Nadhani hapa ingekuwa vizuri zaidi kama huyu makamo wa kwanza wa Rais ashauriane na Rais kwa ajili ya uteuzi wa wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi hawa kutoka kwenye kambi ya upinzani. Lakini kwa sababu ya muda inawezekana labda tunaweza kulichukua wakati mwengine tukaliangalia.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo madogo sana nakubaliana na mswada huu mia juu ya mia na wananchi wa Zanzibar leo wamo katika furaha kubwa kwa jambo hili ambalo tulikuwa tunalisubiri kwa hamu kubwa sana. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Kamati ya Wajumbe sita: Bismillahi Rahmani Rahim Mhe. Spika, leo ni siku tukufu katika historia ya Zanzibar, Zanzibar mpya baada ya muda mfupi itapitishwa leo humu ndani (*Makofi*).

Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hatua hiyo, mimi naitwa Ali Mzee Ali kwa watu wengi labda wawili tu walisahau kuipongeza kamati yetu. Lakini wote waliipongeza kamati yetu nimeelemewa mimi kwa niaba ya wajumbe wa Kamati yangu nachukua nafasi hii kuwarejeshea shukurani wajumbe wote wa Baraza hili kwa kushirikiana na mimi, kwa kutuomba dua. Lakini wajumbe wa Baraza walikuwa wanatoa sifa hizi ni zao kwa sababu kamati hii ni kamati ya Baraza la Wawakilishi. Lakini kama kuna mtu ambaye anastahiki sifa basi hakuna mwengine isipokuwa wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho.

Mhe. Kificho mimi nilikuwa Marekani nimerudi nimekuta barua kwa kuwa umeniteua kuwa mjumbe wa kamati hii lakini ilikuwa sijui nani wenzangu ambao umewateua, anaempenda Kificho kama hampendi Ali Mzee basi hampendi Kificho na anayempenda Ali Mzee kama hampendi Kificho basi hampendi Ali Mzee, mimi na wewe ni ndugu, marafiki na tunapendana na tunaaminiana. (*Makofi*)

Mhe. Kificho inawezekana ndio hotuba zangu za mwisho hizi umenipa uwezo miaka minne nikusaidie hapo siku yoyote nikiamua kuwa Spika wa Comoro nitasema nilifanya kazi miaka minne kule Zanzibar na nani aliyenipa uwezo huu ni wewe, nakushukuru sana asana. Katika miaka minne yetu hii mimi na wewe hatujapata kukosana ila ni mara moja tu hiyo ni kawaida Mtume Muhammad kashushiwa aya mara mbili Mwenyezi Mungu kumkosoa sembuse mimi na wewe mara moja tu tena kwa mambo ya kitoto. Mimi nimekusamehe na wewe umenisamehe. (*Makofi*)

Nachukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi changu cha miaka kumi humu ndani sijapata kugombana na mtu hata mmoja, hata wale nilioambiwa walisema husema aa si kweli mbona mbele ya uso wangu haniambii, kwa hivyo nawashukuru sana nimefanya nao kazi pamoja na wananiheshimu Alhamdulillah. Sifa hizi kuzipata ni za baraza sio zangu lakini Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa niruhusu nitoe sifa zilizotoka sio baada ya kura za maoni ni kabla Wazanzibari kwa kupitia wawakilishi wao katika Baraza la Wawakilishi wameamua kuchukua hatua kubwa na muhimu kwa kutafuta suluhu ya Kizanzibari kwa matatizo ya Zanzibar. Baraza hili limeunda kamati ya watu sita ambayo jukumu lake kubwa itakuwa ni kutekeleza azimio la Baraza la Wawakilishi la kuendesha zoezi la kura za maoni lililo huru na la haki ili kuwawezesha wananchi kuamua aina ya serikali wanayoitaka.

Napenda kutoa pongezi na heshima zangu kwa dhati kwa wajumbe wa kamati hii Mola awajaalie busara ya kuweza kuongoza vyema shughuli hii ya kusaidiana na kujenga mfumo utakaoweza kufanyika kwa uchaguzi ulio huru wa haki na amani na kuanzisha kwa serikali inayosikiliza sauti ya Wazanzibari wote duwa zangu zi pamoja nanyi.

Alfonso Leonard balozi wa Marekani nchini Tanzania alitoa salamu hizi tarehe 14 Julai, 2010 kabla ya kura za maoni. Hizi salamu sio zangu za Baraza la Wawakilishi watu wengi wamezungumza maazimio. Hili Baraza la Wawakilishi la leo ambalo wewe unaliongoza wajumbe wake waliomo ndani humu na wanaomwa wabakie ndani ya historia. Litengenezwe jiwe liwekwe pale waandikwe hawa ndio wawakilishi ambao wamepitisha serikali ya mseto ya Zanzibar majina yao yaweko pale. (*Makofi*)

Kwa sababu na jina la mwanzo litakuwa la Pandu Ameir Kificho kwa nini nikasema hivyo kwa sababu tumefanya maamuzi makubwa. Leo hapa watu walikuwa wanaisoma sheria ile ya Mzee Karume lakini sheria ile ina wenyewe, sasa jambo hili na sisi hivi leo lina wenyewe kadhalika sheria ile imetiwa sahihi na watu wafuatao. Rais Abeid Amani Karume, Msaidizi Rais Abdalla Kassim Hanga, Mhe. Abraham Babu, Mhe. Hasnu Makame, Mhe. Aboud Jumbe, Mhe. Salehe Sadala, Mhe. Idrissa Abdulwakil, Mhe. Othman Sharif, Mhe. Abdulazizi Twala, Mhe. Hassan Nassor Moyo yule pale juu.

Kwa kuwa mimi ni mwenyekiti wa Baraza.

Mhe. Spika: Naomba Mzee Hassan Nassor Moyo asimame tena kwa kuwa ametajwa hapa na yupo pale juu ili tumpe pongezi zake Mhe. Hassan Nassor Moyo (*Makofi*)

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, katika wajumbe waliokuwa mwaka 1963 wa Afro Shirazi Party wajumbe walio hai ni Mhe. Hassan Nassor Moyo na Aboud Jumbe waliobakia wote wameshakufa, lakini Mhe. Hassan Nassor Moyo naomba nimitaje kidogo halafu nitaendelea. Mhe. Hassan Nassor Moyo alihudhuria mkutano wa *London conference* mkutano ambao ulizungumzia mustakbal wa Zanzibar mkutano huo ulikuwa tarehe 24 Septemba, 1963 Mhe. Hassan Nassor Moyo alihudhuria kwa niaba ya chama cha Afro Shirazi Party.

Mkutano huo ambao umeamua hatma ya Zanzibar lakini leo Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumza nitarudia kwenye majina yale kuhusu jamhuri, nchi ikiwa jamhuri inakuwa na Rais, mkutano wa London uliamua Zanzibar, Muingereza aliamua sasa kumkabidhi rasmi Mfalme nchi yake na anaondosha himaya juu yake. Lakini mkutano ule ulitakiwa uwe na uchaguzi Disemba 1963 lakini Muingereza akakataa akafanya uchaguzi ule ule wa Juni, 1963 ndio uliowapa serikali ya ndani na ndio ule ule akaja kumkabidhi mfalme nchi yake, watu wengi walizungumza uhuru ule wako waliosema uhuru bandia, waliosema uhuru wa kweli. Lakini kwa mujibu wa nyaraka Muingereza alimkabidhi Mfalme nchi yake na ndio maana ile *instrument* hajapewa Mohammed Shamte Hamad hakupewa.

Tarehe 2 Novemba, 1963 barua ya kukaa Zanzibar kwa serikali ya Uingereza, Mhe. Mtukufu nina heshima ya kurejea mkataba kati ya sultani wa Zanzibar na Kanal Ian Smith ile skuli inayoitwa St. Gretha yule sio muhindi alikuwa ni balozi wa Uingereza anaitwa Ian Smith ambaye ni mjumbe wa Malkia wa Uingereza katika Zanzibar iliyotiwa sahihi tarehe 14 Juni, 1890 na kuweka Zanzibar chini ya ulinzi wa Uingereza kwa vile Zanzibar imepata uhuru wake tarehe 10 Disemba 1953 ni lazima mkataba huo ufutwe katika maeneo ya milki zangu ambazo hazimo katika mkataba niliotia saina tarehe 8 Oktoba 1953 unaohusu *conference*.

Kule kwenye *conference* meli kumi za Kenya zilikuwa chini ya himaya ya Zanzibar sasa katika mazungumzo yale ikasemwa sasa na Kenya nayo ipate uhuru, kwa hivyo akaambiwa himaya hii sasa itaondoka kwako lakini utalipwa fidia na mfalme akalipwa fidia na ndio maana siku ile alipopinduliwa alikimbilia Mombasa kwa kudhani bado kule ni himaya yake na kule Kenyata akamwambia rudi akenda Tanganyika. Sasa zile fedha ambazo kalipwa kwa ukarimu na moyo mzuri, na kupenda ubinadamu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume akasema fedha ile yote anayolipwa

ibaki kule London, anapewa mfalme aendelee na maisha yake na mpaka leo mfalme yuko hai anaishi kwa fedha zile.

Kwa hivyo moyo wa kupenda na moyo wa kusamehe ulianza zamani kwa Mzee Karume, kwa hivyo ninapendekeza kuwa mkataba wa mwaka 1090 ufafanuliwe maeneo ya milki yangu yaliyo Kenya kuanzia tarehe kumi imetiwa sahihi na Jemshid bin Abdulla bin Khalifa Sultan wa Zanzibar. Sasa Muingereza anamjibu tarehe 12 Novemba. Mtukufu Sultani nina heshima kurejea barua yako ya tarehe 2 Novemba 1903 inayohusu mkataba ulioiweka Zanzibar chini ya himaya ya Uingereza na kutiwa saina tarehe 14 Juni, 1090. Kwa idhini niliyopewa na Malkia wa Uingereza nathibitisha kuwa mkataba huo utanza rasmi tarehe 10 mwaka 1963 na utahusu maeneo yote ya milki yako yaliyo nje ya Kenya, imetiwa sahihi na Sir. George Morrone, balozi mkaazi wa Uingereza.

Sasa kwa nini nilitoa habari hii Mhe. Spika, alizungumza juu ya jamhuri kwa sababu yenye mfalme haiwezi kuwa jamhuri tarehe 12 Januari, 1964 asubuhi Mzee Karume akatangaza Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ikazaliwa jamhuri ile na Zanzibar imeanza kuwa Jamhuri tarehe 12 Januari 1964 kuwa nchi kamili ambayo Rais Karume alikuwa Kiongozi. Zanzibar ikabakia kuwa nchi mpaka siku ya juu wa juu atakapoamua kula ardhi yake, sasa niliona hilo niliweke wazi.

Sasa nirudie kuwamaliza wale wajumbe Hassan Nassor Moyo, Fild Masher John Okello, Kamishna wa Polisi Edington Kissasi mwanawe yule pale yupo, Mhe. Yussuf Himid mwanawe huyu hapa, Seif Bakari, Mhe. Ramadhan Haji, Mhe. Said Natepe, Mhe. Pili Khamis, Mhe. Khamis Hemed, Mhe. Hamid Ameir Ali, Mhe. Saidi Iddi Bavuai, Mhe. Said Washoto, Mhe. Moh'd Abdalla Mfaranyaki, Mhe. Moh'd Abdalla Kaujore, Mhe. Hasnu Suleiman, Mhe. Khamis Daruweshi, Mhe. Khamis Abdalla Ameir, Mhe. Mohammed Mfaume Omar, Mhe. Muhsin Ali, Mhe. Moh'd Juma Pindua, Mhe. Daud Mahmoud kamlea Mhe. Haji Omar.

Huyu Mhe. Haji Omar mnamuona hivi huyu kaleleka na hawa ndio waliomlea, ndio maana umemuona kasimama kidete kalelewa ndani ya misingi ya mapinduzi, huu ndio ukweli huyu hapa.

Sasa Mhe. Spika, na sisi baada ya miaka ishirini au thalathini humu ndani, watu watasema hivi Baraza la Wawakilishi lililokaa tarehe 9 Agosti, 2010 chini ya kiongozi wao Mhe. Pandu Ameir Kificho, Mhe. Ali Mzee, Haji Omar Kheir, Thuwaibah Edington Kissasi, Mkongwe Nassor Juma hawa ndio waliopitisha, sasa hiyo kumbukumbu na pale iwekwe. Wala hili halitaki ombi ndio liwe tu kwa sababu ndio ilivyo duniani na nimezungumza leo na Sheikh Ali Yussuf nimemwambia kasema nitafanya hivyo, lakini watu wawili siwaweki wewe sikuweki na Mwalim Haroun nikamwambia haidhuru, anasema Kificho nitamuweka kwa sababu kimsingi jambo hili ni muhimu sana na la historia, liwekwe pale nafikiri waheshimiwa wote hili wanalikubali, sidhani kama kuna mheshimiwa aliyelikataa. (*Makofi*),

Sasa hili suala letu la maridhiano ni jambo zuri na tumegawa karatasi zile za sheria Nam. 6 iko wazi inakataa mpaka mtu kusema asili yake. Mhe. Spika, mimi na wewe tulitolewa vikaratasi mimi siwajui waliofanya nimewasamehe na wewe wasamehe, alinambia mimi simsifu. Kwanza mimi sina tabia ya kusifu ovyo. Mimi mtu nikimsifu namsifu kweli kweli kama ninavyokusifu wewe nitakusifu kweli kweli. Rais Karume tangu ameingia madarakani hotuba yake ya mwanzo aliyoitoe pale alizungumza amani na utulivu. Ni muumini na anasamehe na leo Rais Karume hapa tunaambiwa apewe nishani ninasema hayo ninakuachieni wenyewe mtaamua mnavyoona. Lakini Rais Karume ni muumini wa amani na utulivu na leo Zanzibar ameifikisha alipoifikisha.

Mhe. Spika, ndugu Seif Sharif Hamad. Huyu niliisoma hotuba yake wakati wa sheria hii namna alivyoyaeleza mapinduzi, namna mapinduzi yalivyomlea na namna anavyoamini mapinduzi. Mhe. Spika, yeye ni mtoto wa Kiswahili, hawa akina Seif Sharif Hamad, Mhe. Juma Duni Haji na Mwinyi Mzale hawa watoto baada ya mapinduzi skuli nyengine walizuiliwa kwenda kusoma, lakini yalipopatikana haya mapinduzi ndio wakapelekwa Chuo Kikuu na waziri wao ni yule pale Hassan Nassor Moyo alikuwa ni Waziri wa Elimu na amefikia kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu.

Mhe. Moyo huyu jana mchana alikuja, alipokuwa akitembelea Beit al Ajaibu alimkuta Seif Sharif pale karani ameshatoka chuoni akamchukua mpaka kwa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, akamwambia kijana wetu, mtoto wetu huyu akampamba unajua **Mhe. Moyo** akikupamba tena hakuna anayekataa.

Mhe. Spika, basi Mhe. Jumbe akampa Wizara ya Elimu. Lakini wakati Mhe. Aboud Jumbe amechafua hali ya hewa amekuja Mzee Ali Hassan Mwinyi aliyeshiriki kwenda kumchukua Mzee Mwinyi na kumpeleka ni Mzee Hassan Moyo na Mzee Mtandika. Mzee Mwinyi akapata nafasi ya kuwa Rais wa Zanzibar. Alimwambia Mhe. Moyo kwamba utakuwa Waziri Kiongozi yule pale, namruhusu kama nasema uongo atumie kanuni aipitishie kwako. Mhe. Spika, alimwambia utakuwa Waziri Kiongozi yeye akamwambia aah! niachie mimi kaka yangu yule basi alimpendekeza Seif kwa Mwinyi akamchagua kuwa ni msaidizi wake. (*Kicheko*).

Mhe. Spika, sioni ajabu kwa wale waliosema sijui Mhe. Moyo amekutanisha siajabu. Lakini cha muhimu ni kwamba kila jambo lina wakati wake, kwa hivyo wakati sasa umeshafika. Mhe. Spika, mwaka 1999 ulikaa kiti kama hicho kule ninayo hotuba yako hapa, ulitoa maneno mazito nasaha nyingi watu wapitishie mswada lakini haukupita, na waliokataa wamo humu ndani upande huu hapo na upande huu mwengine pia wapo. Mhe. Spika, leo wakati umeshafika lakini ni nani mwenye raha zaidi leo ni wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho ambaye ulitukatalia na joho lako hilo na leo unatukubalia kupitisha na naamini pale ni sawa watapitisha kauli moja.

Mhe. Spika, wewe unaona mbali ninayo *hansard* yako hapa uliyozungumza Baraza la Wawakilishi liwe na mawakili wengi na wanawake wengi. Leo mwaka mzima humu ndani hatuna mwanasheria. Mhe. Spika, ni kwamba uliona mbali, mimi nasema tena waziri tafuta, hii *hansard* kama katika ushauri wenu mnaweza kufikiria mambo ya wanasheria humu ndani, hili wazo la Mzee Kificho. Leo tunapitisha wanawake wewe umesema humu wawe hata asilimia 50. Mhe. Kificho unawapenda wanawake na ni mtetezi wa wanawake, una huruma na wanawake. Mhe. Spika, umesema hata mama nyumbani akikupa amri lazima ufuata, kwa hivyo wanawake wanafaa wawemo. Mhe. Spika, leo tena tunaongeza wanawake humu ndani, wanawake wote humu ndani wanafaa wakupende na wakuheshimu na wanakupenda na kukuheshimu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, historia haitokusahau kwani umeandika historia na ulisema mkutano wa watu wa Ulaya, mimi nilipokuwa Mwenyekiti nazungukazunguka ulisema kuwa, mimi nilipata tabu sana katika miaka yangu ya Uspika, ulieleza mwenyewe lakini wewe ni jabari ulisema mimi Ameir Kificho naunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa tena watu wapige kura ya “ndio”.

Mhe. Spika, wewe ni shujaa sio wale wanaosema hivi na huku wanasema hivi. Wewe ni shujaa ulisema wazi sheria inakataza au haikatazi nakwambieni mpige kura ya ndio. Mimi namuheshimu sana Mhe. Seif Bakari wakati Afro Shirazi na Tanu zinaunganishwa Seif Bakari alisema mimi siafiki jambo hili liwe, na akasema ikae kwenye rekodi kama Seif Bakari Omar anapinga. Mhe. Spika, na alisema kama hicho chama kipya kikija basi siombi nafasi yoyote, lakini nikipewa nitachukua na Seif Bakari mpaka kafa hajaomba nafasi.

Mhe. Spika, lakini hali ya hewa ilipochafuka aliekwa *house arrest* lakini alieleza kwenye kikao cha Kamati Kuu ya Chama kuwa mimi napinga tuwaogope sana viongozi wenye kauli mbili mbili. Mimi Mhe. Spika, wallahi billahi ningekuwa ninapinga ningesema kwenye Kamati Kuu napinga, humu ndani ningesema napinga lakini ningetoa hoja. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wale ambao wana kauli njema. Kwa hivyo, haya mambo yamemalizika lakini taifa hili leo jipya limezaliwa, Zanzibar ni mpya tuna maridhiano, tuna raha sasa Mwenyezi Mungu wale ambao bado roho zao hazijakaa sawa, Mwenyezi Mungu awasafishe roho zao, warudi nyuma waelewe.

Mhe. Spika, niruhusu nimnukuu mtu mmoja. “Anasema katika nchi fujo na vurugu hazirithiwi bali zinapandikizwa na viongozi kwa maslahi binafsi”. Mhe. Spika, ushahidi wa jambo hili uliridhika wakati wa vyama vikuu vya siasa Zanzibar vilipokaa kuzungumza muafaka ili kuondoa chuki hizo baina ya wanachama wake. Kama viongozi wa kisiasa waliweza kulifanya jambo hili mwaka 2001, kwa nini washindwe wakati huu, viongozi wa kisiasa waliopo Zanzibar wakitaka iwepo na amani basi

hakuna kizuizi lazima amani hiyo itapatikana. Mpo hapo hakuna ushahidi wa kitaalamu unaothibitisha kuwa matatizo ya Zanzibar ni zao la itikadi na siasa za kitabaka. Mhe. Spika, hapana shaka hali hii inazidishwa na viongozi wenye hamu kubwa ya kutaka kutawala.

Mhe. Spika, haya maneno kasema nani? Haya maneno mwaka 2004 alisema rafiki yangu, ndugu yangu, mpenzi wangu Mhe. Shamsi Vuai Nahodha. Mwaka 2004 alisema maneno haya April, 28. Mhe. Spika, ni kweli watu waliotaka madaraka ndio wanasema maneno haya, wala sijatunga historia.

Mhe. Spika, leo tuondoke hapa na kauli moja sote twende tukawaeleze wananchi wetu na leo tunaonekana moja kwa moja mheshimiwa. Mimi nilipokuja nilikaa pale na Mhe. Amina Iddi Mabrouk basi nikatumiwa *message* mheshimiwa nikamwambia kumbe naonekana bwana. Lakini Mhe. Kificho na sisi wenzako hapa sote ni waumini wa umoja tujenge nchi yetu, sote ni Wazanzibari, sote tumeingiliana hivyo tukijenga nchi yetu na tukishikamana basi Mwenyezi Mungu atatupa baraka, atatupa heri mambo yatakuwa mazuri na tupendane, tusameheane, tusahau yaliyopita, tujenge nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache narudia tena kusema kwamba wawakilishi wamekubali kama kuna gharama watatoa tutengeneze kituo hicho.

Mhe. Spika, la mwisho nilisema katika Baraza hili tuandike *certificate* tufanye tu-*find* sote risala au pongezi. Mimi nawafiki tutengeneze Rais bado yupo mpaka tarehe 31 sio lazima Jumatano tukipata muda siku moja tutaandaa kwenda kumpelekea. Lakini na yeye Mhe. Rais akiwa na ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi ukenda kumuona umwambie na yeye atoe barua kwa wawakilishi wote mwenyewe akaisaini kwa kuwa "*I am President Amani Abeid Karume, I am please and certisfied with Members of the House of Representative for...*

Mhe. Spika, makabidhiano ya hizo *certificate* ziwe mchana. Mimi juzi nilimualika Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nyumbani kwangu nikapiga pale biriani, ndizi mbivu na vyakula vingi tu. Kwa niaba ya nani, ilikuwa kwa niaba yako Mhe. Spika, ile ni heshima kubwa ya kamati hii na wewe. Kwa hivyo, na hiyo ya Mhe. Rais hata nyumbani kwangu hata watu 100 wataingia tena nje na viti, nitapika pilau au biriani kila mmoja aitwe aende kuchukua *certificate* yake rasmi ya Mhe. Rais kusema wazi hawa wameweza kutekeleza kujenga Zanzibar mpya. Mhe. Spika, nawauliza Waheshimiwa Wajumbe wanasemaje ni sawa juu ya hilo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe cha kupiga makofi mengi kwake na kujipongeza sisi wenyewe. Sasa kuna mambo matatu ambayo yameshauriwa na inaonekana yamekubalika moja shauri ambalo alilotoa Mhe. Haroun Ali Suleiman na kutengeneza hati maalum iliyotiwa saini na sisi sote, kuwapongeza viongozi wetu wawili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti na mtakubaliana na mimi kwamba kumpa nafasi ya kutosha Mhe. Ali Mzee Ali ilikuwa na maana sana kiasi Baraza la Mapinduzi. Pia na ndugu yetu, mwenzetu Mhe. Seif Sharif Hamad Katibu Mkuu wa Chama cha CUF na Waziri Kiongozi Mstaafu.

Pia tumuombe Mhe. Karume na yeye atengeneze hati ya kutupongeza sisi hapa na kuridhika kwake juu ya kazi nzuri ambayo tumeifanya na tumalizia kuifanya, pia kutengeneza jiwe likabaki hapo nje ikawa ni kumbukumbu yetu ikawaonesha Wajumbe wa Baraza hili waliotengeneza Zanzibar mpya wakiongozwa na ndugu yenu Pandu Ameir Kificho. Haya ndio katika mambo ambayo yameletwa na inaonekana tumeridhika sote.

Jambo la kwanza la hati ya kuwapongeza viongozi wetu wawili Mhe. Haroun alijitolea, hati itakuwa ni ya Baraza lakini alijitolea gharama zake atatoa yeye. Waheshimiwa Wajumbe masuala mengine tutajua namna gani gharama zake zinaweza zikatoka.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya machache hayo haya yote tutayafanyia utekelezaji naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora kufanya majumuisho.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya pili kusimama katika ukumbi huu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba katika uhai wangu amenijaalia kupata nafasi hii kuwa mtu wa kwanza kuwasilisha Mswada wa Sheria katika Baraza hili jipya kutokana na kule tulikokuwa tukikaa zamani. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu. Mhe. Spika, najua watoto wangu watakuja kusoma historia na watakuwa wana nguvu ya kufanya *research* juu ya mambo yanayofanyika katika Baraza ili kuweza kujua mambo mazuri kabisa ambayo yanaandaliwa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, nawashukuru Wajumbe wote kwanza kwa michango yao mbali mbali waliyotoa katika mswada huu niliwasilisha leo asubuhi. Mhe. Spika, mswada huu umekuwa mwepesi sana kwa sababu jambo lolote linalofuatana na historia basi uzito wake huwa hauonekani tena.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Mzee Ali kwa historia aliyolimina hapa najua huu mswada umekuwa mwepesi kabisa, ameanza kumimina historia tangu wakati ule alipokuwa akifanya kazi kupita katika maeneo mbali mbali kuzungumza, na leo hapa ndio amemimina biwi la historia. Kwa hivyo, kila mtu hapa anaondoka yuko macho anajua kwamba mambo ya nchi hii yako vipi.

Mhe. Spika, nataka niwataje wale ambao wamepata nafasi ya kuchangia katika mswada wangu. Mhe. Spika, kwa ujumla ni watu 32 nao ni:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir
2. Mhe. Haji Faki Shaali
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
7. Mhe. Said Ali Mbarouk
8. Mhe. Mansour Yussuf Himid
9. Mhe. Juma Duni Haji
10. Mhe. Abass Juma Muhunzi
11. Mhe. Haroun Ali Suleiman
12. Mhe. Ali Abdalla Ali
13. Mhe. Nassor Moh'd Mazrui
14. Mhe. Sultani Moh'd Mugheir
15. Mhe. Tafana Kassim Mzee
16. Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla)
17. Mhe. Rashid Seif Suleiman
18. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
19. Mhe. Zakiya Omar Juma
20. Mhe. Mzee Ali Ussi
21. Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim
22. Mhe. Machano Othman Said
23. Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini
24. Mhe. Buruhan Saadat Haji
25. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman
26. Mhe. Zahra Ali Hamad
27. Mhe. Saleh Ramadhan Feruz
28. Mhe. Mkongwe Nassor Juma
29. Mhe. Salmin Awadh Salmin
30. Mhe. Ali Denge Makame
31. Mhe. Dadi Faki Dadi
32. Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Spika, ulipotoa maelezo yako ya kusema kwamba unawaomba radhi wajumbe ni kwa hivyo wengine hutawaita kuchangia na utamalizia kwa wale watatu wa mwisho, basi wale ambao waliokuwa na nia ya kuchangia wameleta barua zao za kuchangia kwa maandishi. Mhe. Spika, nao ni:-

1. Mhe. Ame Ussi Juma
2. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga na
3. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi.

Mhe. Spika, michango ya wajumbe kusema kweli leo nimeanza kupata michango ya aina yake. Michango yote iliandamana na pongezi wakipongezwa watu mbali mbali waliofanya kazi nzuri katika masuala haya ya marekebisho ya katiba. Ni watu wachache sana ndio walikwenda katika vifungu kwa hapa na pale.

Mhe. Spika, sijui kama wale wote waliokuwa wametoa pongezi watanikubalia kwamba nizitambue pongezi zao, na waliohusika ambao wamewataja na wenyewe watakuwa wamejisikia kwa sababu televisheni yetu iko moja kwa moja kwa hiyo itakuwa wamejisikia wote waliopewa pongezi, wale ambao wamo humu ndani na wale ambao wako nje. Mhe. Spika, nadhani wajumbe wako watakuwa radhi kuona kwamba nisizirudie zile pongezi tena badala yake nizungumze vile vifungu ambavyo vimegusa katika michango yao.

Kwanza namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuwasilisha katika Baraza hili marekebisho ya yaliyofanywa na kamati yake ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya mswada huu. Kwa kweli tulipotoka katika kamati ile mswada umekuwa mzuri zaidi. Kama alivyosema Mhe. Mugheir ni kwamba marekebisho waliyoyafanya kuna mengine sisi hata hatukuyaona. Mfano, mzuri ule mmoja ambao ameutoa kusema kwamba wakati kiti cha Rais kinapokuwa wazi wale wanaochukua madaraka sisi tulitaja kwamba atakuwa Makamo wa pili wa Rais, kama hayupo atakuwa Spika, kama hayupo atakuwa Jaji Mkuu.

Mhe. Spika, lakini kamati ikatwambia ata ndio Spika, lakini nafikiri hapa ni kwamba anayekamata kiti cha Urais hatoki katika kile chama ambacho anatoka Rais. Kwa hivyo, kama Spika atakuwa hatoki katika chama kile atakuwa hafai kukamata kiti kile cha Urais kama hatoki chama kimoja na Rais. Kwa hivyo, hili ni rekebisho muhimu kabisa na tumelipokea na tumelikubali inshaallah katika hali hiyo kwa kweli limeweza kuboresha ile sheria yetu ya mswada tuliyokuwa tunakusudia marekebisho yake.

Mhe. Spika, pamoja na marekebisho mengine mbali mbali ambayo yamefanywa katika kamati yetu Mwenyezi Mungu akitujaalia tumeyaona na tumefanya marekebisho.

Mhe. Haji Faki Shaali Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora naye nampongeza kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa na kuunga mkono marekebisho haya ya katiba. Pia alisaidia kutuelimisha nchi ambazo zimefuata utaratibu huu, utaratibu wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa imefanyika katika nchi nyingi na kwa kweli si ajabu kufanyika hapa Zanzibar. Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kweli ni maendeleo na ni utanuzi wa demokrasia na unasaidia kuondoa fujo na badala yake inajenga mshikamano baina yetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali yeye amezungumzia juu ya suala maalum la vikosi vya SMZ. Mhe. Ali sijui kama pale alipo kama anayo katiba lakini angelifungua kifungu cha 121 cha katiba. Kifungu cha 121 cha katiba kimezitaja hizi idara maalum na kweli imetaja Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Kimetaja Chuo cha Mafunzo lakini haikutaja kikosi chengine.

Mhe. Spika, ninachotaka kumwambia Mhe. Ali ni kwamba katiba haikuishia hapo, kifungu cha 3 kimesema hivi "Rais wa Zanzibar anaweza ikiwa ataona inafaa kuanzisha idara nyengine yoyote kwa idara maalum. Mhe. Spika, hii ndio maana yake tumeongezewa na Kikosi cha Valantia pamoja na

Kikosi cha Zimamoto na kama Rais ataona inafaa kuanzisha kikosi chengine basi bila shaka ataanzisha.

Mhe. Spika, suala kama hili aliliulizia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej kama kawaida na yeye ametoa pongezi kwa watu mbali mbali, lakini alisema kwamba anaomba katika kile kifungu cha uteuzi wa rais, pamoja na kuwa kuna asilimia 40 wanawake wamepewa, lakini si vibaya kwamba na rais pia akateuwa na wanawake wakaongeza idadi. Si wazo baya ni zuri na bila shaka litakuwa linawafikia vizuri. Isipokuwa ninachotaka kusema na kutahadharisha Baraza hili kwamba serikali ilipoamua kuweka hii asilimia 40 ya wajumbe wote, Mhe. Spika, wajumbe wa Baraza letu ni 81.

Mhe. Spika, katika wajumbe 81 asilimia 40 ni wajumbe 32. katika hali halisi ya sasa hivi kama ikitokea kuna wanawake angalau wawili au watatu kutoka kwenye majimbo maana yake ndani ya Baraza kuna wajumbe 34 kama watakuwa wawili na 35 kama watakuwa watatu. Wakiwa 34 basi Mhe. Spika, humu ndani tutabakia wanaume 47, na kama rais ataendelea kuteuwa zaidi basi kuna uwezekano wa kubakia wanaume 45, naona utafika wakati na wanaume nao wataanza kudai haki watasema sasa na sisi wameshakuwa hawa wanaongezeka kila siku.

Lakini Mhe. Spika, ninachosema hapa nia hasa ni asilimia 50 kwa 50. kwa hivyo, si vibaya kama watakwenda kwenye majimbo tukawa sawa sawa 50 kwa 50 yaani ikawa 40 hawa na 40 hawa itakuwa ni vizuri kabisa, hiyo sio mbaya wakaingia katika maeneo hayo. Lakini hata hivyo, wazo limesikika na litazingatiwa.

Mhe. Asha Bakari Makame yeye ametoa pongezi, namshukuru sana kwa pongezi zake na ameunga mkono na kuhimiza suala la kufanya kazi kwa pamoja sasa hivi. Lakini amewataka hasa wale ambao kwa bahati mbaya wameanguka katika mchakato kwamba sasa hivi ni vizuri tukashirikiana tukajenga nchi yetu kwa pamoja.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary kama tunavyojua yeye ni mwanasheria, namshukuru sana kwa mawazo yake aliyoyotoa katika mswada huu na nimevutiwa sana aliposema kwamba, katiba ni tochi inayotoa mwanga. Kwa hivyo, nchi yetu sasa kwa marekebisho haya bila shaka itang'ara. Nimepata matumaini makubwa kwa sababu yametoka katika mdomo wa mwanasheria. Hivyo, nimepata matumaini kwamba nchi yetu itakuwa ina katiba iliyonzuri ikilinganishwa na nchi nyingi nyenginezo.

Mhe. Said Ali Mbarouk yeye ametoa wito wa kumuenzi Rais wa Zanzibar ambapo Mheshiamiwa umeshatoa maelezo mbali mbali kuhusu suala hili. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magaribi na yeye katika uzinduzi wa barabara ya kurukia ndege pale, alipendekeza kuanzishwa kwa utengenezaji wa nishani. Ninavyojua kuanzia siku ile Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi anaaza kukusanya michango sijui keshapata ngapi, lakini najua michango imeanza kutoka pale pale uwanjani nadhani na wengine ni vizuri wakapeleka ikasaidia kutengeneza hiyo nishani yenyewe iliyokusudiwa.

Mhe. Said Ali pia amezungumza suala la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Spika, Mhe. Ali Mzee Ali ameshalijibu suala hili. Lakini kwa ufupi tu, nina maelezo kidogo nimepata kutoka kwa wanasheria wangu juu ya suala hili ni vizuri nikayasoma.

Mhe. Spika, yanasema kwamba, katika mfumo wa Serikali Jamhuri maana yake kwa ufupi ni serikali inayoongozwa na watu badala ya serikali ya kifalme. Hivyo hata kama hukutamka hivyo, nchi yenye serikali ya watu wote badala ya serikali ya kifalme nchi hiyo ni jamhuri. Kwa mfano, Marekani ni jamhuri lakini neno 'Jamhuri' halimo katika jina la nchi hiyo. Hivyo si lazima neno 'Jamhuri' liwemo katika jina la nchi ili nchi hiyo iwe jamhuri.

Mfano wa nchi iliyotumia neno 'Jamhuri' kwa maana halisi ya kitaalamu ni Marekani ambayo chini ya ibara ya nne ya Katiba ya Marekani imeyahakikishia majimbo yote Mfumo wa Serikali ya Jamhuri. Sababu ya pili ni kwamba mara nyingi unapoita nchi jamhuri imezoeleka kuwa ni taifa lenye uwezo wa mahusiano kamili ya kimataifa. Kwa mujibu wa makubaliano ya Katiba ya Muungano jambo moja

ambalo Tanganyika na Zanzibar walikubaliana kuunganisha ni jamhuri na ndio maana taifa letu linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, mwanasheria anatoa indhari hapa kwamba si sahihi kwa kutumia neno 'Jamhuri'. Na tujue kwamba katika suala hili *sovereignty* mbili tumezichanganya, ile ya Tanganyika na hii ya Zanzibar.

Mhe. Said vile vile amezungumzia juu ya habari ya kinga ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambapo bahati nzuri pia limezungumziwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Spika, hapa ninachotaka kusema tunayo sheria ya kinga sisi ambayoa inampa uwezo Mhe. Mwakilishi awe na kinga wakati anapofanya shughuli zake za Baraza. Katika hali hiyo shughuli za Baraza zimetajwa katika katiba nazo ni zile nne zilizotajwa katika katiba yetu. Sasa zile ndizo zilizochukuliwa hatua ya kuandikwa katika haya marekebisho yetu. Lakini sheria ile nafikiri imefafanua zaidi kwamba anapokuwa katika shughuli zake, lakini tutapata tabu kufafanua anapokuwa katika shughuli zake.

Kwa sababu wakati mwengine Mheshimiwa anaweza kuwepo katika shughuli zake kwa jambo la manufaa, lakini wakati mwengine ghadhabu tu zinaweza zikamfanya mtu aonekane katika shughuli zake kumbe anafanya *instigation* za mambao ya ajabu ajabu. Kwa hivyo, wanasheria wanasema hili suala ni bora likakaa kwanza liendeleo hivi lilivyoandikwa katika katiba yetu kwenye marekebisho yaliyofanywa sasa hivi.

Kuna suala la Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo Mhe. Said nayo pia ameiulizia. Mhe. Spika, kuundwa kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni sehemu ya mpango mkubwa wa mageuzi ya utumishi wa umma Zanzibar (*Public Service Commission*). Mpango huu umetekelezwa katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania Bara. Madhumuni makubwa ya mpango huu ni kuleta ufanisi katika utendaji wa serikali.

Miongoni mwa hatua zinazochukuliwa katika kutekeleza mpango huu, ni kuunda Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Kamisheni hii itakwua na kazi kubwa ya kumsaidia Mhe. Rais katika kusimamia utendaji wa serikali kwa ujumla. Kamisheni haitachukua wala kuingilia kazi za Tume ya Utumishi wa Serikali, Tume ya Utumishi wa Mahkama wala Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi na Tume ya Utumishi wa Idara Maalum, bali itakuwa na kazi ya kuhakikisha kuwa zinatimiza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, taratibu na maadili ya utumishi wa umma.

Hili tutasaidia kuwa na viwango vya nidhamu na utendaji vinavyofanana. Aidha, kamisheni itakuwa chombo cha kutanabahisha na kuzielekeza tume kufuata sheria, kanuni au maadili pale tume yoyote itapoonekana haifanyi hivyo katika kazi zake.

Kwa mfano, chini ya mfumo mpya wa Utumishi wa Umma, Tume yoyote ya Utumishi itatakiwa kufuata njia za wazi na zisizokuwa na upendeleo wakati wa kuajiri wafanyakazi. Iwapo Kamisheni itaona kwamba tume haikufuata taratibu zinazokubalika inaweza kutengua utaratibu wote na kuagiza ufanywe upya kwa kufuata taratibu.

Kazi nyengine kubwa ya Kamisheni itakuwa ni kuhakikisha kuwa maslahi, mafao na mazingira ya kazi ya watumishi hayapishani sana baina ya watumishi wanaosimamiwa na Tume zote za Utumishi. Jambo hili litaleta haki zaidi kwa watumishi wa umma badala ya mfumo uliopo sasa.

Kamisheni ya Utumishi itakuwa ikitoa taarifa za mwaka juu ya utumishi wa umma chini ya tume zote. Taarifa hizo zitakuwa zikiwasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi ili kupata michango na maelekezo zaidi ya kuimarisha utumishi.

Kamisheni itakuwa na wajumbe ambao watapendekewa na Spika, Jaji Mkuu na wakati huo huo viongozi na hivyo haitakuwa na muhimili mmoja tu, bali itashirikisha ipasavyo muhimili yote katika kuiunda na hata kupata taarifa zake. Hivyo kwa ujumla kuundwa kwa kamisheni ni sehemu ya

jitihada za kuimarisha utendaji wa jumla wa serikali na vyombo vyake vyote. Hiyo ndio nia ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, ni kweli neno ‘Serikali’ lipo katika kifungu 116(2)(a) na (b) kifungu cha 60 cha mswada kama alivyoyaona Mhe. Said Ali Mbarouk kuwa yanapaswa yafutwe. Ni makosa ya uandishi, lakini Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliyaona na hivyo yanapaswa yafutwe kwa vile yanaondoa dhana ya kuwa sio tume zote zitazoajiri watumishi serikalini. Ni tume ya Utumishi wa Serikali ambayo zamani tukiita Tume ya Uajiri pekee ndio itafanya hivyo, tume nyengine itaajiri kwa taasisi zao husika. Yaani sio kwamba tume zote ndio zitakuwa zinaajiriwa pale, tume nyengine zitafanywa kwa taratibu zao walizonazo wao wenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na yeye ametoa pongezi nyingi sana katika mchango wake. Mhe. Juma Duni ametoa pongezi na amezungumza jambo moja muhimu sana la kukumbuka tunakotoka sisi tuliokusanyika katika Baraza hili.

Nakubaliana naye kwamba ni kweli wakati ule ulikuwa ukishafika darasa lako kama umeweza, kwa sababu unasoma mpaka darasa la sita ninavyofahamu mimi, kama umeweza kulipa basi utasoma darasa la saba na la nane, kama umeweza kulipa tena ndio utaendelea kusoma darasa la tisa mpaka kumaliza la kumi na mbili, kama umeweza lakini. Kwa sababu wengi ambao walifika darasa la sita lakini walishindwa kuendelea katika darasa la saba na la nane, walishindwa kabisa na wala *fee* kwa wakati huo Mhe. Spika, haikuwa kubwa.

Sheha anakuombea kutoka shilingi thalathini na mbili zilizowekwa pale mpaka zinabakia shilingi tano tu, lakini shilingi tano wazee wetu walikuwa wanashindwa kuzilipa kabisa. Kwa hivyo, wengi walikuwa wakishindwa wakati ule, hiyo shilingi tano sasa hivi labda kachori, lakini kwa wakati huo ilikuwa huwezi kuipata kabisa hiyo shilingi tano.

Sasa ni kweli Mhe. Juma Duni Haji amekumbusha kwa hvyo, hatuna budi kukiri kwamba Mapinduzi yametusaia sana sote tuliokuwa hapa na watoto wetu walioko nje ya hapa, kwa kutangazwa elimu bila ya malipo na sisi ndio tukapata nafasi ya kuendelea, lakini kweli.

Mhe. Juma Duni leo angekuwa mvuvi na wala nisingemjua kwa sababu sasa hivi angekuwa yuko Mkokotoni anauza samaki wake na mimi sasa hivi ningekuwa mkwezi na nimeshapata kibyongo kwa kupanda minazi kwetu kule shamba. Hiyo ndio hali ambayo tungekuwa wengi wetu tuliopo hapa, tumshukuru Mwenyezi Mungu katika hali hiyo.

Mhe. Abass Juma Muhunzi amezungumza mambo ya pongezi lakini pia ametoa indhari kwamba Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ni vizuri ikawa *serious* katika kufanya mambo yake kwa nia ya kuleta maendeleo. Pia alionya hasa kwamba, uimarishaji wa Afisi ya Spika ni jambo muhimu sana na kwa kweli lifanyike.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye pia ametoa pongezi lakini pia amekumbusha hali halisi iliyokuwa ikitukuta sisi kama alivyokumbusha Mhe. Juma Duni.

Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu Mhe. Spika, kwa kazi anayoifanya katika jimbo lake kwa ajili ya kuwaelimisha watu kukubali suala zima la Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuifafanua wazi kwa wananchi wake. Ni juzi tu alikuwa anatoka katika kazi hiyo. Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye alikuwa ni mjumbe wa kamati na yeye vile vile ametoa pongezi za kutosha juu ya masuala hayo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii amezungumza maneno mazito na kwa kweli nampongeza kwa sababu kweli wananchi walifikiria suala alilolisema Mhe. Waziri wa Afya kwamba, Mhe. Amani alichokifanya ni kukusanya Wazanzibari pamoja sio kuuza nchi, alichokifanya ni kukusanya Wazanzibari pamoja tuwe kitu kimoja. Amezungumza kwa lugha yake ya mjini yenye kuvutia sana sisi wengine inatupa tabu sana kuiga lugha hiyo, lakini Mhe. Waziri wa Afya anaiweza na mara nyingi akisema huwa napenda sana kumsikiliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi amezungumza pongezi na amehimiza sana masuala ya amani na utulivu. Ni kweli nakumbuka ile siku aliyosema kwamba, alisimamishwa Kizimbani na akaambiwa usipite katika njia hiyo, kwa bahati na mimi nilitokea nyuma yake. Akanambia maalim mimi nimeambiwa nisiende huko sijui wewe kama ndio utakwenda, lakini kwa bahati tukenda sote yeye mwenzangu akatembea kwa miguu akawa *bodyguard* wangu anapita chini ya gari yangu mpaka nikavuka pale. Namshukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Ali Salim amesema jambo na kusema kwamba, kila jambo linakwenda kwa wakati. Mwenyezi Mungu amepanga kwamba mambo mazuri Unguja tuyafanye kwenye kipindi hiki na tuyafanye ndani ya jengo hili jipya. Ndio leo wakati umefika tumeyafanya ndani ya jengo hili jipya masuala haya. Kwa hivyo, kila kitu na kinapangwa kwa wakati, sisi tunaweza tukapanga yetu tu, lakini kwa kweli Mwenyezi Mungu ndiye anayefanikisha yale anayoyataka, hayo tulioyapanga akitaka tutafanikiwa kama hataki tatafanya yale ambayo anayataka yeye. Hiyo ndio hali hlisi kusema kweli.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na yeye vile vile amezungumzia suala la Umoja wa Kitaifa na amelitilia mkazo sana suala hili. Mhe. Rashid Seif na yeye vile vile amepongeza kama nilivyosema mwanzo na akasema kwamba anampongeza sana Mhe. Amani Abeid Karume kwa uwezo alionao na akakubali kuzungumza pamoja na Maalim Seif Sharif na wakafikia maridhiano. Alikuwa na madaraka, uwezo na kila kitu, lakini akakubali kufikia maridhiano. Ni suala zuri kabisa.

Mhe. Ali Mzee na yeye ameunga mkono sana suala hili la Umoja wa Kitaifa. Mhe. Wajumbe wote waliomo katika Baraza hili wameunga mkono suala hili la Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini amezungumza juu ya woga wa wananchi, wananchi wanadhania kwamba labda neno ‘Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar’ litaondoka. Ninachotaka kusema katika suala hili ni kwamba, nchi yoyote inaendeshwa na katiba na katiba bado inasema kwamba, Zanzibar kutakuwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tunaemchagua ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Huyu tutakayemchagua hilo ndilo jina lake.

Baraza la Mapinduzi bado litakuwemo na katika vifungu vyote lime na litaendelea kuwemo, lakini itakuwa ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni ya Umoja wa Kitaifa ndio marekebisho ambayo tumeyafanya. Hio ndio hali halisi ambayo tunaifanya.

Kwa hivyo, watu hawana sababu ya kuwa na wasi wasi. Kitu muhimu sasa tunakwenda katika amani, utulivu na umoja. Wananchi wote waelimishwe kama walivyosema wajumbe wengi wafahamu vizuri suala hili na wakubaliane nalo twende kwenye uchaguzi Oktoba kwa maelewano, utulivu, kila mtu achague chama anachotaka pasina matatizo ya aina yoyote. Hilo ndilo suala muhimu kabisa uchaguzi wetu uwe salama na amani kwa sababu taryari wazee wetu wamesharidhiana na nimesema tangu asubuhi hapa kwa kweli maridhiano waliofikiwa viongozi wetu wale ndio lengo hasa la Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na ndio maana ikatoka sheria ya Nam. 6 ya mwaka 1954. kwa hivyo, watu hawana haja ya kuwa na wasi wasi juu ya suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi naye amefafanua juu ya maana ya Serikali ya Mseto kama alivyowaambia watu wake huko kuwa Serikali ya Mseto mbali na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mbali, sisi tunakwenda kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa hatwendi katika Serikali ya Mseto.

Serikali ya Mseto mara nyingi hufanywa baada ya uchaguzi, kama mtu kapata viti havikumtosha basi humuomba aliyenavyo waongezwe wafanye mseto. Sisi hatufanyi hivyo, tunakubaliana kabisa kikatiba kwamba tutakwenda kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi ametoa hadithi. Ilikuwa ni hadithi, lakini nilikuwa nikimsikiliza vizuri. Ni hadithi yenye maana sana namna Mandela alivyorudi kuwaunganisha watu wa Afrika ya Kusini kwa ule mchezo ambao Mhe. Waziri wa Mawasiliano

aliutaja kwamba watu walikuwa wanauchukia kwa sababu ulikuwa ni mchezo wa Makaburu. Lakini kwa sababu Mhe. Nelson Mandela aliutilia mkazo mchezo ule na ukawa unachezwa kwa kuwakusanyisha wote kabisa, Waafrika ikawa wakati mwengine wanasusiana kwenda katika mchezo, lakini ilifika hatua walikubaliana na kukumbatiana hiyo ndio hali hilisi.

Kwa hivyo, huu ni mfano mzuri ambao viongozi wetu wameuchukua sasa hivi. Sisi tunaona tabu kwenda katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa lakini nina hakika tutafahamu na tutafaidika na matunda yake, sina wasi wasi katika hili.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira na yeye vile vile amezungumzia masuala ya kuunga mkono. Mhe. Zakiya Omar Juma naye amezungumza suala hilo na ameshukuru sana kwa kupata nafasi ya kufanya kazi na Mhe. Ali Mzee. Kwa sababu alifaidika sana na taaluma aliyopata pale kutoka kwa Mhe. Ali Mzee.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nimeshasema kwamba suala lake la vikosi lile liko katika kifungu cha 121(3) ambapo rais pamoja na kuwa havikutajwa pale, lakini ilipoandikwa vilitajwa vile vilivyokuwepo, lakini sasa hivi vyengine vinavyoongezeka vinakwenda kwa kila kifungu cha 121(3).

Mhe. Saleh Ramadhan Ferouz naye ameshukuru sana kwamba kweli sasa hivi hakuna anayeweza kuiharibu historia ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa sababu sisi wenyewe tuliomo katika Baraza hili tumeshafika hatua ya kulinda ile historia yetu kwamba, Pemba na Unguja ni nchi moja na sio muungano. Amezungumza masuala ya rais kupatiwa shahada na mambo mengineyo kama walivyozungumza wengine, ambapo Mhe. Spika, umeshayazungumza masuala hayo. Mhe. Mkongwe Nassor Juma naye masuala hayo hayo.

Mhe. Salmin Awadh amegusa vifungu, kimoja kile kinachohusu masuala ya kinga ambayo nimesema kama kilivyokuwa hapo zamani hakikufafanua vya kutosha juu ya kinga za wajumbe hasa wanapokuwa katika kamati teule. Lugha iliyotumika ni pana lakini sio ya wazi. Ili kuondoa utatanishi ndio maana kimeandikwa kwa lugha ya wazi.

Mhe. Spika, nimesema kwamba kazi za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni zile ziliomo nne, lakini pia sheria yetu inaruhusu kwa mtu anapokuwa katika kazi zake za kawaida za kushughulikia Baraza anapata kinga vile vile Mhe. Spika.

Suala jengine ambalo Mheshimiwa amelizungumza kifungu cha 86 ambacho kimefanyiwa marekebisho, samahani Mhe. Spika, kidogo nifunue nione yale marekebisho yaliyofanywa kwenye kifungu cha 86. Kifungu hiki Mhe. Spika, ndio kile kinachohusu masuala ya kinga, limeondoka lile neno 'mahala pengine popote'. Lakini kifungu chengine ambacho amekizungumza ni kifungu cha 34. Hicho nataka nikifafanue kidogo.

Kifungu cha 34 kinasema bila ya kujali masharti ya vifungu vya 28(3) na 30(1)(b) vya Katiba, endapo mtu anayemfuata rais kwa madaraka atashika kiti cha rais kwa kipindi kinachopungua miaka minne, ataruhusiwa kugombea nafasi ya raia mara mbili.

Hii maana yake tumefanya uchaguzi, tumempata rais, amefanya kazi kwa mwaka mmoja, baada ya mwaka mmoja likatokea lisilotazamiwa dharura inayomfanya rais kukiacha kile kiti akaingia rais mwengine pale. Kwa hivyo, ile miaka minne atakayomaliza yule rais kipindi kinachopungua hii imetimia, ikitimia miaka minne, ngoja niisome tena.

“Endapo mtu anayemfuata rais kwa madaraka, akashika kiti cha rais kwa kipindi kinachopungua miaka minne, ataruhusiwa kugombea nafasi ya rais mara mbili, endapo baada ya miaka mitatu ndio rais yule ameondoka madarakani kaja rais kakamata mika miwili basi huyu atamaliza ile miaka miwili na akishamaliza atagombea tena mara mbili.

Kwa hivyo, atakuwa yeye kapata miaka miwili na kule kapata miaka mitano na mitano atakuwa yeye kafanya kazi kwa muda wa miaka 12. Lakini ikiwa miaka minne basi atagombea mara moja tu, yaani miaka minne ile ya kwanza na miaka mitano atakayoipata mara ya pili, itakuwa miaka yote tisa. Ndicho tunachokirekebisha katika kifungu hiki. Kwa hivyo, hatagombea tena atakuwa amepata ile miaka tisa ndio maana ya kifungu hiki.

Sasa kama kuna neno Mhe. Salmin Awadh Salmin amesema limeachana hapo, basi nampa nafasi ya kuja kuzungumza na mimi na tukutane na wanasheria wetu ili iweze kukaa vizuri. Lakini ukilitizama kwa ghafla utaona kwamba inafahamika kuwa rais aliyekaa kwa muda wa miaka miwili atagombea vipindi viwili. Miaka miwili, mitano, halafu mitano, aliyekaa mwaka mmoja atagombea mwaka mmoja ule halafu mitano halafu mitano.

Lakini aliyekaa miaka minne yaani baada ya mwaka mmoja tu, kaingia madarakani rais huyo aliyefuatia kwa madaraka atachukua miaka minne ile halafu atachukua mitano. Kwa hivyo, atagombea mara moja kwa ile miaka ya kule mbele. Hiyo ndio iliyokusudiwa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni mdogo na tulipanga tumalize saa mbili kamili ambapo bado dakika kidogo tu. Sasa tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi atoe hoja ya kuongeza muda mpaka tutapomaliza kazi hii.

Mhe. Waziri hayupo, basi atamaliza yeye mwenyewe ataongeza muda.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala bora amebakisha suala moja tu kulijibu na muda wa kuahirisha kikao unakaribia, naomba kutoa hoja kwamba, Baraza liendeleo hadi Mhe. Waziri atapomaliza kujibu hoja zake. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mwenyewe atapiga kura hapo hapo alipo. Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: (Anaendelea) Mhe. Spika, kuna suala moja tu limebakia ambalo ni vizuri nilizungumze nimelizungumzwa na Mhe. Dadi Faki Dadi kuhusu kwa nini Mhe. Rais ashauriane na Kiongozi wa Upinzani Barazani, badala ya kwenda kushauriana na Makamo wa Kwanza Rais ambaye anae kule kule ndani.

Kwa ufupi jibu lake ni kwamba huyu Kiongozi wa Upinzani mle ndani anashughulikia chama zaidi ya kimoja kwa hivyo ndio maana anashauriana nae mle ndani ya Baraza. Yule Makamo wa Rais ana wanachama wake tu mle lakini Kiongozi wa Upinzani ndani ya Baraza anakuwa na chama zaidi ya kimoja ambavyo viko kwenye upande wa upinzani.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuhoji nataka nitoe maelezo kidogo. Huu ni Mswada wa Marekebisho ya Katiba utaratibu wake tunatakiwa tupate theluthi mbili ya wajumbe. Wajumbe wetu ni 81 theluthi mbili yake ni wajumbe 54. Kazi hiyo tutaifanya mara baada ya kutoka kwenye Kamati ya Baraza Zima pale ambapo Mhe. Waziri atakuja kuomba sasa Baraza likubali vifungu vile ambavyo tumevipitisha katika Baraza zima. Tutawaomba Makatibu wetu wahesabu wajumbe.

Kwa kawaida kwenye masuala kama haya huwa tunaita *roll call*. Lakini kwa mazingira niliyoyaona humu ndani hiyo inaweza ikatuchukua muda mkubwa kwa kuchukua orodha ile tukaanza kuita mmoja mmoja. Tutakachokifanya tutakwenda kwa utaratibu wa kawaida wa kunyanyua mikono kwa wale wanaounga mkono hoja na kuwataka Makatibu wetu wahesabu idadi ya wale waliounga mkono na hatimaye wahesabu wale ambao hawaungi mkono hoja hii. Shughuli hiyo tutaifanya mara baada ya kutoka kwenye Kamati ya Baraza Zima Waziri atakapoomba sasa mswada wake ukubaliwe na hatimaye katika kusomwa mara ya pili. Huo ndio utaratibu tutakaokwenda nao.

Hapa kimsingi tunataka tukubaliane au kukataa ile hoja ambayo baada ya mjadala na majumuisho aliyotoa kama tunaafiki au la. Lakini hesabu kamili itakuja baada ya kupitia ule mswada mzima kifungu kwa kifungu na hapo ndipo tutahesabu zile kura. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

Basi sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuipitia mswada kifungu baada ya kifungu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naelewa matatizo tutayarekebisha ili tuone kwamba hali hiyo haitokei tena.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984

SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2 - Kusomwa.

SEHEMU YA PILI MAREKEBISHO MBALI MBALI

Kifungu cha 3 - Marekebisho ya kifungu cha 1 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4 - Marekebisho ya kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 5 - Kuongeza kifungu kipya cha 2 A. Kifungu kipya kinachorekebisha kifungu cha 9 (3) cha Katiba.
Kifungu cha 6 - Marekebisho ya kifungu cha 10 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7 - Marekebisho ya kifungu cha 12.
Kifungu cha 8 - Marekebisho ya kifungu cha 24.
Kifungu cha 9 - Marekebisho ya kifungu cha 25 A.
Kifungu cha 10 - Marekebisho ya kifungu cha 26 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11 - Marekebisho ya kifungu cha 27.
Kifungu cha 12 - Marekebisho ya kifungu cha 28.
Kifungu cha 13 - Marekebisho ya kifungu cha 29.
Kifungu cha 14 - Marekebisho ya kifungu cha 30.
Kifungu cha 15 - Marekebisho ya kifungu cha 32.
Kifungu cha 16 - Marekebisho ya kifungu cha 33 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 17 - Marekebisho ya kifungu cha 34.

Kifungu cha 18 -	Marekebisho ya kifungu cha 37.
Kifungu cha 19 -	Marekebisho ya kichwa cha maneno.
Kifungu cha 20 -	Marekebisho ya kifungu cha 39 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 21 -	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 39 A pamoja na
marekebisho yake.	
Kifungu cha 22 -	Marekebisho ya kifungu cha 40 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23 -	Marekebisho ya kifungu cha 41 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24 -	Marekebisho ya kifungu cha 42.
Kifungu cha 25 -	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 42 A.
Kifungu cha 26 -	Marekebisho ya kifungu cha 43.
Kifungu cha 27 -	Marekebisho ya kifungu cha 44.
Kifungu cha 28 -	Marekebisho ya kifungu cha 45.
Kifungu cha 29 -	Marekebisho ya kifungu cha 46.
Kifungu cha 30 -	Marekebisho ya kifungu cha 47.
Kifungu cha 31 -	Marekebisho ya kifungu cha 48.
Kifungu cha 32 -	Marekebisho ya kifungu cha 49 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 33 -	Marekebisho ya kifungu cha 50 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 34 -	Marekebisho ya kifungu cha 54.
Kifungu cha 35 -	Marekebisho ya kifungu cha 55.

Mhe. Spika: Kifungu hicho kimefutwa ndio marekebisho yenyewe.

Kifungu cha 36 -	Marekebisho ya kifungu cha 57.
Kifungu cha 37 -	Marekebisho ya kifungu cha 61.
Kifungu cha 38 -	Marekebisho ya kichwa cha maneno.
Kifungu cha 39 -	Marekebisho ya kifungu cha 63.
Kifungu cha 40 -	Marekebisho ya kifungu cha 64.
Kifungu cha 41 -	Marekebisho ya kifungu cha 66 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 42 -	Marekebisho ya kifungu cha 67.
Kifungu cha 43 -	Marekebisho ya kifungu cha 72.
Kifungu cha 44 -	Marekebisho ya kifungu cha 73.
Kifungu cha 45 -	Marekebisho ya kifungu cha 74.
Kifungu cha 46 -	Marekebisho ya kifungu cha 78.
Kifungu cha 47 -	Marekebisho ya kifungu cha 79.
Kifungu cha 48 -	Kuongeza kifungu kipya cha 80 A pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 49 -	Marekebisho ya kifungu cha 81.
Kifungu cha 50 -	Marekebisho ya kifungu cha 84.
Kifungu cha 51 -	Marekebisho ya kifungu cha 86.
Kifungu cha 52 -	Marekebisho ya kifungu cha 91.
Kifungu cha 53 -	Marekebisho ya kifungu cha 92.
Kifungu cha 54 -	Marekebisho ya kifungu cha 96.
Kifungu cha 55 -	Marekebisho ya kifungu cha 99 A.
Kifungu cha 56 -	Marekebisho ya kifungu cha 102.
Kifungu cha 57 -	Marekebisho ya kichwa cha maneno.
Kifungu cha 58 -	Marekebisho ya kifungu cha 116.
Kifungu cha 59 -	Marekebisho ya kifungu cha 117.
Kifungu cha 60 -	Marekebisho ya kifungu cha 118 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 61 -	Marekebisho ya kifungu cha 120.
Kifungu cha 62 -	Marekebisho ya kifungu cha 121.
Kifungu cha 63 -	Marekebisho ya kifungu cha 122.
Kifungu cha 64 -	Marekebisho ya kifungu cha 124.
Kifungu cha 65 -	Marekebisho ya kifungu cha 128.
Kifungu cha 66 -	Marekebisho ya kifungu cha 129.
Kifungu cha 67 -	Marekebisho ya kifungu cha 134.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawatahadharisha tunapokaa inaonekana tukae kwa *slow motion* ili kuhakikisha kwamba tunakuwa salama.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaoafiki mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono tusebiri tuhesabiwe.

Katibu: Mhe. Spika, ni 75. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Wajumbe wanaokataa hoja hii ya mswada huu wanyanyue mikono, hakuna. Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 2010 usomwe mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoafiki mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono.

Katibu: Mhe. Spika, ni 75. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe pengine kaingia mjumbe mpya. Wale wanaokataa mswada huu hakuna.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa kunisaidia vya kutosha kabisa katika kuendesha kikao hichi cha leo kuanzia asubuhi. Nakushukuruni zaidi hasa kwa wingi wa wajumbe mliohudhuria leo. Tukielewa kwamba Baraza hili tunapungukiwa na mjumbe wetu mmoja ambaye nafasi yake bado iko wazi mpaka leo Marehemu Mhe. Soud Yussuf Mgeni na wenzetu wawili wanaoumwa Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Adam Mwakanjuki.

Vyenginevyo wajumbe watatu tu ukiachia hao ndio hawakufika kwenye Baraza hili nao naamini kwa dharura mbali mbali ambazo wamepata tangu asubuhi, wamepata misiba, wengine wawili wamekwenda Pemba kwa kufiliwa na jamaa zao. Mhe. Abubakar Khamis Bakary aliniarifu hivyo na ndio ikafanya kwamba idadi iwe na upungufu kama wajumbe 6 kwa ujumla wake.

Kwa hiyo, nakushukuruni kwa kujitokeza kwa wingi sana na tukaamua jambo hili muhimu kwa mustakbali wa nchi yetu na hatima ya nchi yetu na watu wake.

Baada ya machache hayo basi, Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niaharishe kikao hichi hadi kesho tarehe 10 Agosti, 2010 saa 3:00 barabara za asubuhi na tusingahau tunakuja hapa tusije tukaenda kwenye Ukumbi ule wa zamani. Ahsanteni sana.

*(Saa 2:17 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 10/08/2010
saa 3:00 asubuhi)*

